

**USIMULIZI KATIKA RIWAYA TRILOJIA YA KISWAHILI: MFANO WA
*SIRI SIRINI***

LUCYLINE NJERI MWONGELA

**Tasnifu Iliyowasilishwa katika Shule ya Mafuzu kwa Minajili ya Kutosheleza
Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha
Chuka**

CHUO KIKUU CHA CHUKA

NOVEMBA, 2021

UNGAMO NA IDHINI


Ungamo


Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada au stahada katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi.......... Tarehe.....15/11/2021
Lucyline Njeri Mwongela
AM12/7854/12

Idhini

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Chuka.

Sahihi.......... Tarehe.....15/11/2021
Profesa John M. Kobia
Idara ya Fani
Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihi.......... Tarehe.....15/11/2021
Daktari Allan Mugambi
Idara ya Fani
Chuo Kikuu cha Chuka

HATILINZI

©2021

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kupiga chapa, kutafsiri, kuhifadhi kwa mfumo wowote ule au kutoa sehemu yoyote ile ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia marehemu babangu Bedford Mati na mamangu Virginia Nyamu.

SHUKRANI

Namshukuru Mungu kwa nafasi, neema na uvumilivu katika masomo. Shukrani ziwaendee wasimamizi wangu Profesa John M. Kobia na Daktari Allan Mugambi kwa mawaidha yao yaliyochangia ufanisi wa kazi hii. Namshukuru Bwana Enock Matundura kwa ushauri wake. Nawashukuru Profesa David Nyaga Bururia na Bi Rosemary Njeri Gitari kwa kunihimiza na kunipa moyo. Nawashukuru wanafunzi wenzangu Evangeline Makena na Janerose Igoki kwa kunihimiza. Namshukuru mume wangu Protasio Mwongela, watoto wetu Rowan Mwende, Brian Munene, Byron Murithi, Antony Mwangi, Edith Nkirote, Joan Nyabate na wajukuu wetu Kyle Maina, Naima Njeri, Malik Lintari na Myles Omesa kwa uvumilivu wao wakati wa shughuli hii ya masomo. Aidha, kuna wengine wengi waliochangia kazi hii lakini sijaweza kuwataja. Nawashukuru pia na kuomba radhi kwa vile singeweza kutaja kila mtu. Kwenu nyote naomba Mungu awabariki.

IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia usimulizi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini* iliyotungwa na Rocha Chimerah (2013, 2014). Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* imeandikwa katika msururu wa riwaya tatu: *Siri Sirini 1, Mshairi na Mfungwa* (2013), *Siri Sirini 2, Mpiga Mbizi Kilindini* (2014) na *Siri Sirini 3, Mtihani wa Mwanamke* (2014). Riwaya hizi tatu zinafanana kimaudhui, kiwahasika, kimandhari na kimtindo. Malengo ya utafiti yalikuwa kubainisha mbinu mbalimbali za usimulizi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini* na kuchunguza jinsi wahusika walivyosawiriwa katika usimulizi wa riwaya hii. Utafiti uliongozwa na nadharia ya naratolojia iliyoasisiwa na Plato na kuendelezwa na Propp (1968), Claude (1970), Barthes (1975), Todorov (1977), Bal (1999) na Fludernik (2009). Nadharia ya naratolojia hutumika katika hadithi, mfuatano wa matukio katika matini kiwakati, kutambua njia na jinsi mbalimbali za kusimulia hadithi na kipengele cha wahusika. Mihimili ya nadharia ya naratolojia imesaidia katika kuihakiki riwaya hii kwa kubainisha mbinu za usimulizi zinazotumika kuisimulia hadithi na usawiri wa wahusika. Utafiti ulijikita maktabani ambapo vitabu, tasnifu na maandishi yaliyoangaza masuala ya nadharia, usimulizi na trilojia yalisomwa. Mbinu ya sampuli ya kimaksudi ilitumika katika uteuzi wa riwaya trilojia ya *Siri Sirini*. Ukusanyaji wa data ulitokana na usomaji wa riwaya trilojia ya *Siri Sirini*. Mafungu yaliyoonyesha mbinu mbalimbali za usimulizi na maneno ya wahusika yalinukuliwa. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa mbinu ya maelezo kulingana na malengo ya utafiti. Utafiti ulibainisha kuwa riwaya trilojia ya *Siri Sirini* imesimuliwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za usimulizi kama vile usimulizi wa: Hotuba, ki-itimamu, penyezi, tautolojia, motifu ya safari, nyimbo, kirejeshi, elekezi, muhtasari, udondoshi, onyesho, uendelezaji, mtuo na idadimarudio katika uwasilishaji wa matukio. Wahusika katika riwaya wamesawiriwa kama: Mhusika mkwezwa, mhusika wa kimapinduzi na mhusika wa kisaikolojia. Utafiti huu utamsaidia msomaji kuuelewa muundo wa riwaya trilojia kwa kuzingatia kipengele cha usimulizi na ujumbe unaowasilishwa katika hadithi. Utafiti utafaidi jamii ya wasomi na waandishi wa kazi za kibunifu za Kiswahili kuelewa zaidi dhana ya usimulizi na nafasi yake katika riwaya trilojia. Utafiti utaonyesha jinsi nyingine ya kuichanganua riwaya kwa kutumia nadharia ya naratolojia mbali na mbinu zingine kama zile za kimtindo, kimaudhui na za lugha. Juu ya hayo, matokeo ya utafiti yataongezea marejeleo katika uwanja wa uchambuzi wa fasihi ya Kiswahili na kutumika na watafiti wa kazi za kibunifu. Utafiti ulipendekeza tafiti zaidi zifanywe ili kuchunguza mbinu za usimulizi katika tungo za fasihi andishi. Hali kadhalika riwaya hii inaweza kutafitiwa kwa kutumia nadharia zingine tofauti na naratolojia.

ABSTRACT

This research discusses narration in *Siri Sirini* trilogy authored by Rocha Chimera (2013, 2014). *Siri Sirini* trilogy is written in three series: *Siri Sirini 1, Mshairi na Mfungwa* (2013), *Siri Sirini 2, Mpiga Mbizi Kilindini* (2014) and *Siri Sirini 3, Mtihani wa Mwanamke* (2014). The three novels have the same themes, characters, setting and style. The objectives of the study focuses on expounding various narrative devices used in narrating *Siri Sirini* trilogy and the way characters are depicted in the narration of this novel. This study was guided by the theory of narratology whose proponent is Plato and developed by Propp (1968), Claude (1970), Barthes (1975), Todorov (1977), Bal (1999) and Fludernik (2009). The theory of narratology deals with: The story, sequence of events in time, identifies ways and means of narrating a story and the aspect of characterization. The tenets of the theory of narratology used in this study are: To recognize various narrative devices used in narration, to realize the sequence of events in time considering the order of the story, duration and repetition in narration and the aspect of characterization in narration. This study was carried out in the library where books, research materials, thesis and literature on the theory, narration and trilogy were read. This research used purposive sampling procedure where *Siri Sirini* trilogy was selected. Data was obtained through reading of *Siri Sirini* trilogy. Sentences reflecting the use of various narrative techniques, speech and thoughts of characters were extracted from the text. Data was analysed and results presented in form of an informed discourse guided by the objectives of the study. The research findings manifested various narrative techniques such as: Speech, epistles, songs, journey motif, tautology, flashbacks, flashforwards, summary, ellipsis, scene, extension, pause and frequency in the presentation of events. The characters were presented as a hero, revolutionary and psychological. This study will benefit the scholars to understand the structure of this trilogy regarding the aspect of narration and the issues invoked. This research will assist authors of creative works in Kiswahili to comprehend the aspect of narration and its place in the narration of the Kiswahili novel that is a trilogy. This study shows another way of analysing a Kiswahili novel using the theory of narratology besides other literary devices such as style, themes and language. The findings of this study will be an additional reference in the study of Kiswahili literature. This study recommends further research in the analysis of narrative techniques in other written literature. Also this trilogy can be investigated by using other theories besides narratology.

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI.....	ii
HATILINZI.....	iii
TABARUKU.....	iv
SHUKRANI.....	v
IKISIRI.....	vi
ABSTRACT.....	vii
YALIYOMO.....	viii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI 1

1.1 Usuli wa Utafiti.....	1
1.2 Suala la Utafiti.....	2
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	3
1.4 Maswali ya Utafiti.....	3
1.5 Umuhimu wa Utafiti.....	3
1.6 Maelezo ya Istilahi.....	4

SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI.....5

2.1 Usimulizi katika Fasihi.....	5
2.2 Riwaya ya Kiswahili.....	15
2.3 Dhana ya Riwaya Trilojia.....	21
2.4 Riwaya Trilojia ya <i>Siri Sirini</i>	23
2.5 Msingi wa Nadharia.....	24
2.6 Hitimisho.....	26

SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.....27

3.1 Mpangilio wa Utafiti.....	27
3.2 Uteuzi wa Sampuli.....	27
3.3 Ukusanyaji wa Data.....	27
3.4 Maadili ya Utafiti.....	28
3.5 Uchanganuzi wa Data.....	28
3.6 Uwasilishaji wa Data.....	28
3.7 Hitimisho.....	29

SURA YA NNE: MBINU ZA USIMULIZI KATIKA RIWAYA TRILOJIA YA SIRI SIRINI.....	30
4.1 Utangulizi.....	30
4.2 Usimulizi wa hotuba.....	30
4.3 Usimulizi wa ki-itimamu.....	36
4.4 Usimulizi penyezi.....	39
4.5 Usimulizi tautolojia.....	42
4.6 Usimulizi wa motifu ya safari.....	46
4.7 Usimulizi wa nyimbo.....	53
4.8 Usimulizi wa kirejeshi.....	59
4.9 Usimulizi elekezi.....	64
4.10 Usimulizi wa muhtasari.....	67
4.11 Usimulizi udondoshi.....	69
4.12 Usimulizi onyesho.....	72
4.13 Usimulizi uendelezaji.....	76
4.14 Usimulizi mtuo.....	78
4.15 Usimulizi wa idadimarudio.....	81
4.15.1 Usimulizi mosi.....	81
4.15.2 Usimulizi rudufu.....	85
4.15.3 Usimulizi banifu.....	90
4.16 Hitimisho.....	92
SURA YA TANO: WAHUSIKA KATIKA RIWAYA TRILOJIA YA SIRI SIRINI.....	94
5.1 Dhana ya uhusika.....	94
5.2 Uainishaji wa wahusika.....	95
5.2.1 Mhusika mkwezwa.....	95
5.2.1.1 Fumo Liyongo.....	96
5.2.2 Mhusika wa kimapinduzi.....	102
5.2.2.1 Fumo Liyongo.....	102
5.2.2.2 Mwanakupona.....	104
5.2.2.3 Dhaidho Sengo Biri.....	105
5.2.2.4 Mfawidhi Kijumwa Mfaume.....	106
5.2.2.5 Menzwa Biryu.....	107

5.2.2.6 Kibwana Mwengo Bashee	108
5.2.2.7 Mwanalemba.....	109
5.2.2.8 Mwanaziza	110
5.2.2.9 Malkia wa Sheba.....	110
5.2.2.10 Abanoye	111
5.2.2.11 Suleiman Mringwari	113
5.2.2.12 Mfalme Filipo wa Pili	114
5.2.2.13 Khalikzanda	115
5.2.2.14 Halfani Muyaka	116
5.2.3 Mhusika wa kisaikolojia.....	116
5.2.3.1 Abanoye	116
5.2.3.2 Osman Ali Kidhabi	118
5.3 Hitimisho.....	120
SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	121
6.1 Muhtasari.....	121
6.2 Hitimisho.....	121
6.3 Mapendekezo	122
MAREJELEO	123
VIAMBATISHO	129
Kiambatisho 1: Kibali Cha utafiti Kutoka Chuo Kikuu cha Chuka.....	129
Kiambatisho 2: Kibali Cha Utafiti	130

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Utafiti

Usimulizi ni kipengele cha fani (Njogu na Chimera, 1999). Njogu na Chimera wanaeleza kuwa usimulizi ni sauti ya uwasilishaji wa hadithi. Ili hadithi iweze kumfikia msomaji au msikilizaji ni lazima kuwe na usimuliaji wa hadithi yenyewe (Wamitila, 2008). Usimulizi ni suala la kimsingi katika uwasilishaji wa kazi za nathari na hatukosi kuisikia sauti ya msimulizi tunapoisoma hadithi (Mohochi, 2000). Usimulizi unahusisha maneno, mazungumzo, mawazo, vitushi, matukio na tamaduni zilizo na hadithi ya kusimulia (Bal, 1999). Kazi yoyote ya fasihi huwa mna hadithi ambayo inasimuliwa na msimulizi anayesimulia hadithi katika nafsi ya kwanza, nafsi ya pili au nafsi ya tatu (Wamitila, 2002). Msimulizi wa nafsi ya kwanza ni yule anayejitambulisha waziwazi na anaweza kushiriki katika matukio katika kazi fulani au anayeyashuhudia. Anatambulishwa kwa kiwakilishi 'mimi'. Msimulizi wa nafsi ya pili hajazoeleka na hutambulishwa kwa kiwakilishi 'wewe'. Msimulizi wa nafsi ya tatu amezoeleka sana katika uandishi wa fasihi ya Kiswahili na hutambulishwa kwa mofimu'a'. Ni usimulizi ambapo mwandishi huwa na uhuru mkubwa na ndiye mtawala wa hadithi (Njogu na Chimera, 1999).

Usimulizi unaweza kuwa wa moja kwa moja na unaofululiza kwa njia iliyo rahisi au ukawa na mikatizo ya hapa na pale (Wamitila, 2002). Usimulizi una nafasi kubwa katika kuwaelekeza wasomaji kwenye wasifu wa wahusika (Bal, 1999). Kazi za nathari huwa ndefu zenye wahusika na mtiririko wa visa vinavyoeleza ukweli fulani kuhusu maisha ya binadamu (Wamitila, 2003). Ni kazi zinazoweza kusimuliwa kwa kutumia njia mbalimbali za usimulizi (Msokile, 1993). Msimulizi hufanikisha usimulizi wake kwa kutumia ufundi wa kisanaa (Madumulla, 2009). Mojawapo wa sanaa ni mtindo wa trilojia. Trilojia ni tamthilia, riwaya au opera yenye sehemu tatu mfululizo zenye maudhui moja ambamo kila sehemu hujitegemea (TUKI, 2006). Harmon na Hugh (2000) wanaeleza kuwa trilojia ni kazi ya sanaa yenye sehemu tatu zinazohusiana na kwamba huandikwa kwa misingi ya wazo pana. Trilojia ni kazi za kibunifu kama vile filamu, michezo ya Kompyuta na fasihi zinazofanana kiwahusika, kimaudhui, kimandhari na kimtindo.

Trilojia nyingi zimeandikwa katika lugha ya Kiingereza kama vile *The African Trilogy* iliyoandikwa na Chinua Achebe. Ni trilojia inayojumuisha: *Things Fall Apart, No Longer at Ease* na *The Arrow of God* (Rice, 2018). Trilojia nyingine ni *My Life in Crime* iliyoandikwa na John Kiriamiti. Inajumuisha: *My Life as a Criminal, My Life in Crime* na *My Life in Prison* (Mwangi, 2013). Trilojia zingine ni kama vile *The Beijing Trilogy* (Zhang, 2016) na *The New York Trilogy* (Eslamich, 2016).

Riwaya ya kwanza ya Kiswahili kuandikwa katika msururu wa riwaya tatu ni *Siri Sirini* iliyoandikwa na Rocha Chimera (2013, 2014). Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* inahusisha: *Siri Sirini 1, Mshairi na Mfungwa* (2013), *Siri Sirini 2, Mpiga Mbizi Kilindini* (2014) na *Siri Sirini 3, Mtihani wa Mwanamke* (2014). Riwaya hizi tatu zinafanana kimaudhui, kimandhari, kiwahasika na kimtindo. Rocha Chimera ni msomi anayejihusisha na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili na fasihi na mbinu za kufundisha somo hili. Amefanya utafiti wa suala la nadharia na sura ya tamthilia ya Kiswahili. Amechapisha vitabu kadhaa vikiwemo: *Nyongo Mkalia Ini* (1995), *Mnara Wawaka Moto* (1998), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu* (1999) kilichopata ushindi wa Tuzo la Noma 2000 (Kimaro, 2016), *Kiswahili Past, Present and Future Horizons* (1998) kilichopata ushindi mwaka wa 2002 (Otieno, 2017). Ni mmoja wa washauri wa mradi wa *Kamusi ya Karne ya 21* (Longhorn, 2013).

Utafiti huu ulizingatia kipengele cha usimulizi ambacho ni cha fani. Utafiti huu ulilenga kubainisha mbinu mbalimbali za usimulizi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini* na jinsi wahusika walivyosawiriwa katika usimulizi wa riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

1.2 Suala la Utafiti

Trilojia ni msururu wa kazi tatu za filamu, michezo ya kuigiza au kifasihi uliotokana na mila za Ugiriki. Katika fasihi andishi hasa riwaya, mfumo wa trilojia umetumika. Hata hivyo riwaya nyingi zilizoandikwa kwa mtindo wa trilojia zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza mfano wa *The New York Trilogy, The Beijing Trilogy, The African Trilogy* and *My Life in Crime Trilogy*. Riwaya ya kwanza ya Kiswahili kuandikwa katika mtindo wa trilojia ni *Siri Sirini* iliyoandikwa na Rocha Chimera. Riwaya hizi ni: *Siri Sirini 1, Mshairi na Mfungwa, Siri Sirini 2, Mpiga Mbizi Kilindini* na *Siri Sirini 3, Mtihani wa Mwanamke*. Kwa kuwa riwaya hii ina upekee wa kuwa riwaya ya kwanza

ya Kiswahili kuandikwa katika msururu wa riwaya tatu, utafiti huu ulilenga kuchunguza mbinu mbalimbali za kiusimulizi ambazo mwandishi alitumia kuiandika ili kuwasilisha ujumbe.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa:

- i. Kubainisha mbinu mbalimbali za usimulizi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.
- ii. Kuchunguza jinsi wahusika walivyosawiriwa katika usimulizi wa riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

1.4 Maswali ya Utafiti

Maswali yafuatayo yalitumiwa kuongoza utafiti huu:

- i. Je, ni mbinu zipi za usimulizi zilizotumika katika kusimulia riwaya trilojia ya *Siri Sirini*?
- ii. Je, usimulizi wa riwaya trilojia ya *Siri Sirini* uliwasawiri vipi wahusika?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utamsaidia msomaji kuelewa muundo wa riwaya trilojia kwa kuzingatia kipengele cha usimulizi na ujumbe unaowasilishwa katika hadithi. Utafiti utafaidi jamii ya wasomi na waandishi wa kazi za kibunifu kuelewa zaidi dhana ya usimulizi na nafasi yake katika utunzi. Utafiti utaonyesha jinsi nyingine ya kuichanganua riwaya kwa kutumia nadharia ya naratolojia mbali na mbinu zingine zinazoelezwa kama zile za kimtindo, kimaudhui na za lugha. Zaidi ya hayo, matokeo ya utafiti yataongezea marejeleo katika uwanja wa uchambuzi wa fasihi ya Kiswahili na kutumika na watafiti wa kazi za kibunifu.

1.6 Maelezo ya Istilahi

Utafiti huu ulitumia istilahi zifuatazo ambazo zilifafanuliwa kwa kurejelea matumizi yake katika utafiti.

- Matini:** Ni makala ya riwaya trilojia ya *Siri Sirini* yaliyowasilishwa kwa njia ya maandishi.
- Mtuo:** Ni usimulizi wa mandhari katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.
- Muhtasari:** Ni ufupishaji wa muda fulani wa hadithi kwa kauli chache ili kuharakisha hadithi katika matini ya *Siri Sirini*.
- Naratolojia:** Ni nadharia inayohusika na sifa na muundo wa hadithi. Ni nadharia iliyotumika kuchunguza usimulizi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.
- Onyesho:** Ni usimulizi wa mazungumzo katika matini ya *Siri Sirini*.
- Trilojia:** Ni msururu wa riwaya tatu za *Siri Sirini: Siri Sirini 1, 2 na 3*.
- Udondoshi:** Hurejelea pale ambapo maelezo fulani katika trilojia ya *Siri Sirini* yameachwa.
- Uendelezaji:** Ni usimulizi ambapo msimulizi huangaza ndoto au mawazo ya mhusika katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.
- Usimulizi banifu:** Ni umara ambapo tukio linaweza mara nyingi halafu mara zote zile zinabanwa na kusimuliwa mara moja katika hadithi ya *Siri Sirini*.
- Usimulizi mosi:** Ni aina ya idadimarudio ambapo tukio linaweza kutokea mara moja na kusimulia mara moja katika hadithi ya *Siri Sirini*.
- Usimulizi rudufu:** Ni umara ambapo tukio linafanyika mara moja na kusimuliwa mara nyingi katika simulizi ya *Siri Sirini*.

SURA YA PILI

MWAUO WA MAANDISHI

2.1 Usimulizi katika Fasihi

Fisher (1984) alichunguza usimulizi kama njia ya mazungumzo. Alitambua kuwa maisha ya binadamu ni hadithi inayosimulia maisha yao ya kila siku. Mfapati alitambua kwamba msimulizi husimulia hadithi kwa hadhira hai zinazolenga masuala ya jamii. Ni hadithi zinazozingatia mpangilio fulani na huwa na ujumbe fulani. Mfapati alibaini kuwa mbinu ya usimulizi ni muhimu katika kupitisha ujumbe. Matokeo ya uchunguzi huu yalikuwa muhimu kwa vile yalikuwa kielelezo cha yale yaliyotafitiwa katika utafiti huu. Ijapokuwa utafiti wa Fisher ulilenga mazungumzo katika usimulizi, utafiti huu ulipiga hatua na kutafiti mbinu mbalimbali za usimulizi zilizotumika kuisimulia matini teule.

Katika maelezo yake kuhusu simulizi, Msokile (1993) anafafanua simulizi kama maelezo juu ya tukio fulani yanayosimuliwa na msimulizi. Mfapati anaeleza kuwa simulizi ni mazungumzo. Mfapati amebainisha msimulizi penyezi ambaye hutoa mawazo kuhusu vituko na matendo katika hadithi. Mfapati anafafanua kuwa hadithi inaweza kuwa na mpangilio wa ki-anakroni, muundo anaoita wa kisengerenyuma na kisengerembele. Mfapati anaeleza kuwa wahusika katika riwaya ndio hujenga hadithi na kuwaainisha kama wahusika wakuu na wahusika wadogo. Kwa hivyo maelezo yake yalifaa riwaya trilogia kutafitiwa katika kipengele cha wahusika na mbinu za usimulizi.

Akifafanua vijengo vya riwaya, Mohamed (1995) anaeleza kuwa hadithi husimuliwa kupitia sauti ya msimulizi na kwamba msimulizi hutumia mbinu mbalimbali za kukidhi mahitaji yake. Mohamed anafafanua mbinu hizi kama usimulizi wa nafsi ya kwanza ambapo msimulizi anaweza kuwa mshiriki wa matukio au asiwe mshiriki. Ni usimulizi unaojenga uhusiano wa karibu kati ya hadithi na msomaji. Katika usimulizi wa nafsi ya tatu, msimulizi wa hadithi huelezea matukio au mambo yanayomhusu mtu mwingine. Mfapati amewatambulisha wahusika mvingo, bapa na kinyago. Maandishi haya yalisaidia utafiti huu katika kuchunguza usawiri wa wahusika na mbinu za usimulizi katika matini teule.

Maandishi ya Abrams (1999) kuhusu hadithi yanaeleza kuwa hadithi ni kisa kinachosimuliwa kwa njia ya kinathari au kishairi kuhusu matukio, wahusika na wanachokisema na kukifanya. Abrams anafafanua kuwa kazi ya kifasihi kama vile riwaya, hadithi fupi na utenzi husimuliwa na msimulizi. Mtafiti ameeleza kuwa wahusika ni viumbe muhimu katika kazi ya kibunifu wanaotumika na mtunzi kuadilisha. Mtafiti amefafanua kuwa wahusika wanaweza kutambulika kutokana na matendo, mawazo, msisimko na jinsi wanavyoshawishika. Maelezo haya yalikuwa na manufaa kwa kuwa yalitoa mwanga zaidi kuhusu hadithi na wahusika kwani ni baadhi ya sehemu zilizotafitiwa katika riwaya teule.

Katika utafiti wao, Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kuwa usimulizi ni sauti ya uwasilishaji wa hadithi. Wanafafanua aina kadha za usimulizi. Aina moja ya kusimulia ni pale mwandishi mwenyewe anatumia nafsi ya tatu na huwa na uhuru mkubwa. Ndiye mtawala wa hadithini. Aidha, wanasema kuwa huu ndio mtindo wa usimulizi unaotumika sana katika fasihi ya Kiswahili. Aina nyingine ya usimulizi ni pale ambapo mmoja wa wahusika anasimulia kuhusu matendo yake na ya wahusika wenzake. Huu ni usimulizi wa mazungumzo. Maelezo haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu kwa kuwa yalitumika kutambua aina za usimulizi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

Katika maelezo yake, Bal (1999) anafafanua kwamba msimulizi anaweza kutumia mbinu zozote za usimulizi zinazotumika kusimulia hadithi. Mtafiti anamrejelea msimulizi wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Mtafiti anaeleza kuwa urefu wa hadithi husababisha mpango wa ki-anakroni ambapo msimulizi hukiuka kanuni za mpangilio wa matukio kwa kurejelea matukio ya awali katika usimulizi au hutanguliza matukio yatakayotendeka katika hadithi. Mtafiti anafafanua kuwa matukio yanaweza kurudiwa katika usimulizi. Maandishi haya yalifanikisha utafiti huu kwa vile yalitoa mwanga zaidi kuhusu usimulizi.

Akirejelea kipengele cha usimulizi Bertocini (2000) alichunguza hadithi fupi ya M. S Mohamed, 'Uhuru wa Siku Moja' katika diwani *Kicheko Cha Ushindi*. Mtafiti alihakiki hadithi hii kwa misingi ya muundo, ploti na lugha. Mtafiti alitambua kuwa hadithi hii ni ya kisasa ambayo inazingatia mfuatano wa wakati katika usimulizi. Mtafiti ametambua kuwa msimulizi amekiuka utaratibu wa kiwakati kwa kutumia mbinu

rejeshi. Mtafiti ametambua kuwa muda unaodhihirika katika usimulizi wa hadithi hii ni muhtasari ambapo muda wa usomaji ni mfupi kuliko ule wa hadithi. Mtafiti ametambua kuwa hadithi imesimuliwa katika nafsi ya tatu ambapo msimulizi hashughuliki katika mambo anayosimulia. Pia, hadithi imesimuliwa kwa mtazamo wa mhusika Mambo. Mtafiti amebaini kwamba usimulizi uliotumika ni wa maelezo ambapo hisia tofauti hujitokeza. Usimulizi wa nafsi ya kwanza umejitokeza hasa pale msimulizi ametumia wakati halisi. Msimulizi ametumia tamathali za usemi kama vile jazanda, taswira na kinaya. Mtafiti ametambua mhusika mmoja, Mambo. Tofauti na utafiti wa Bertoncini uliochangana matini tofauti, kazi yake ilifaa utafiti huu kuchunguza mbinu za usimulizi na usawiri wa wahusika.

Mawazo ya Mohochi (2000) kuhusu usimulizi ni kwamba usimulizi ni suala la kimsingi sana katika uwasilishaji wa kazi mbalimbali za kifasihi hasa za nathari. Mtafiti ametambulisha usimulizi wa nafsi ya kwanza ambapo msimulizi hutoa maelezo marefu kuhusu wahusika na matukio ya kihistoria. Ni usimulizi unaoifanya hadithi kuwa hai kwa kuifanya ifanane na maisha ya kila siku. Mtafiti anaeleza kuwa wahusika wanaweza kuzungumza au kutumia barua katika usimulizi. Usimulizi mwingine aliyoshughulikia ni wa nafsi ya tatu ambapo msimulizi anapewa nafasi ya kuwa mhusika mkuu au mhusika mwingine yeyote hadithini. Mtafiti ameeleza mfuatano wa matukio wa ki-anakroni ambapo mbinu rejeshi hutumika kwa lengo la kubainisha misukumo ya wahusika. Mtafiti amerejelea takriri kama mbinu mojawapo ya usimulizi. Mtafiti anafafanua kuwa takriri huwa na manufaa makubwa katika usimulizi kwa kuisitiza wazo au kujenga uziada katika matini. Ufafanuzi wa Mohochi ulichangia utafiti huu kuchunguza kipengele cha usimulizi na usawiri wa wahusika.

Kazi ya Traore (2001) ilichunguza uhusiano wa fasihi simulizi na fasihi andishi katika usimulizi. Alitumia kazi za nathari: *Wasifu wa Siti Binti Saad, Utengano na Siku Njema*. Mtafiti ameonyesha jinsi mbinu ya sanaa ya taarab imetumika kumchora mwanamke na kujadili maudhui mbalimbali. Utafiti wa Traore ulisaidia utafiti huu kuchunguza mbinu za usimulizi za fasihi simulizi zilizotumika kusimulia riwaya trilojia ya *Siri Sirini*. Tofauti na utafiti huu mtafiti ameonyesha uhusiano wa tanzu mbili kuu za fasihi na jinsi zinavyochangiana. Utafiti wa Traore ulisaidia utafiti huu kuchunguza mbinu za usimulizi za fasihi simulizi zilizotumika kusimulia hadithi hii.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa kazi za kifasihi huwa mna kisa kinachosimuliwa na msimulizi anayesimuliwa hadithi hiyo kwa njia maalum. Mtafiti ametambua njia hizo kuwa usimulizi wa nafsi ya kwanza na usimulizi wa nafsi ya tatu. Mtafiti anaeleza kuwa hadithi inaweza kusimuliwa kwa matumizi ya takriri na kuwa usimulizi hutazamwa sambamba na kipengele cha wakati. Mtafiti anafafanua kuwa mara nyingi matukio yanayopatikana katika matini huwa hayafuatani kiwakati. Hali hii inasababishwa na mbinu mbalimbali za kisimulizi kama kuyataka kuyarejelea matukio yaliyopita au kuyatanguliza mambo ya mbele katika hadithi. Mtafiti ameeleza kuwa matukio yanaweza kusimuliwa baada ya kutokea, kabla ya kutokea au wakati huo huo wa kutokea. Wamitila amerejelea suala la wakati- hadithi na wakati-matini na kueleza kuwa usimulizi una nafasi kubwa katika kuwaelekeza wasomaji kwenye wasifu wa wahusika. Mtafiti anafafanua kuwa wahusika husawiriwa kwa: Wasifu wao, tabia zao, lugha zao, vionjo na itikadi zao. Maelezo ya mtafiti huyu yalikuwa ya manufaa katika uchunguzi huu katika kuchunguza vipengele vya wahusika na usimulizi.

Wamitila (2003) ameeleza usimulizi penyezi, usimulizi wa ki-itimamu, usimulizi kirejeshi, usimulizi tangulizi na usimulizi tautolojia. Aidha, Wamitila (2008) amefafanua kuwa wahusika ndio jira ya matukio na matendo katika hadithi na kwamba wanaweza kuangaliwa kutegemea tajriba zao, mabadiliko yao na uradidi wa matukio. Utafiti huu umenufaika na maelezo haya katika kuchunguza mbinu za usimulizi na usawiri wa wahusika katika riwaya teule.

Kipengele cha usimulizi kilitafitiwa na Ngure (2003). Mtafiti anaeleza fasihi simulizi katika jamii ya kisasa. Ngure anatoa mfano wa usimulizi wa hadithi iliyosimuliwa katika redio ya BBC, Uingereza. Usimulizi wa hadithi hiyo redioni unaonyesha njia za kisasa zinazotumiwa kuwasilisha fasihi simulizi. Ni hadithi inayoonyesha maudhui ya uwongo. Japo kazi ya Ngure imelenga usimulizi wa hadithi katika redio, utafiti huo ulinufaisha kazi hii kuhakiki usimulizi wa hadithi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

Akishughulikia usimulizi wa filamu, Wichlacz (2006) aliandika kwamba usimulizi katika matini, maigizo, nyimbo au runinga humtegemea msimulizi katika kuwasilisha ujumbe. Mtafiti anaeleza kuwa usimulizi wa filamu huazima masimulizi kutoka kwa matini hasa hadithi fupi na tamthilia. Mtafiti anaeleza kuwa usimulizi wa filamu

unaweza kudhihirisha mawazo ya wahusika. Mtafiti anafafanua kuwa usimulizi wa filamu huwa katika nafsi ya kwanza au nafsi ya tatu na kwamba msimulizi ndiye sauti ya hadithi inayosimuliwa. Tofauti na maandishi haya yanayolenga usimulizi wa filamu, yalisaidia riwaya teule kutafitiwa usimulizi na usawiri wa wahusika.

Maandishi ya Fludernik (2009) yanaeleza kuwa simulizi ni hadithi inayosimuliwa na msimulizi. Mtafiti amefafanua kuwa msimulizi wa nafsi ya kwanza anaweza kuwa mmoja wa wahusika anayesimulia hadithi huku akifafanua matukio. Usimulizi huu hutokea sana katika mazungumzo hasa hatika riwaya. Mtafiti anaeleza kuwa msimulizi wa nafsi ya tatu husimulia mambo yanayomhusu. Mtafiti anafafanua kuwa usimulizi sharti uhusishe msuko, matendo na umuhimu wa wakati katika usimulizi huku akitofautisha kati ya wakati-matini na wakati-hadithi. Mtafiti ameeleza kuwa hadithi nyingi husimuliwa katika mfuatano wa kiwakati ingawa zipo hadithi ambazo hazifuati mpangilio huu. Maoni yake kuhusu wahusika ni kwamba wanatambulishwa kwa kupewa majina. Mtafiti amefafanua majukumu ya msimulizi kama vile kueleza sababu za matukio fulani kutokea, kuonyesha msukumo wa wahusika katika kuendeleza hadithi, kuadilisha jamii na kuwasilisha maoni yake katika usimulizi. Utafiti huu umenufaika na maandishi haya katika kuchunguza usimulizi na usawiri wa wahusika.

Utafiti wa Elshout (2011) ulichunguza ufaafu wa kuingiza balagha katika usimulizi. Mtafiti alitumia hadithi ya Raabe, 'Celtic bones' na kutambua ya kwamba msimulizi alitumia nafsi ya kwanza, tanakali za sauti, kinaya, tasfida na tasbihi kusimulia hadithi hii. Mtafiti alibaini kuwa wahusika waliotumika katika hadithi walionyesha ushindani katika usimulizi. Japo utafiti huo umelenga tamathali za usemi, ulifaa utafiti huu kuchunguza usawiri wa wahusika na kipengele cha usimulizi katika riwaya trilojia.

Akichunguza diskozi na dhana ya usimulizi kama njia mpya ya kuonyesha taswira katika hadithi ya Hans Christian Anderson, Bom (2011) alitambua kuwa watu hupata fasiri mbalimbali za maneno yaliyotumika katika hadithi. Mtafiti alibaini kwamba hadithi zinazosimuliwa hulenga masuala mbalimbali ya jamii husika na kuwa lugha iliyotumika katika usimulizi wa hadithi husababisha hisia fulani kwa hadhira. Ingawa matini iliyochanganuliwa ni tofauti, utafiti wake ulikuwa na manufaa katika kuchunguza kipengele cha usimulizi katika riwaya teule.

Akitafiti nafasi ya mwanamke katika hadithi za jamii ya Indo-Persian, Shahbaz (2011) alitambua kuwa hadithi hizi zina mpangilio maalum na huwa na hadithi ndani ya hadithi. Mtafiti alitambua kwamba hadithi zote zilishughulikia maudhui ya ujanja wa wanawake. Maudhui ya mapenzi yameangaziwa huku mwanamke akitumiwa kama chombo cha kukidhi mahitaji ya mwanamume. Mtafiti alibaini kuwa hadithi hizi huwa na mafunzo kwa jamii inayochukua mwanamke kama kiumbe duni. Mwanamke ametambuliwa kuwa mjanja, mzinzi, mwasi, mjinga, mbea na wengine wamechorwa kama wanyamavu, wapole, watiifu, wacha Mungu na walioheshimika. Japo utafiti wa Shahbaz unafanana na huu kwa kuzingatia usimulizi, unatofautiana kwa kuwa umechunguza hadithi fupi na ulifaa utafiti huu katika kutafiti mpangilio wa hadithi na usawiri wa wahusika.

Akishughulikia umuhimu wa teknohama, Madsen (2011) alitafiti usimulizi wa hadithi kuhusu familia. Mtafiti alitafiti suala la uzazi na jinsi wazazi walivyofanikiwa kupata watoto kama ilivyosimuliwa. Familia hizi zilikuwa na matatizo ya kupata watoto. Walitumia wazazi mbadala ili kuweza kupata watoto. Mtafiti alitambua kuwa wazazi hawa waliwasiliana kwa kutumia Kompyuta, kwamba walitumia ishara na majina ya lakabu katika mawasiliano. Mtafiti alibaini kuwa teknohama imejenga jamii mpya yenye upekee iliyokiuka mipaka ya mila na tamaduni. Mtafiti alitambua kuwa kuna changamoto katika uhusiano baina ya nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea. Tofauti na utafiti wa Madsen uliotumia binadamu halisi katika usimulizi, utafiti huo ulifaa utafiti huu kuchunguza usimulizi katika kazi za kibunifu ambayo ni riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

Uchunguzi kuhusu usimulizi ulifanywa na Engberg (2011). Mtafiti alichunguza hadithi zinazohusu uhalisia wa hadithi ya wakristo wa dhehebu la zion. Mtafiti alitaka kufahamu mahusiano na imani yao kwa Waisraeli. Mtafiti alitambua kuwa historia ya watu hawa ni hadithi inayotungwa makusudi ili kusimuliwa mbele ya hadhira. Mtafiti alibaini kwamba mawazo ya wakristo hawa yana sehemu zote za hadithi: Kuwepo kwa vituko kutegemea mandhari, wahusika na kwamba matukio yanaletwa pamoja ili kuwasilisha ujumbe fulani. Mtafiti alitambua kwamba masuala ya jinsia yanaleweka kwa kuchanganua ploti, tamathali za usemi na wahusika katika mazingira fulani. Japo utafiti wake umelenga hadithi ya wakristo, unafanana na huu kwa sababu unahusiana

na usimulizi wa hadithi katika riwaya teule na ulifaa utafiti huu kujadili jinsi wahusika walivyosawiriwa na mbinu za usimulizi.

Akitafiti kuhusu mpangilio wa ngoma inayochezwa kuigiza hadithi zilizo na mada ya mapenzi, Bernkopf (2011) alitambua kuwa ngoma hizi huwa na mwanzo, kati na mwisho. Mtafiti alitambua kuwa si lazima hadithi zote zifuate mpangilio huu hasa kwa kuzingatia muda na wakati. Mtafiti alibaini kuwepo kwa matendo katika uigizaji wa ngoma mahali popote katika hadithi na umuhimu wa migogoro ya mapenzi ya wahusika katika hadithi. Mtafiti alitambua kuwa wahusika hubadilishana majukumu katika hadithi na mhusika mmoja anaweza kupewa majukumu mbalimbali. Tofauti na utafiti huo uliohusu ngoma, ulinufaisha utafiti huu katika kuwasawiri wahusika na kipengele cha usimulizi katika riwaya trilojia.

Usimulizi kama njia ya kujifunza hadithi za watoto ulishughulikiwa na Odegaard (2011). Mtafiti alitambua kuwa hadithi za watoto husimulia uhalisia wa maisha na mara nyingine huwa hadithi za kubuni. Mtafiti alibaini kwamba maana ya hadithi hutegemea fasiri inayopatikana kutokana na shughuli wanazoshiriki watoto. Wahusika wanaotumika huwa wa miraba minne na hutumika kimapumbo. Mtafiti alitambua kuwa maudhui yanayoshughulikiwa katika hadithi hizi ni elimu, uoga na hasira. Ijapokuwa utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa umechunguza hadithi za watoto, ulinufaisha utafiti huu kuchunguza usimulizi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini* na jinsi wahusika walivyosawiriwa.

Drach (2011) alichunguza umuhimu wa mbinu ya kuleta pamoja matini na sehemu za matini zilizo tofauti katika mtindo, muundo na maudhui katika usimulizi wa sinema. Mtafiti alitumia filamu ya Berlin Alexanderplatz iliyotengenezwa kutoka kwa riwaya ya *Berlin Alexanderplatz*. Mtafiti alitambua kuwa sauti ya msimulizi ni muhimu katika uwasilishaji wa filamu na kwamba usimulizi huu unaonekana kuwa na mpangilio maalum unaohusisha muda na wakati. Mtafiti alibaini kwamba ploti katika filamu ni rahisi na kwamba mwelekezi humpa hadhi kuu mhusika mkuu na kwamba visehemu mbalimbali vilivyotumika katika riwaya vinatajwa katika filamu. Ingawa utafiti wa Drach ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa umelenga sinema, ulinufaisha utafiti huu kuchunguza mbinu za usimulizi na usawiri wa wahusika.

Maoni kuhusu usimulizi yamejadiliwa na Grund na Westney (2011). Watafiti hawa walichunguza ushirikiano uliopo katika usimulizi wa hadithi na usimulizi wa muziki katika studio unaofanyika mbele ya hadhira. Watafiti walitambua kuwa waigizaji wa hadithi na waigizaji wa muziki wanafanana katika kuwavutia watazamaji. Watafiti walibainisha tofauti katika kusimulia hadithi na katika kusimulia muziki. Katika usimulizi wa muziki, mpangilio maalumu unalazimishwa ilhali katika usimulizi wa hadithi, msimulizi anatumia mbinu za usimulizi ili kuwaridhisha watazamaji na huwa na maudhui fulani. Japo utafiti wao umelenga usimulizi wa muziki na usimulizi wa hadithi katika studio, ulikuwa na manufaa katika utafiti huu kwa sababu usimulizi ni baadhi ya vipengele vilivyotafitiwa.

Usimulizi katika sanaa ya michezo ulitafitiwa na Ayramo (2011). Mtafiti alitafiti usimulizi katika sanaa ya michezo akitumia michezo ya Kompyuta. Mtafiti alitambua kwamba michezo ya Kompyuta huwa na mwanzo, kati na mwisho. Mtafiti alibaini kwamba wahusika katika michezo hushiriki mazungumzo yanayohusiana na uhalisia wa matukio katika jamii husika. Japo utafiti wa Ayramo ni tofauti na huu kwa sababu ulitumia michezo ya Kompyuta, ulinufaisha utafiti huu kuchunguza mbinu za usimulizi na jinsi ya kuwasawiri wahusika katika riwaya teule.

Akishughulikia usimulizi kama njia ya mawasiliano katika mashirika, Norlyk (2011) alitambua kuwa mashirika huwa na mpangilio fulani ulio na maadili ya shirika husika. Mtafiti alibaini kuwepo kwa mhusika mkuu na wahusika wasaidizi na kwamba katika matangazo, mwandishi huandika wazo linalosimuliwa na msimulizi. Lugha anayotumia msimulizi huwa rahisi, ya kushawishi na hutumia nafsi ya kwanza. Ingawa utafiti wa Norlyk ni tofauti na huu kwa vile umetumia mashirika, ulikuwa wa manufaa katika utafiti huu.

Uchunguzi wa Chirila (2011) ulihusisha kwelikinzani katika hadithi ya Toni Morrison, 'paradise'. Mtafiti alitambua kuwa msimulizi alitumia nafsi ya tatu na aliwahasisha wahusika wengi huku msimulizi akitumia taswira, ishara, takriri, mbinu rejeshi, jazanda na visasili vinavyowakilisha maadili ya jamii. Japo utafiti wa mtafiti huyu unafanana na huu kwa kuwa umechunguza wahusika, usimulizi wa nafsi ya tatu, takriri na mbinu

rejeshi, kuna tofauti. Yeye ametafiti hadithi fupi. Utafiti huo ulikuwa na manufaa katika utafiti huu kutafiti mbinu za usimulizi na usawiri wa wahusika.

Utafiti wa kipengele cha usimulizi ulifanywa na Burundi (2011). Mtafiti alichunguza usimulizi katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Mtafiti alibaini kuwa usimulizi ni mtindo wa uwasilishaji unaotumiwa katika kazi za kifasihi. Mtafiti alitambua kuwa kila kazi ya fasihi huwa na hadithi inayosimuliwa na msimulizi. Mtafiti alibaini kuwa katika utenzi huu msimulizi ndiye mtunzi. Mtafiti ametambua kuwa fani ya usimulizi imeonyesha upekee katika kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe katika utenzi husika. Usimulizi wa nafsi ya kwanza, nafsi ya tatu, usimulizi horomo, maizi na penyezi umetumika. Wahusika wamejitokeza katika utenzi. Tamathali za usemi zimeonekana mtunzi kutoa dhamira yake ya udhalimu. Tofauti na matini ya kazi aliyotafitia Burundi, utafiti wake ulinufaisha utafiti huu kuchunguza usimulizi na usawiri wa wahusika.

Shitemi (2011) alichunguza usimulizi katika *Utenzi wa Siri li Siraili*. Mtafiti alichunguza matumizi ya usimulizi katika utenzi. Mtafiti alitambua kuwa utenzi teule umesimuliwa. Mtafiti aliwatambulisha wasimulizi kwa kigezo cha daraja ya hadithi na kupata aina mbili za wasimulizi ambao ni: Walio ndani ya hadithi na walio nje ya hadithi. Mtafiti alitambua kuwepo kwa mtazamo wa ndani na mtazamo wa nje katika usimulizi wa utenzi huu. Mtafiti alichunguza aina za wasimulizi kwa kutumia vigezo vya viwango na uhusika. Mtafiti alitambua utegemefu wa msimulizi na hadhi ya msimulizi, suala la wakati katika usimulizi, mpangilio wa matukio, uwasilishaji mawazo na usemi katika utenzi. Japo mtafiti amechunguza mtazamo wa msimulizi, uwasilishaji mawazo na usemi na utegemefu wa msimulizi, utafiti wake ulikuwa na manufaa katika utafiti huu kwa sababu ulichunguza baadhi ya sehemu vilivyoshughulikiwa.

Uchanganuzi wa usimulizi katika utenzi ulishughulikiwa na Arege (2012). Mtafiti alichunguza usimulizi katika utenzi wa Kiswahili kwa kutumia *Utenzi wa Rasi'lg'huli*. Mtafiti alichunguza: Mbinu za usimulizi, suala la wakati, mpangilio wa matukio katika usimulizi, wahusika, maudhui, urari wa vina na mizani, mandhari na matumizi ya lugha. Tofauti na uchunguzi huu, mtafiti amechunguza utenzi. Utafiti wa Arege

ulinufaisha utafiti huu kuchunguza mbinu za usimulizi na usawiri wa wahusika katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

Akiripoti kuhusu usimulizi wa densi mtindo wa ‘Kathak’ katika jamii ya India, Qureshi (2014) ameeleza kuwa mtindo wa ‘Kathak’ umetokana na neno ‘katha’ linalomaanisha hadithi. Ni hadithi inayosimuliwa kwa kutumia ishara. Msimulizi anaashiria kwa kupunga mikono, miguu na vidole. Macho pia, yanatumika kudhihirisha hisia fulani. Yanayosimuliwa ni masuala ya dini na visa vingine vya kibunifu. Msimulizi huwashirikisha hadhira hai kwa kupiga makofi. Japo maandishi haya yamelenga densi, yanafanana na utafiti huu kwa kulenga msimulizi, mbinu za msimulizi na wanaosimulia. Ingawa maandishi haya yalitumia densi, yalikuwa na manufaa kwa utafiti huu kuchunguza mbinu za usimulizi na usawiri wa wahusika katika riwaya teule.

Akiandika kuhusu usimulizi wa hadithi, Maosa (2017) anafafanua kuwa hadithi zilisimuliwa wakati wa jioni baada ya kazi. Watoto walikusanyika kuota moto huku wakisimuliwa hadithi na babu zao. Maosa anaeleza kuwa katika ulimwengu wa sasa wazazi huwa mbioni kutafuta mali na hukosa nafasi ya kukaa na watoto kwa masimulizi. Mtafiti anafafanua kuwa simutamba huwanyima wazazi nafasi ya kuwasiliana na watoto wao. Mtafiti anaeleza kuwa msimulizi huwa na manufaa mengi kwa hadhira kama vile kukuza ubunifu wao, kuwafikirisha, kuwaadilisha, kuwamakinisha, kuwajasirisha na kuwalainisha katika mawasiliano. Mtafiti anasisitiza umuhimu wa kuwasimulia watoto hadithi wakati wa jioni kwa sababu bila usimuliaji huu, jamii hukosa mwelekeo. Tofauti na maandishi haya yaliyolenga usimulizi wa hadithi kwa hadhira hai, utafiti huu ulifaidika katika kutafiti usimulizi katika matini ya *Siri Sirini*.

Maandishi mengine kuhusu usimulizi ni ya Lillywhite (2018). Katika kazi yake, mtafiti anasimulia kuwepo kwa sanaa ya ufarishaji. Anafafanua kwamba chama cha Ufarishi nchini Kenya kilianzishwa miaka ishirini iliyopita na kwa sasa kina washirika mia moja. Anaeleza kuwa sanaa ya ufarishi iliibuka nchini Misri na inatumika katika tamaduni mbalimbali na watu wa matabaka mbalimbali. Ni sanaa ambayo haijulikana sana nchini Kenya na wanaoitumia huomba mawaidha kutoka Umarekani. Chama cha Sanaa ya Ufarishi nchini Kenya huwashawishi akina mama kutumia malighafi

yanayopatikana kwa urahisi nchini. Mapato wanayoyapata kutokana na kazi ya ufarishi huwasaidia kuzikimu familia zao na kuwasaidia wasiojiweza katika jamii. Japo maandishi haya yamelenga sanaa ya Ufarishi, yalifaa utafiti huu kuchunguza usimulizi katika riwaya teule.

Akiandika kuhusu usimulizi wa hadithi zinazohusu historia ya nchi ya Kenya iliyofanyika katika kongamano la wasimulizi, Maina (2019) anaeleza kuwa wasimulizi hawa walijaribu kuifufua historia ya nchi ya Kenya kupitia usimuliaji. Kongamano hili lilijikita katika kitabu *Living Memories* kilichoandikwa na Al Kogi. Baadhi ya yaliyomo katika kitabu hiki ni mahojiano waliyofanyiwa wakenya wakongwe. Mmoja wa wasimulizi alisimulia hadithi ya 'Wairia' iliyosimulia mashaka aliyopitia mhusika mmoja wa jinsia ya kike mikononi mwa askari wa kikoloni. Hadithi inaonyesha juhudi za wanawake katika ukombozi. Waliohudhuria kikao walibaini kuwa maovu waliotendewa wakenya wakati wa ukoloni bado yanawaandama na kuwaathiri. Wananchi wanaendelea kukandamizwa kisheria huku ufiada na dhuluma dhidi ya wanawake ukiendelezwa. Bali na usimuliaji wa hadithi, wanakikao walizua maswali mengi yaliyolenga jamii ya nchi ya Kenya miaka hamsini na tano baada ya kupata uhuru. Ingawa matini iliyochanganuliwa ni tofauti, kazi hii ilisaidia riwaya trilojia ya *Siri Sirini* kuchunguzwa vipengele vya usimulizi na wahusika.

2.2 Riwaya ya Kiswahili

Njogu (1987) alishughulikia maudhui ya mapinduzi katika *Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Mtafiti alizingatia historia ya visiwani Zanzibar inayofungamana na maudhui ya mapinduzi huku ikitufahamisha hali za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mtafiti alitambua kuwa chanzo cha mapinduzi kilitokana na uzalishaji mali wenye muundo wa kitabaka. Mtafiti amebaini kuwa maandishi wa *Riwaya za Visiwani Zanzibar* wamehamasishana na kuathiriana. Mtafiti amewasawiri wahusika katika riwaya hizi kwa kuzingatia maudhui wanayoendeleza katika riwaya husika. Tofauti na utafiti wa Njogu uliyoshughulikia sana suala la maudhui, utafiti wake ulinufaisha utafiti huu kuwasawiri wahusika katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

Akitafiti dhamira katika riwaya ,Senkoro (1988) alihakiki riwaya ya *Shida*. Mtafiti alitambua kuwa dhamira ya riwaya hii ni ujenzi wa jamii mpya ambapo mhusika Shida

aliamua kurudi kijijini na kuyaanza maisha mapya. Aidha, alibaini maudhui ya migororo, mvutano baina ya mji na vijiji, matabaka, dhana potofu, nafasi ya mwanamke na elimu. Japo matini iliyohakikiwa ni tofauti, utafiti huu umenufaika katika kuchunguza usawiri wa wahusika katika riwaya teule.

Utafiti kuhusu riwaya ulifanywa na Mayaka (1991). Mtafiti alichunguza ukengeushi wa wasomi katika riwaya za Kezilahabi. Mtafiti alitumia riwaya zifuatazo: *Rosa Mistika*, *Kichwa Maji*, *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Gamba la Nyoka*. Mtafiti alitambua kuwa wahusika wasomi wamekengeuka. Mtafiti alibaini kuwa wasomi walishikilia nafasi kubwa katika jamii ingawa kulikuwa na matatizo yaliyoletwa na ukengeushi. Japo riwaya alizofanyia utafiti ni tofauti, utafiti wake ulifanikisha utafiti huu kuchunguza usawiri wa wahusika.

Katika utafiti wake, Mlacha (1996) alichunguza utamaduni wa Mwafrika katika riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka*. Mtafiti alitafiti nafasi ya riwaya husika katika kutunza na kusambaza mila na desturi kwa watu wa jamii ya Wakerewe. Riwaya hii ni mojawapo ya riwaya ambazo zimezingatia utamaduni wa Mwafrika. Uchunguzi umeonyesha kuwa riwaya hii imezingatia zaidi mila na desturi za Wakerewe kwa kutumia maisha ya kila siku ya familia ya Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka. Maisha yao yameonyesha mzunguko baina ya mtu, utamaduni na muundo wa jamii husika. Mtafiti amebaini njia zinazotumiwa na wanajamii kwa makusudi au bila kujua katika utunzaji na usambazi wa mila na desturi hizo. Mtafiti alitambua kuwa riwaya hii ina muundo wa hali ya juu katika kujenga dhamira ya mila na desturi za Wakerewe. Japo mtafiti amechunguza maudhui ya utamaduni, hajachunguza kipengele cha usimulizi ambacho utafiti huu ulichunguza. Utafiti wa Mlacha ulifaidi utafiti huu kutambua mpangilio wa hadithi.

Utafiti uliofanywa na Swaleh (1997) ulichunguza taswira ya mwanamke katika riwaya ya M. S Mohamed, *Tata Za Asumini*. Mtafiti alitambua kuwa mwanamke amesawiriwa kama kiumbe dhaifu kilichopuuza jitihada za kujikomboa. Mtafiti anamuona mwanamke kama zao la utamaduni unaomtukuza mwanamume. Aidha, mwanamke anamngojea mwanamume amkomboe kutoka kwa utumwa. Mtafiti anatoa pendekezo kuwa wakati umewadia wa mwanamke kujikomboa kutokana na ulimwengu

uliotawaliwa na mwanamume. Mtafiti anapendekeza kwamba waandishi wa riwaya wawachore wanawake kama viumbe vilivyo na uwezo wa kujimudu. Tofauti na utafiti wa Swaleh uliyochunguza taswira ya mwanamke, utafiti wake ulifaidi utafiti huu kuwasawiri wahusika wa jinsia zote katika riwaya teule.

Akishughulikia mienendo mipya katika uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*, Mbatiah (1997) alilenga kudhibitisha kwamba baada ya kuchapisha *Nagona* na *Mzingile*, uandishi wa Kezilahabi umeingia katika mkondo mpya. Mtafiti alitambua kwamba kazi hizi mbili ni za kifalsafa ya udhanaishi na zinatoa mwandishi kutoka tapo la waandishi wa kiuhalisia na kumtia katika tapo la fasihi ya uduni inayodhamiria kuvunja kaida za uandishi wa riwaya. Japo utafiti huo umechunguza uandishi mpya, utafiti huu ulichunguza mbinu za usimulizi zilizotumika kusimulia riwaya ya kwanza ya Kiswahili kuwa katika msururu wa riwaya tatu. Utafiti wake ulisaidia utafiti huu kutafiti upekee wa riwaya trilojia ya *Siri Sirini* kwa kuchunguza wahusika na mbinu za usimulizi.

Utafiti wa Wamitila (2002) ulichunguza suala la mandhari katika fasihi ya Kiswahili. Katika uchunguzi, mtafiti alitumia riwaya: *Kuishi Kwingi ni Kuona Mengi*, *Rosa Mistika*, *Nyongo Mkalia Ini*, *Wema Hawajazaliwa*, *Walenisi*, *Kichwa Maji*, *Utengano*, *Kosa la Bwana Msa* na *Mzimu wa Watu wa Kale*. Mtafiti alitambua kuwa mandhari yanahusiana na sehemu zingine za kimuundo katika matini za kibunifu na kuwa mandhari hutumika kijazanda kuonyesha mtazamo wa mwandishi wa riwaya, muundo, motifu na wahusika. Ingawa matini zilizochanganuliwa ni tofauti, kazi yake ilinufaisha utafiti huu kuchunguza usimulizi wa mandhari ambacho ni kipengele cha fani.

Makala kuhusu riwaya yalishughulikiwa na Wamitila (2003). Mtafiti alichunguza ikiwa mna kuathiriana au kuingiliana katika uandishi wa riwaya za Kezilahabi, *Nagona* na *Mzingile* na ile ya Juan Rulfo, *Pedro Paramo*. Mtafiti alichunguza ukiukaji wa utaratibu wa kiwakati, mpangilio wa matukio, muundo na uhusiano wa kazi hizi. Mtafiti alibaini kwamba riwaya zote ni fupi, zenye muundo changamano na zimekiuka utaratibu wa muundo wa riwaya hasa kwa upande wa ploti, ukuaji wa wahusika, mandhari na mtazamo. Mtafiti alitambua kuwa riwaya hizi zinaingiliana na kwamba kuathiriana ni aina moja ya mwingiliano. Japo mtafiti amechunguza kuathiriana na kuingiliana kwa

riwaya kwa kuzingatia wakati, mpangilio wa matukio, muundo na urefu, matini zilizotafitiwa ni tofauti. Utafiti wake ulinufaisha utafiti huu kuchunguza mfuatano wa matukio kiwakati katika riwaya trilojia.

Utafiti wa riwaya ulifanywa na Vonyoli (2004). Mtafiti alitafiti hadithi kama chombo cha maudhui katika fasihi kwa kutumia riwaya za Mkangi, *Mafuta* na *Walenisi*. Mtafiti alitambua kwamba hadithi hizi ni mafumbo yanayobeba maudhui mazito yanayohusishwa matukio ya kihistoria hasa ubepari na mapinduzi. Mtafiti ameonyesha nafasi za wahusika katika hadithi hizi. Ingawa mtafiti alichunguza matini tofauti na utafiti huu, utafiti wake ulifaa utafiti huu kutafiti kipengele cha wahusika.

Kuhusiana na maendeleo ya riwaya ya Kiswahili, Ntarangwi (2004) anaeleza kuwa riwaya ilianza kama hadithi zilizoandikwa kinathari. Mtafiti anafafanua kuwa riwaya kama kazi ya fasihi andishi ni utanzu wenye uwezo wa kuzingatia mambo kwa upana sana. Mambo haya yanaweza kuwa ya kimaudhui au kimuundo. Mhakiki anaeleza kuwa riwaya inaweza kuhakikiwa kwa kuzingatia mtunzi au kujadili kazi yenyewe kwa kuzingatia maudhui na fani. Kuhusu wahusika, mhakiki anaeleza kuwa wahusika ni viumbe wa hadithini waliobuniwa na msanii ili kuendeleza maudhui katika kazi yake. Mtafiti anaeleza kuwa mhusika hupewa maneno, dhana na hulka ambazo ni muhimu katika kujenga hadithi, dhamira na maudhui katika kazi ile. Mtafiti anatoa maelezo kwamba wahusika hutambuliwa kwa majina yao, majukumu yao katika kazi nzima, mahusiano yao na wengine, masengenyo ya wengine kuwahusu wao na maelezo ya mtunzi kuwahusu. Maandishi ya mtafiti yalikuwa mwanga katika kuchunguza vipengele vya usimulizi na wahusika katika riwaya trilojia.

Utafiti wa Musee (2007) ulichunguza matumizi ya majazi kama mkakati wa kuepuka upigaji marufuku katika riwaya za Mkangi, *Mafuta* na *Walenisi*. Mtafiti alitambua kuwa riwaya hizi zimetumia mtindo wa majazi kwa sababu mwandishi aliogopa utawala uliokuwepo. Kazi hizi ziliangazia masuala nyeti ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ya wakati ule. Mtafiti alibaini kuwa Mkangi anadhihirisha kuwa udhalimu wa watawala sio pigo kubwa kwa waandishi wapigwao marufuku kwani kunayo njia ya kuifikia hadhira kama mwandishi. Mtafiti alifahamu kuwa viwango vya majazi ni matumizi ya majina yanayoakisi maana na kwamba katika kazi za fasihi, waandishi huwapa

wahusika, mahali na vitu majina yanayodokeza sifa na tabia zao. Ijapokuwa utafiti wa Musee umeegemea majazi, ulifaidi utafiti huu kutafiti usawiri wa wahusika katika matini teule.

Ochenja (2008) alitafiti sifa zinazofanya riwaya za Walibora kubainika zaidi kama maigizo kuliko kama masimulizi ya kinathari. Mtafiti alichunguza ikiwa maudhui ya riwaya za Walibora yamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuyafanya masimulizi yake yawe kama maonyesho. Alitumia riwaya, *Ndoto ya Amerika* na *Kufa Kuzikana*. Mtafiti alichunguza namna Walibora alivyotumia mtindo wa maigizo katika kueleza maudhui ya riwaya zake. Mtafiti alionyesha namna uhalisi unavyojitokeza katika vitabu vya mwandishi huyu kupitia mandhari, vitendo na maneno ya wahusika. Mtafiti ametambua kuwa riwaya za Walibora ni mfano mahsusi wa mwingiliano kati ya sifa za riwaya na sifa za tamthilia na kuwa maudhui ya riwaya zake yamechangia pakubwa katika kuyafanya masimulizi yake kuwa kama maigizo. Ijapokuwa riwaya zilizotafitiwa ni tofauti, utafiti wake ulifaa utafiti huu kuchunguza usimulizi wa mandhari na usawiri wa wahusika.

Utafiti wa riwaya ulifanywa na Kavuria (2008). Mtafiti alichunguza dhuluma dhidi ya watoto katika riwaya za Kiswahili akitumia riwaya: *Siku Njema*, *Kipimo cha Mizani*, *Tumaini* na *Yatima*. Mtafiti alichunguza sura mbalimbali za utekelezaji wa dhuluma, asasi mbalimbali zinazoendeleza dhuluma, njia mbalimbali za utekelezaji wa dhuluma, utambuzi wa dhuluma na athari mbalimbali kwa watoto. Mtafiti alitambua kuwa watoto walijeruhiwa kimwili, kihisia, kimapenzi na kiusalama. Mtafiti alitambua kuwa wanaowadhulumu watoto ni wazazi halisi na wazazi wa kambo, walezi, waajiri, walimu au watoto wenyewe wanawadhulumu wenzao. Mtafiti amewasawiri wahusika hawa kuwa wakatili. Mtafiti ameonyesha kuwa waandishi wa kike na wa kiume wamelingana katika kulisawiri tatizo hili. Ingawaje matini zilizotafitiwa ni tofauti, utafiti wake ulifaa utafiti huu kuchunguza usawiri wa wahusika katika riwaya trilojia.

Utafiti wa Rono (2013) ulihakiki maudhui na fani katika riwaya ya *Kidagaa Kimemuozea*. Mtafiti alichunguza maudhui na mbinu zilizotumiwa kuwachora wahusika. Mhakiki amefanikiwa kushughulikia maudhui ya uozo wa viongozi, matabaka, uasi, ukatili, ulevi, tamaa, malezi, ushirikiano, utu na uzembe. Mtafiti

amefanikiwa kuangazia dhana ya mhusika na njia tofauti za kuainisha wahusika. Japo mtafiti amehakiki maudhui na wahusika, utafiti wake ulisaidia utafiti huu kuchunguza usawiri wa wahusika katika matini teule.

Katika utafiti wake wa riwaya, Sabula (2014) alichunguza nafasi ya wanawake katika uhifadhi wa mazingira katika riwaya ya *Nakuruto*. Mtafiti alibainisha kuwa ufeministi wa kiekolojia una nafasi ya kuwazindua wanawake na kuleta ukombozi wa kimazingira. Mtafiti alitambua kuwa: Mhusika Nakuruto aliwazindua wanajamii kupitia elimu na maarifa yake ya kimazingira hivyo kusababisha mapinduzi, kusimangwa, kutukanwa na kudharauliwa kwa wanawake wanapojihusisha na harakati za utunzaji wa mazingira. Pia, alibainisha kwamba umaskini, kukauka kwa chemichemi za maji, uskwota, magonjwa na vifo ni athari zinazosababishwa na uharibifu wa mazingira. Tofauti na utafiti wa Sabula uliotafiti mhusika mwanamke, utafiti wake ulisaidia utafiti huu kuchunguza usawiri wa wahusika wa jinsia zote katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

Riwaya ilitafitiwa na Kilonzo (2015). Mtafiti alichunguza Ujitambuzi na Utambulisho wa Kijinsia katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Mtafiti alitambua kuwa Ujitambuzi na Utambulisho wa Kijinsia katika kupigania ukombozi wa kijinsia katika jamii ni suala linalohitaji kuhusishwa kwa jinsia mbili ili lifanikiwe. Mtafiti alibaini kuwa jinsia ya kike ndiyo inayoonekana kuwa mstari wa mbele kupigania ukombozi. Alitambua kwamba ukombozi wa kijinsia unapaswa kushughulikiwa katika masuala ya kisiasa, kidini na kiuchumi. Japo utafiti wake unatofautiana na huu kwa vile umelenga maudhui ya kijinsia, ulisaidia utafiti huu kuwasawiri wahusika katika riwaya teule.

Nyamete, Buliba na Kamau (2016) walitafiti ufafanuzi wa vichocheo vya migogoro ya kindoa katika riwaya ya *Kidagaa Kimemuozea*. Watafiti hawa walitambua kuwa migogoro ya kindoa katika riwaya husika ilisababishwa na: Kukosekana kwa uaminifu katika ndoa, ubinafsi, kiburi, mawasiliano finyu, kutowajibika, tofauti ya asili ya wanandoa, tamaa iliyokithiri na tendo la ndoa ambalo limefanywa kuwa himaya ya wanaume. Watafiti walibaini kwamba migogoro ni jambo la kawaida katika mahusiano ya kimapenzi na kwa hakika haliepukiki isipokuwa wenza kujifunza jinsi ya kukabiliana nalo na kuondoka wakiwa salama. Ingawa matini iliyochunguzwa ni

tofauti, utafiti wao ulifanikisha utafiti huu kutafiti usawiri wa wahusika katika trilojia teule.

Utafiti uliotathmini mabadiliko ya usawiri wa mwanamke katika riwaya ya *Utengano* na *Kamwe si Mbali Tena* ulifanywa na Fasih (2017). Utafiti wake ulitambua kuwa mwanamke ni mhusika binadamu kama wanadamu wengine, kwamba ana uwezo mkubwa wa kutenda mambo mbalimbali, mema na mabaya. Mtafiti alibaini kwamba kuna tofauti baina ya usawiri wa mwanamke katika maisha ya zamani (*Utengano* 1980) na usawiri wa mwanamke katika riwaya ya kisasa (*Kamwe si Mbali Tena* 2014). Vilevile, ameonyesha kwamba mwanamke ni mhusika anayekwenda sambamba na mabadiliko ya wakati, historia, imani, ushirika, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Japo utafiti wa Fasih unafanana na utafiti huu kwa kulenga usawiri wa mhusika mwanamke, kuna tofauti. Utafiti huu ulinufaika na utafiti wake katika kuchunguza usawiri wa wahusika wa jinsia zote katika matini teule.

Utafiti wa Haji (2018) ulitathmini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*. Mtafiti alitambua kwamba riwaya hizi mbili zinafanana katika usawiri wa wahusika kwa mbinu zifuatazo: Mwingilianomatini, uzungumzi nafsi, kutumia wahusika wengine, majigambo, motifu ya safari na kidrama. Haji alitambua tofauti ya riwaya hizi mbili katika usawiri wa wahusika. Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* imetumia taharuki, visasili na ulinganuzi na usambamba ilhali riwaya ya *Asali Chungu* imetumia majazi na tayashuri. Japo riwaya za utafiti ni tofauti, utafiti wake ulifanikisha utafiti huu kutafiti usawiri wa wahusika.

2.3 Dhana ya Riwaya Trilojia

Zhang (2016) alitafiti hadithi inayowahusu vijana katika riwaya trilojia ya *The Beijing Trilogy*. Trilojia hii inahusisha; *Give me a Girl when I am Eighteen*, *Everything Grows* na *Beijing, Beijing*. Katika utafiti wake, Zhang alitambua kuwa wahusika vijana wa jinsia ya kike wamekandamizwa na kudunishwa. Wahusika vijana wa jinsia ya kiume wameonyesha taasubi ya kiume. Mtafiti anafafanua kuwa hadithi ya vijana katika trilojia hii imesimuliwa kwa ucheshi na kwa lugha inayowavutia wasomaji. Aidha, vijana wanachorwa kuwa na wasiwasi, sifa mojawapo inayowakumba vijana katika jamii. Wanafunzi katika Vyuho Vikuu wanaonyeshwa kuwa na changamoto nyingi. Japo

matini za utafiti ni tofauti, utafiti huo ulikuwa na manufaa katika kutafiti usawiri wa wahusika katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

Riwaya trilojia ilitafitiwa na Eslamich (2016). Mtafiti alitafiti kazi ya sanaa iliyoigwa katika *The New York Trilogy*. Trilojia hii inahusisha riwaya: *City of Glass*, *Ghosts* na *The Locked Room*. Mtafiti alibaini kuwa *The New York Trilogy* imeiga sanaa ya ujasusi. Mtafiti anafafanua kwamba hadithi inayosimuliwa katika msururu wa riwaya hizi ni moja na kuwa wahusika wakuu wanafanana katika uwasilishaji wa vituko vyao. Ingawa mtafiti amechunguza sanaa iliyoigwa tofauti na utafiti huu uliochunguza kipengele cha usimulizi na wahusika, utafiti wake ulisaidia utafiti huu kutafiti mtindo wa trilojia uliyotumika kusimulia riwaya trilojia teule.

Akishughulikia njia mwafaka za kuandika riwaya trilojia, Koboldt (2018) anafafanua kuwa kuandika trilojia huwa na manufaa mengi hasa kwa waandishi wa kazi za sanaa. Koboldt anaeleza kuwa uandishi wa trilojia humruhusu mwandishi kusimulia hadithi yake kwa kutumia wahusika walewale, mtindo uleule na mandhari ileile. Aidha, trilojia humpa msomaji uaminifu na humpa mwandishi hadhira kwa vitabu vingine vinavyofuatia. Anaeleza kuwa urefu wa riwaya katika msururu hutofautiana. Mtafiti anasisitiza kuwa msururu wa riwaya tatu unapendeza zaidi. Katika uandishi wa trilojia, mtafiti anafafanua kuwa kitabu cha kwanza ndicho rahisi kuandika kwa sababu hakina muda wa mwisho wa kukikamilisha. Kitabu cha pili ndicho kigumu kuandika kwa sababu wasomaji wa riwaya ya kwanza huwa na matarajio makubwa ya kuisoma ya pili. Muda wa kuandika riwaya ya pili huwa mfupina ni lazima mwandishi aendeleze hadithi aliyoanzia katika riwaya ya kwanza. Riwaya ya tatu huwa hitimisho. Ndiyo riwaya inayotamatisha hadithi na huwa muhimu sana. Mwandishi huwa na ushawishi wa kuona kwamba kila jambo katika msururu limeshughulikiwa ipasavyo kama vile kutatua migogoro aliyojenga katika riwaya ya kwanza na ya pili. Maandishi haya yalikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwa kuchangia ufafanuzi wa riwaya trilojia.

Katika utafiti wake, Rice (2018) anaeleza kuwa *The African Trilogy* inayohusisha *Things Fall Apart*, *No Longer at Ease* na *The Arrow of God* imelenga vizazi vitatu katika jamii ya Kiafrika. Kila kizazi kinajitahidi kupigana na ukoloni uliyoikumba

jamii. Japo utafiti wake umelenga suala la ukoloni, ulifaa utafiti huu kuhakiki masuala mbalimbali katika riwaya trilojia teule.

2.4 Riwaya Trilojia ya *Siri Sirini*

Utafiti kuhusu mchango wa wanawake katika jamii ulifanywa na Yenjela (2015). Mtafiti alichunguza mchango wa wanawake majagina katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*. Mtafiti aliangazia wahusika wanawake ambao ni: Malkia wa Sheba, Malkia Hatshepsut, Mwanakupona na Abanoye. Mtafiti alibaini kuwa Mwanakupona alichangia kuleta mabadiliko ya elimu nchini Shanga. Malkia wa Sheba alisababisha mapinduzi ya uongozi. Mtafiti anafafanua kuwa Malkia wa Sheba ni mfano wa wanawake wa Kiafrika wanaoweza kuigwa katika utatuzi wa masuala ya kijamii. Mtafiti anaeleza kwamba Malkia Hatshepsut alikuwa kiongozi wa kwanza nchini Misri aliyeongoza kwa muda mrefu, miaka ishirini na miwili. Malkia Hatshepsut alikumbukwa kwa mchango wake katika uchumi ulimwenguni. Abanoye alichangia katika ukombozi wa Washanga kutoka kwa uongozi dhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari. Baada ya ukombozi kupatikana, Abanoye hakudai wadhifa wowote katika serikali mpya ya Shanga. Tofauti na utafiti wa Yenjela uliotafiti wanawake majagina, utafiti wake ulinufaisha utafiti huu kuchunguza usawiri wa wahusika wote na kipengele cha usimulizi.

Yenjela (2017) alitafiti suala la historia katika riwaya teule nchini Kenya. Alitumia riwaya za Kiswahili: *Wimbo Mpya, Walenisi, Ukiwa, Mwisho wa Kosa, Anasa* na trilojia ya *Siri Sirini*. Mtafiti alibaini kwamba historia iliyosimuliwa katika riwaya hizi inalenga: Masuala ya vita na madhara yake, ukoloni na ukoloni mamboleo, unyanyasaji wa watu na mfumo wa kisiasa. Mtafiti alibaini kuwa mapenzi hayafungamani na misingi ya dini, matabaka au ukabila. Aidha, utafiti umeonyesha kuwa watu wanaoishi mijini wanapata changamoto nyingi hasa za kiuchumi lakini wanatafuta njia mbadala za kuyamudu maisha. Mtafiti aliegemea suala la historia katika riwaya alizochagua. Tofauti na utafiti wa Yenjela uliotafiti suala ya historia, utafiti huo ulifanikisha utafiti huu kuangazia masuala mbalimbali katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

2.5 Msingi wa Nadharia.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya naratolojia kwa sababu utafiti ulichunguza usimulizi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*. Nadharia ya naratolojia hutumika kuchunguza sifa za muundo wa simulizi kwa kugawa vipengele vya simulizi na kuzingatia uamilifu na uhusiano uliopo. Jambo muhimu katika naratolojia ni kutalii muundo wa hadithi na kwa kufanya hivyo kuna uhitaji wa kuchunguza sehemu mbalimbali za muundo huu na kufafanua uhusiano uliopo baina ya sehemu hizo (Ong'ondi, 2005). Fludernik (2009) anaeleza kuwa naratolojia hutoa vipengele vinavyoweza kutumiwa katika kuzihakiki simulizi kwa kuchunguza sifa za ndani za muundo wa hadithi, usimulizi wake, mtazamo unaotokea, usemi wa wahusika pamoja na wakati. Nadharia hii inahusu simulizi na usimuliaji wake na ilikuwa ya manufaa katika kubainisha vipengele vya usimulizi katika riwaya hii.

Kulingana na (Wamitila, 2002) Nadharia ya naratolojia imewekewa msingi na mawazo ya mwanafalsafa wa Kiyunani, Plato (428-348). Mawazo haya yanajitokeza katika andiko la *The Republic 111* ambapo alitumia dhana mbili za kimsingi, 'daigesia' na 'mimesia'. Katika 'daigesia', msimulizi anajitokeza wazi wazi na kutambulika ilhali katika 'mimesia' msimulizi hajitokezi wazi. Mwanafunzi wa Plato, Aristotle alikiangalia kipengele cha kuelezea kama chenye sifa ya ki-mimesia (mtaje). Aristotle katika andiko la *The Poetics* anatambua mhusika na kitendo kama kipengele muhimu katika hadithi na kusema kwamba tabia ya mhusika lazima ionyeshwe kupitia ploti (Habib, 2011). Nadharia ya naratolojia ilichipuka kutokana na nadharia ya umuundo ya Kirusi iliyoasisiwa na Vladimir Propp (1928). Katika *The Morphology of the Folktale*, Propp alichunguza hurafa zaidi ya mia moja na kutambua matukio fulani yaliyozihusisha. Katika kazi hiyo anaorodhesha matukio hayo na viamili vyake katika mfuatano maalum wa kiusababishi. Shughuli mbalimbali juu ya nadharia ya kimuundo zilianza kuchukua mkondo mahsusi baada ya 1958 hasa baada ya tafsiri ya kazi ya Propp ya *The Morphology of the Folktale*.

Naratolojia ilianza kama somo baadaye mwaka wa 1966 baada ya uchapishaji wa makala maalum, 'Communications' yaliyotengewa uchambuzi wa muundo wa hadithi (Wambui, 2018). Wambui (2018) anaeleza kwamba makala haya yalikusishwa wachangiaji kama Bremond Claude (1970), Roland Barthes (1975), Tzevetan Todorov

(1977) na Seymour Chatman (1978). Kazi ya Ferdinand De Saussure inahusiana na ile ya Propp hasa katika uchunguzi wa hadithi (Ghosh, 2016). Nadharia hii ilikuzwa na kutumika zaidi nchini Ufaransa hasa katika miaka ya 1970 kama anavyodokeza Wambui (2018) Mtaalamu mwingine aliyerejelewa katika ukuaji wa nadharia ya Naratolojia ni Lord Raglan katika kazi yake maarufu *The Hero* (Wamitila, 2002). Raglan alivichunguza visasili vya jamii mbalimbali akiyaangazia maisha ya mashujaa wa kitamaduni. Raglan alitokeza na sifa ishirini na mbili alizoieleza kama motifu zinazopatikana katika visasili vingi. Motifu hizo huwa na mfuatano maalum kama vile: Kuzaliwa kwa shujaa hutabiriwa, kuzaliwa kwake hutanguliwa na matukio maalum na ya kushangaza, hufanywa jaribio la kuuliwa, huenda kuishi mbali na kwao, hukumbana na majaribu mengi, hurejea baadaye kuikomboa jamii yao na mwishowe hufa kwa kusalitiwa (mtaje).

Naratolojia ni nadharia inayojishughulisha na sifa zinazofafanua matukio, muundo wa matukio, mfuatano wa visa au maudhui yake (Wamitila, 2002). Inashughulikia aina za wasimulizi na mbinu mbalimbali za usimulizi zinazotumika kuisimulia hadithi (Abrams, 1999). Nadharia ya naratolojia husaidia kuelewa, kuchanganua na kutathmini hadithi (Bal 1999) na hufafanua hadithi kwa kutoa maelezo ya matukio fulani na mfuatano halisi au ya kibunilizi na kutambua kuwa hadithi hutambwa kwa njia mbalimbali kama vile kusimuliwa kwa njia ya nathari, ushairi, katika maandishi au simulizi (Wamitila, 2002). Naratolojia huchunguza mfuatano wa matukio katika matini kiwakati na kwamba mbinu mbalimbali za kisimulizi kama vile mbinu rejeshi au mbinu elekezi husababisha matukio kutofautiana kiwakati (Bal, 1999). Jinsi mbalimbali ya kuwasilisha matukio katika matini yoyote ni muhimu katika naratolojia. Jinsi hizi ni uelezaji (daigesia) na uonyeshaji (mimesia). Aidha, matukio yanaweza kusimuliwa baada ya kutokea, kabla ya kutokea au wakati huo yanapotokea (Wamitila, 2002).

Kipengele cha wakati ni muhimu katika usimulizi kwa sababu matukio yoyote hutendeka katika wakati maalum. Naratolojia inabainisha kati ya wakati-hadithi na wakati-matini. Wakati pia, huweza kuangaliwa kwa kuchunguza mpangilio wa hadithi, muda na idadimarudio (Bal, 1999). Nadharia ya naratolojia vilevile, huchunguza mtazamo wa msimulizi. Msimulizi anaweza kuwa na mtazamo fulani kuhusu masuala fulani angetaka kumshirikisha msomaji (Wamitila, 2008). Nadharia ya naratolojia

huwaangalia wahusika kama kipengele muhimu cha matini ya kifasihi. Wahusika wanaelezwa moja kwa moja au kwa kuwahusisha matendo yao, maneno yao, sura zao, mazingira, mandhari au hali yao (Abrams, 1999).

Wana-Naratolojia wameonyesha umuhimu wa msimulizi, jinsi mbalimbali za kuwasilisha hadithi, wakati na umuhimu wa wahusika katika kujenga vitushi na kuendeleza hadithi. Wametambua umuhimu wa nadharia ya naratolojia katika kutoa mwongozo wa kuhakiki matini. Nadharia ya Naratolojia ni muhimu katika utafiti huu kwa vile uchunguzi wa ki-naratolojia unahusisha: Hadithi, msimulizi, njia na jinsi ya kusimulia hadithi, mfuatano wa matukio kiwakati na wahusika. Nadharia ya naratolojia ilifaa utafiti huu kwa sababu ilitoa mwelekeo wa yaliyochunguzwa kuhusiana na vipengele vya usimulizi na wahusika.

Mihimili ya nadharia ya naratolojia ni mingi kama ilivyojadiliwa hapo juu lakini utafiti huu ulitumia mihimili mitatu ambayo ni:

- i) Kutambua kuwa matukio katika matini huweza kusimuliwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za usimulizi.
- ii) Kutambua mfuatano wa matukio kiwakati na kwa kuzingatia mpangilio wa hadithi, muda na idadimarudio katika usimulizi.
- iii) Kutambua kipengele cha wahusika katika usimulizi.

Vigezo hivi vilizingatiwa kuchunguza mbinu za usimulizi na usawiri wa wahusika katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

2.6 Hitimisho

Mwauo wa maandishi umebainisha kuwa usimulizi ni nguzo kuu katika uwasilishaji wa ujumbe. Maandishi haya yameonyesha kuwa usimulizi unahusishwa na tenzi, filamu, nyimbo, muziki, ngoma, mazungumzo, hadithi za watoto, michezo ya Kompyuta, densi, michezo ya watoto, ufarishi na riwaya. Vilevile, maandishi yameonyesha kuwa riwaya ya Kiswahili imefanyiwa utafiti wa kimaudhui na kifani. Maandishi pia yameangazia vipengele vya nadharia ya naratolojia ambavyo viliongoza utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Mpangilio wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kifasihi ambapo riwaya trilojia ya *Siri Sirini* iliteuliwa miongoni mwa riwaya nyingi. Ni utafiti wa maktaba. Katika maktaba, mtafiti alidurusu maandishi yaliyoeleza nadharia ya naratolojia iliyotumika kama msingi katika utafiti. Mtafiti alisoma maandishi yaliyomsaidia kufahamu mbinu za ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Maandishi kuhusu usimulizi katika fasihi, riwaya ya Kiswahili na riwaya trilojia yalisomwa. Utafiti pia ulifanywa kwenye mtandao kwa maana tarakilishi ilikuwa nyenzo muhimu ya kupata maarifa zaidi juu ya mada. Matini za *Siri Sirini 1, 2 na 3* zilisomwa na mtafiti kwa makini ili kuelewa yaliyochunguzwa katika utafiti. Matini tatu za *Siri Sirini* zilisomwa na kupata data. Mtafiti alihakiki riwaya trilojia ya *Siri Sirini* kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya naratolojia na madhumuni ya utafiti. Mtafiti aliwasilisha matokeo ya data aliyokusanya kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti.

3.2 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli maksudi ilitumiwa katika kuteua utanzu wa fasihi andishi. Sampuli lengwa katika utafiti ni usimulizi katika riwaya trilojia. Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* iliteuliwa kwa mbinu maksudi kwa sababu ina data iliyohitajika. Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* imetungwa na Rocha M. Chimera kwa kutumia mbinu mbalimbali za usimulizi. Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* aidha ina upekee wa kuandikwa katika msururu wa riwaya tatu ambazo ni *Siri Sirini 1, Mshairi na Mfungwa, Siri Sirini 2, Mpiga Mbizi Kilindini* na *Siri Sirini 3, Mtihani wa Mwanamke*. Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* ni riwaya ya kwanza ya Kiswahili kuandikwa katika msururu wa riwaya tatu hivyo kuwa na msukumo wa kuchunguza mbinu mbalimbali za usimulizi zilizotumika kuisimulia hadithi hii.

3.3 Ukusanyaji wa Data

Hatua ambazo zilichukuliwa katika ukusanyaji wa data zinaweza kuelezwa kama ifuatayo: Mtafiti alisoma matini tatu za *Siri Sirini* kwa makini. Baada ya kusoma, mtafiti alidondoa mambo muhimu kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti ambayo ni mbinu za usimulizi na usawiri wa wahusika. Kisha mtafiti aliyapanga aliyoyadondoa katika sura huku akiyaeleza kwa lugha nathari.

3.4 Maadili ya Utafiti

Mtafiti aliwanukuu wasomi na waandishi wengine kitaaluma na kuandika katika marejeleo. Mtafiti alichanganua data kwa dhati kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya naratolojia ili kuepukana na mapendeleo. Kamati ya Maadili ya Chuo Kikuu cha Chuka iliidhinisha utafiti huu kwamba umekubaliwa kufanywa na kupendekeza kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi kutoa kibali. Mtafiti aliomba cheti cha kufanya utafiti kutoka Halmashauri ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi na akakipata kabla ya kuanza utafiti.

3.5 Uchanganuzi wa Data

Mtafiti alichanganua data aliyokusanya kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti na kuegemea nadharia ya naratolojia. Mtafiti alibainisha mbinu za usimulizi zilizotumika kuisimulia riwaya trilojia ya *Siri Sirini* kama vile usimulizi wa: Hotuba, nyimbo, kirejeshi, elekezi, tautolojia, ki-itimamu, motifu ya safari, muhtasari, penyezi, udondoshi, mandhari, mazungumzo, ndoto na idadimarudio. Maelezo ya jinsi wahusika walivyosawiriwa katika riwaya teule yalielezwa kwa maandishi ya nathari.

3.6 Uwasilishaji wa Data

Uwasilishaji wa kimaelezo ulizingatiwa katika kuiwasilisha data iliyokusanywa kuhusiana na mbinu mbalimbali za kiusimulizi zilizotumiwa kuisimulia riwaya hii trilojia na usawiri wa wahusika. Mtafiti alidondoa mbinu za kiusimulizi katika riwaya husika huku akinukuu vifungu vinavyodhihirisha mbinu husika, akaifafanua kisha kuifasili. Wahusika walisawiriwa kama mhusika mkwezwa ambaye ni Fumo Liyongo. Sifa zake zilijadiliwa na mifano kunukuliwa kutoka kwa riwaya, yakafafanuliwa na fasili kuelezwa kwa lugha nathari. Mhusika wa kisaikolojia ni Abanoye na Osman Ali Kidhabi. Wahusika wa kimapinduzi wameonyeshwa kuwa wengi. Kazi hii iliwasilishwa katika sura sita. Sura ya kwanza ina utangulizi, usuli wa utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na maelezo ya istilahi. Sura ya pili imeangazia mwauo wa maandishi ambao ni: Usimulizi katika fasihi, riwaya ya Kiswahili, dhana ya riwaya trilojia, riwaya trilojia ya *Siri Sirini* na misingi wa nadharia. Sura ya tatu imeonyesha mpangilio wa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, maadili ya utafiti, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

Sura ya nne na tano imejikita katika matokeo ya utafiti. Sura ya sita ni muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

3.7 Hitimisho

Sura hii imejikita katika mambo muhimu ya kimsingi katika utafiti huu. Mambo yaliyojadiliwa katika sura hii yalitoa mwongozo katika utekelezaji wa utafiti. Vipengele vilivyozingatiwa ni: Mpangilio wa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, maadili ya utafiti, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

SURA YA NNE

MBINU ZA USIMULIZI KATIKA RIWAYA TRILOJIA YA *SIRI SIRINI*

4.1 Utangulizi

Usimulizi ni maelezo ya jambo, kisa au matukio fulani kwa njia ya moja kwa moja au mikatizo ya hapa na pale. Wamitila (2003) anaeleza kuwa usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi na kwamba kazi yoyote ya fasihi huwa mna kisa kinachosimuliwa na msimulizi. Msimulizi husimulia hadithi kwa njia fulani. Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* imesimuliwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za usimulizi. Baadhi ya mbinu hizi za usimulizi ni kama vile:

4.2 Usimulizi wa hotuba

Usimulizi wa hotuba ni mazungumzo rasmi yanayotolewa katika vikao rasmi kama vile katika sherehe za kitamaduni, hafla za kisiasa, kortini, msikitini, mazishi na arusini (Matei, 2011). Kwa kawaida hotuba hutolewa na watu maalumu katika nafsi ya kwanza na huteuliwa mada mahsusi. Hotuba huwa rasmi kwa sababu ya mchanganyiko wa watu wanaohutubiwa na hutumia maswali balagha yanayonuiwa kumfanya msikilizaji kutafakari yanayosemwa. Hotuba huwa na mfululizo wa mahadhi na mdundo wa kupendeza bila kukatiza semi wala kusitasita isipokuwa mahali pa kupumua. Lugha inayotumika katika hotuba huwa na ushawishi mwingi (mtaje). Hotuba mbalimbali zimetolewa katika riwaya hii kwa mfano:

Baada ya maamkizi na wahusika kadha kufunga swala na kuswali Suna, Kibwana akiwa mmoja wao, hotuba ikaanza. Watu wakatulia wakawa wenye kuisikiza hotuba hiyo pamoja na mawaidha yanayoambatana nayo kwa utulivu mkuu...Wakati huo huo wakaingia wakaingia askari wengi, makubadhi nyayoni! Moja kwa moja wakawaendea Kibwana na mwanamfaume. Wakawatenganisha wawili hao kisha wakamtenga kabisa Kibwana na watu wote waliokuwa karibu naye. Hapo kipigo kikaanza! Walimpiga Kibwana vibaya sana! (Siri Sirini 1 2013:6)

Msimulizi anafafanua kwamba msikiti ulitumika kusali na kutoa mawaidha ya dini kila Ijumaa. Waliohudhuria walikuwa watu wa matabaka mbalimbali kama vile mwanamfaume, mawaziri, Imamu na raia. Askari waliingia msikitini, wakamtenga mwanamfaume na Kibwana na kumchapa Kibwana bila huruma kuonyesha ukatili wa askari na uongozi dhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari. Tukio hili lilitokea baada ya Kibwana kutafutwa na Waziri wa Sheria kwa tuhuma ya kutunga shairi la 'Siri Sirini'.

Baadhi ya watu hawakuweza kutazamana machoni, wakiona aibu kwamba mwenzao ametandikwa mbele yao bila ya wao kumtetea kuthibitisha ukosefu wa heshima katika msikiti, pahali patakatifu. Kadhi Mkuu alishindwa kuvumilia uvunjaji wa sheria katika maeneo ya kuabudu na kuandika barua ya kustaafu cheo hicho.

Hotuba nyingine msikitini inasema hivi:

Wasemaji kadha wa kadha wakawa wanamalizia hotuba zao kwa maneno yale yale: Ikiwa miti mibichi, mikubwa, imara, iliyojaa utomvu na maji; mibuyu kama Mfawidhi inateketezwa; je ile ambayo tayari ishakaukia, na ambayo ikitiwa moto huchomeke wangu wangu huku ikitatarika kama kifuu cha nazi, kweli utasalimika...Shanga ni jehanamu na kuni ni wanyonge wote wa Shanga. (Siri Sirini 2 2014:155)

Wasimulizi wanaeleza dhuluma wanazopitia chini ya uongozi wa Mfalme Daudi Mringwari kwa vile Waziri wa mambo ya Nje, Mfawidhi Kijumwa Mfaume aliuliwa kikatili. Uchunguzi uliofanywa juu ya mauaji ya Waziri Mfawidhi Kijumwa Mfaume haukuonyesha aliyemuua. Raia hawakutosheka na matokeo ya uchunguzi huo kusababisha hotuba hiyo kutolewa baada ya sala ya Ijumaa. Hotuba inasimulia hofu ya wananchi huku wakitumia istihara ya jehanamu na kuni. Kila msemaji alikuwa amekasirika na walilimbikizia lawama watu bila kuwataja majina kwa maovu yote yaliyotendeka Shanga. Wananchi walitaka kuelezwa lililosababisha mauaji ya kikatili ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume na kufukuzwa nchini Shanga kwa Fumo Liyongo. Walitaka kuhakikishiwa usalama wao. Wasemaji walijisikia huru kusema lolote walilolitaka bila kuogopa kuchunguzwa kudhihirisha kiu cha mabadiliko kwa wananchi. Hata hivyo kulitokea msukumano na watu kujitayarisha kukimbia kutoka mahali pale. Watu walianza kuulizana mawsali huku uvumi ukienezwa kwamba Osman Ali Kidhabi na Kibwana Mwengo Bashee wangekamatwa. Katika vurumai hiyo, kikosi cha askari walifika mahali pale na kuwakamata Osman Ali Kidhabi na Kibwana Mwengo Bashee.

Kuna hotuba iliyotolewa nchini Misri kama ifuatayo:

Mimi niliyetunukiwa heshima hii ya kuiwakilisha nchi yangu katika hii fursa ya kutoa hotuba, naitwa Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Mimi kusema kweli, si mgeni hapa Misri... Nitaanza hotuba yangu kwa kwa kutowaficha. Nitawaambia ninavyohisi... Najihisi dhaifu sana katika ardhi hii kongwe ya Misri. Udhaifu wangu unatokana na

kuutambua utukufu wa mapisi ya Misri. Sii chumvi ninaposema kuwa Misri ni ulimwengu, nao ulimwengu ni Misri. Bila Misri, wanadamu wangukuwa tofauti ndogo sana na mahayawani. Misri ndiyo iliyowafunza wanadamu kuwa watu. (Siri Sirini 1 2013:276)

Msimulizi na wenzake: Waziri Mkuu, Suleiman Mringwari na Osman Ali Kidhabu walikuwa katika ziara nchini Misri kuonyesha uhusiano mwema. Walikuwa wametumwa na Mfalme Daudi Mringwari. Katika hotuba yake, Mfawidhi Kijumwa Mfaume alitaja kuwa alisomea nchini Misri katika Zutandifaki ya Al-Azhar na wahadhiri wake walimkumbuka alipowatembelea kuonyesha umuhimu wa elimu. Hotuba yake ililenga: Maendeleo ya nchi ya Misri kwa upande wa elimu, ustaarabu, dini, ukulima, ujenzi na uhusiano baina ya Misri na Shanga kudhihirisha ushirikiano wa nchi hizo mbili. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alieleza kuwa ujumbe wao ulikuwa kuomba kuanzisha uhusiano wa kielimu ili kuweza kupiga hatua za kimaendeleo. Athari ya hotuba hiyo ilikuwa kubwa mno kwa sababu wote jukwaani walisimama na kumshangilia, wengine walimzingira na kumpa pambaja na wengine kuuliza kama ndiye Mfalme Daudi Mringwari thibitisho la umaarufu wa mhutubu.

Hotuba nchini Misri ilitolewa katika dhifa ya buriani:

Dhifa ilipokuwa tayari kuanza, hotuba zikatolewa, hotuba zilizokuwa zimesheheni sifa za wageni watukuka wa Misri kutoka Barazinji. Kila aliyehutubu hakukosa kusisitiza ya kwamba mpaka baina ya Misri na Barazinji ni wa kidhahania tu; haukuwapo hasa!...Baada ya hotuba, watu walipewa uhuru wa kutangamana na kuzungumza wapendavyo. Hapo ndipo taswira kamili ya nani mwenye kuthaminiwa, na kwa jinsi gani, ilipojitokeza wazi. (Siri Sirini 1 2013: 326)

Msimulizi anajulisha kuwa hotuba zilizotolewa ziliwasifu wajumbe kutoka Shanga. Mhutubu aliwaeleza wasiojua kuwa Barazinji ilikuwa bara la watu weusi na kwamba wenyeji wa kusini mwa Misri mliishi Wanubi, waliokuwa weusi kuonyesha ushirikiano wa nchi hizo mbili. Msimulizi alifafanua kuwa watu weusi waliingia Kaskazini mwa Misri, wakapambana nao, wakawashinda na kuwatawala. Msimulizi alimaliza hotuba yake kwa kusema kuwa jangwa la Sahara haukuwa mpaka wa kudumu uliotenganisha Barazinji na kaskazini mwa bara zima kudhihirisha umoja wa mataifa.

Hotuba nyingine ilitolewa na mwanamfaume wa Misri kwa niaba ya aila ya kifalme; hotuba iliyosisimua sana. Mwisho Waziri Mkuu wa Shanga alitoa hotuba kwa niaba ya wageni wenziwe, Mfalme na Malkia wa Shanga na mwanamfaume aliyeandamana nao. Hotuba yake ilitafsiriwa kwa lugha ya Kiarabu cha Misri na Waziri wa Mambo ya Nje, Mfawidhi Kijumwa Mfaume kudhihirisha usomi na matembezi yake. Msimulizi alipomtaja mwanamfaume katika hotuba yake, macho takriban yote hapo uwanjani yalimwelekea mwanamfaume huku wakinong'onezana na kuitikiatia kwa vichwa vyao. Wanawake walionekana kufurahia kumuona mwanamfaume kuonyesha suala la utabaka. Watu walipewa uhuru wa kutangamana baada ya hotuba kuonyesha ushirikiano wa diplomasia huku mwanamfaume wa Shanga akizingirwa na watu wengi walioonekana kusikizana na kufurahia mazungumzo naye.

Hotuba mbalimbali zilitolewa baada ya wajumbe kurudi Shanga kama vile:

Nafasi ya kwanza alimpa Waziri wa Mambo ya Nje, Mfawidhi Kijumwa Mfaume ...Mfawidhi alifunga usimulizi wake kukuli: Mtukuka; wavyele walinena; 'Fedha zilivunja nguu na milima ikalala'. Basi na mimi kinyinginya chao, mnuna wao, huku nikifuata nyayo zao wayo juu ya wayo, nathubutu kusema: 'Wetu Ngaoyati, alilima nguma mathalan kilele cha mlima, mavuno aliyopata, lima zima nikwambie, na akavuna. (Siri Sirini 1 2013:370)

Hotuba ya msimulizi ilimsifu: Mtwala wa Misri, maendeleo, mafanikio ya mikutano na masomo waliyoyapata katika safari kudhihirisha mshikamano wa nchi ya Misri na Shanga. Msimuliaji aliwaambia kuwa Misri ilithamini sana Shanga na kwamba sifa za Mfalme Daudi Mringwari zilienea Misri. Alisisitiza kuwa watu wa Misri walitaka mataifa hayo mawili yawe na ukuruba mkubwa kuthibitisha ushirikiano wao. Baada ya hotuba yake, watu walifurahi na kupiga makofi huku wakifurahia kipawa chake cha utondozi ingawa Waziri Mkuu na Osman Ali Kidhabi hawakufurahia.

Mjumbe wa pili kutoa hotuba alikuwa Suleiman Mringwari. Anasema hivi :

Alitoa maelezo ya maendeleo ya miji miwili waliyowahi kuitembelea, vyombo vya usafiri, amara, unadhifu wa watu, mavazi yao, usafi wa miji, piramidi za Giza na Sifiniksi, upendo walionaoraia wa Misri. Alisema alivyohisi ni kuwa alienda hija (watu wakacheka). Akasisitiza kwamba kwake yeye, kwenda Misri ni sawa na kuhiji kwa vile huko ndiko alikozaliwa Nabii Musa, ndiko alikotafuta uhifadhi Nabii Issa, Nabii Muhammad alitembelea huko, Nabii Yusuf aliishi huko, Nabii Yakub hali kadhalika.

Hatimaye akapendekeza kwamba muhimu wabadilisha jinsi ya kuitana... Washanga vipawa wanavyo papa hapa Shanga, na inawabidi wavitumie kistahiki. (Siri Sirini 1 2013:371)

Msimulizi alibainisha bayana maendeleo ya nchi ya Misri katika sekta ya usafiri, usafi, mavazi, ujenzi, upendo na dini kudhihirisha hatua za kimaendeleo nchini Misri. Msimulizi alipendekeza Washanga kubadilisha jinsi ya kuitana. Badala ya watu kuitwa kwa vyeo vyao wawe wakiitwa kwa jina la kidini na la kitamaduni kuonyesha mabadiliko aliyoyapata yalikuwa ya kidini na kitamaduni. Athari ya hotuba yake inajitokeza Osman Ali Kidhabi alipohutubu kama ifuatavyo:

Akaikamata na kuwashambulia Mfawidhi na mwanamfaume moja kwa moja, akisema wawili hao ni 'Mfalme-mbadala' na 'Mfalme-mtarajiwa' mtawalia. Kikulacho ki nguoni mwako! Akatahadharisha! (Siri Sirini 1 2013:372)

Hotuba ya Kidhabi ilikuwa shambulizi huku akionyesha kwamba Mfawidhi Kijumwa Mfaume na mwanamfaume walijitwika uongozi nchini Misri. Kidhabi alimuomba Mfalme Daudi Mringwari kujihadhari kuonyesha chuki aliyokuwa nayo kwao. Watu walishtuliwa na hotuba hiyo huku Mfawidhi Kijumwa Mfaume na mwanamfaume wakianza kujitetea. Kwa hivyo, Mfalme Daudi Mringwari aliwaashiria kunyamaza na kusema kuwa wangepazungumzia masuala hayo katika kikao kingine kidogo.

Hotuba ya mwisho ilikuwa ya Waziri Mkuu. Waziri Mkuu alikubaliana na yote yaliyosemwa na wenzake. Watu walijiuliza kama alikubaliana na mambo yote kabisa au kuna baadhi ya mambo, japo machache ambayo hakukubaliana nayo. Kwa ufupi walimtarajia asawazishe yale yaliyosemwa na wenziwe wote kwa jumla pamwe na kuongezea yake kudhihirisha mgogoro baina yake, Mfawidhi Kijumwa Mfaume na mwanamfaume.

Dhabina alitoa mihadhara ifuatayo:

Katika mazingira hayo na muktadha wake mwafaka, masomo ya uzalendo yalianza. Mhadhiri katika vikao hivi, bila kuteuliwa kirasmi, alikuwa ni Bwana Harun Rashid Dhabina, Waziri wa Sheria, Elimu na Utamaduni... Walijikuta wakijiuliza: Huyu mzee yuko upande gani? (Siri Sirini 2 2014:168-174)

Mwandishi anafahamisha kwamba masomo ya uzalendo yalianza na mhadhiri alikuwa Harun Rashid Dhabina. Alianza mihadhara kwa kuzungumzia matukio

yaliyoshuhudiwa katika taifa la Shanga kama vile: Kukamatwa katika ardhi takatifu ya msikiti, hatua za kimaendeleo, shida ya Waswahili na kuvamiwa kwao na wageni. Kadhi Mkuu aliuliza kama ulikuwa ukweli taifa kadhaa ziliwahi kuporomoka kwa ajili ya ufisadi, mbinu mbovu za utawala, tabia mbaya za viongozi, ushirikina na kushiriki dhambi kuonyesha ujasiri. Maneno hayo yaliwanyamazisha wote waliokuwapo na kuyazingatia sana aliyoyasema hivyo kushindwa upande uliougwa mkono. Mhadhara mwingine ni huu:

Hakuna haja ya ufafanuzi, manake mambo yote yako wazi!
Hebu nitajie nchi yo yote Uswahilini ambayo bado haijaingiliwa na wageni... Anza kwa kumwalika kuhudhuria mhadhara utakaofuatia.
(Siri Sirini 2 2014:198-204)

Harun Rashid Dhabina alifafanua kuwa tatizo kubwa lililokabili Barazini nzima lilikuwa wageni kutoka Manga. Manga ndiko alikozaliwa Mwanananga, mke wa kwanza wa Fumo Liyongo dhihirisho la ubaguzi. Uzawa wa Fumo Liyongo ulijadiliwa. Harun Rashid Dhabina alisema kuwa Shanga ingepotelea katika mapisi na kumbukumbu zake zote iwapo haingejitenga na kiburi. Juma Obo aliona vigumu kukubaliana na tathmini hiyo ambayo ilikuwa kitovu cha mihadhara ya Harun Rashid Dhabina. Juma Obo alisimulia kuhusu uongozi mwanana wa Mfalme Daudi Mringwari ambao watu walipaswa kuenzi. Naibu wa Waziri Mkuu aliukosoa mkakati wa mhadhiri na kumuuliza ahusishe raia moja kwa moja katika baraza au kupitia viongozi wao wa mashinani waliowastahi kuonyesha ujasiri. Kwa hivyo, Harun Rashid Dhabina aliulizwa kumhusisha Kibwana Mwengo Bashee katika vikao vya mafunzo ya uzalendo. Mhadhiri alitoa mhadhara mwingine kama ifuatayo:

Nitaanza mhadhara huu kwa kutoa mfano, alinena Dhabina. Mfano huu ni wa kudhihirisha hatari ya kupokea mfumo wa maendeleo kutoka nje bila kuutia katika chungio ya kiwenyeji... Nina maana ya Liyongo kwa mfano. (Siri Sirini 2 2014:228-231)

Dhabina aliwaeleza wasikilizaji wake hatari ya kupokea mfumo wa maendeleo kutoka nje bila kuwahusisha wenyeji kuthibitisha uzalendo. Alifafanua kwa kutoa mfano wa Falme za Mbalanzi na Berbera ambazo hapo awali zilikuwa zimeendelea lakini hazikutambulika tena. Kadhi Mkuu alichangia mhadhara kwa kusema kuwa ufisadi, maonevu, dhuluma na imla katika uongozi huwa nguzo na nyenzo kuu za uzorotefu wa mataifa mengi. Harun Rashid Dhabina alitaka kuepuka maelezo hayo lakini Omar Said

alitaka jawabu. Harun Rashid Dhabina alijibu kwamba maovu yote yaliyotajwa yaliletwa na wageni kama vile Fumo Liyongo kuonyesha chuki.

Kwa hivyo, usimulizi wa hotuba umefanikisha usimulizi wa riwaya hii kwa kueleza masuala yanayohusu dini, historia ya nchi, maendeleo, uongozi na kufafanua masomo ya uzalendo katika jamii husika.

4.3 Usimulizi wa ki-itimamu

Usimulizi wa ki-itimamu ni usimulizi unaopatikana ambapo pana matumizi ya barua kuwasilisha ujumbe fulani (Wamitila, 2003). Barua ni njia kongwe ya mawasiliano baina ya mtu na mtu, mtu na watu, taasisi na mtu, taasisi na taasisi inayolenga kutoa taarifa au ujumbe fulani ambao ni muhimu kufahamika kwa upande uliolengwa na barua hiyo (Ali, 2017). Barua huandikwa katika karatasi na kutiwa kwenye bahasha na kisha kutumwa kwa mlengwa kupokea barua hiyo. Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia hivi sasa barua huandikwa kama ujumbe katika simu na kisha kutumwa kwa mlengwa na kumfikia mara moja. Hii haimaanishi kuwa mfumo wa zamani wa kuandika na kutuma barua haupo ila umepungua kama aelezapo (mtaje). Vifungu hivi vya barua hujitokeza katikati ya tendo fulani kama anavyovitumia mwandishi wa riwaya ya *Siku Njema* (Walibora, 1996) katika usimulizi wa riwaya husika hasa pale Zawadi Chui anamwandikia Kongowea barua iliyokuwa na habari mbalimbali za kushangaza. Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* imetumia barua katika usimulizi mfano wa barua ya Mwanananga kwa Fumo Liyongo inayosema:

Liyongo akakikunjua kile kigombo. Kadhi Mkuu akaichukua fursa hiyo kumwambia: Huwezi kuoia mke wa pili iwapo mkeo atakataa kutoa kibali. Hivyo ndivyo sheria ya dini yetu isemavyo. Shorti mke mkubwa akutakabaliye kwanza, ndipo iwe ni ruhusa kuoia... Ameniruhusu kumwoa Abanoye, lakini kwa masharti, tena magumu! (Siri Sirini 1 2013:345)

Msimulizi anafafanua kwamba Mwanananga alimwandikia mumewe barua kumruhusu kumwoa mke wa pili, Abanoye kuonyesha kanuni za dini husika. Fumo Liyongo alikuwa ametorokea nchi ya Ozi kama mkimbizi baada ya kuvunja ngome na kutoroka kudhihirisha ukatili wa uongozi wa Mfalme Daudi Mringwari. Huko Ozi alipewa makao na Omar Soba, babake Abanoye. Fumo Liyongo alitaka kumuoia Abanoye kwa kuzingatia sheria za dini ya Kiislamu. Fumo Liyongo alimwarifu mkewe wa kwanza,

Mwananinga alipomtembelea nchini Ozi kuthibitisha heshima ya Fumo Liyongo kwa Mwananinga. Kwa hivyo, Kadhi Mkuu alimuuliza Fumo Liyongo kutimiza masharti hayo. Barua nyingine iliandikwa na Mwanakupona hivi:

Akatoka amekamata magombo kadhaa. Nadhani ndio huu. Mwananinga ameuacha maksudi au amesahau... Liyongo hakusema kitu bali aliyakunjuakunjua yale magombo na kuyatazama huku akianza kuusoma. (Siri Sirini 1 2013:354)

Usimulizi wa barua hii unaeleza kuwa Mwanakupona aliandika barua ambayo ni utenzi aliotaka ughaniwe na mmoja wa wazazi wake siku ya arusi yake kuonyesha mchango wa ufanisi wa sherehe ya arusi. Wimbo huu haukuweza kuimbwa kwa sababu ya ukatili wa askari- ngome. Mwananinga alimpelekea mumewe ausome alipomtembelea nchini Ozi. Fumo Liyongo aliusoma na kukubali kwamba Mwanakupona alikuwa mshairi aliyepevuka kudhihirisha kipawa cha utunzi na jinsi elimu aliyosoma ilimsaidia katika utunzi. Mwanakupona alimkabidhi mamake waraka huu alipomtembelea Lamu kabla ya arusi yake. Mwanalemba aliandika barua ifuatayo:

Mzigo ndio huu. Alisema huku akimpatia Mwananinga magombo kadhaa ya maandishi. Mwananinga aliyapitishia macho chapuchapu magombo hayo, kisha ikabainika wazi kwa wenziwe waliokuwa wakimtazama kwa utulivu kwamba yeye mwenyewe utulivu ulikuwa unampaa. (Siri Sirini 2 2014:167)

Msimulizi anasimulia barua iliyoandikwa na Mwanalemba. Barua ilikuwa shairi la 'Siri Sirini' ambapo mtunzi alifichama maovu ya uongozi wa kakake Mfalme Daudi Mringwari. Mwanalemba alitaka Mwananinga kumpelekea Fumo Liyongo magombo hayo nchini Ozi ili atoe maoni yake kuonyesha mshikamano wa familia. Maandishi hayo yalimfurahisha Mwanaziza na kudai kuanza kwa mapambano ambayo yangeendelea hadi pale udhalimu ungekomesha kabisa. Fumo Liyongo aliyasoma magombo yale na kuathirika vya kutosha na kusema ya kwamba huo haukuwa utungo bali mzinga, silaha hatari kuthibitisha kwamba wangeutumia kupambana na uongozi dhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari. Kibwana Mwengo Bashee aliusoma na kuathirika huku Mfalme Daudi Mringwari, Osman Ali Kidhabi, Malkia Mwanalibasi, Waziri Mkuu, Naibu wa Waziri Mkuu na Waziri wa Sheria wakikanganywa na aliyekuwa mtunzi. Waziri wa Sheria alidai kwamba mtunzi alikuwa Mwanakupona. Mwananinga alikamatwa kwa madai ya kuwa mtunzi kudhihirisha udhalimu wa uongozi nchini Shanga.

Mwanaziza alimwandikia Mfalme Daudi Mringwari barua baada ya kukamatwa kwa Mwananinga. Inasema hivi:

Ni waraka kutoka kwa Mama Mwanaziza. Mfalme aliufungua waraka huo na kuusoma. Alipomaliza, akatangaza kama aliyeambiwa afanye hivyo: Shangazi anataka tumwachilie mkazamwanawe bila ... akauangalia waraka tena...bila usiri wala kulimatia. (Siri Sirini 2 2014:249)

Msimulizi anaeleza aliyoyasoma katika barua iliyoandikwa na Mwanaziza. Mwananinga alikuwa amekamatwa kwa madai ya kuwa mtunzi wa 'Siri Sirini' kuonyesha usaliti wa Mfalme Daudi Mringwari kwa aila ya Fumo Liyongo. Mwanaziza alimwandikia Mfalme Daudi Mringwari waraka huo kudai kuachiliwa huru kwa Mwananinga kudhihirisha nafasi yake katika familia pana ya Fumo Liyongo. Mfalme Daudi Mringwari alisoma barua ile na kuwatangazia waliokuwemo mahitaji ya barua ile, kumwachilia Mwananinga bila usiri wala kulimatia. Kwa hivyo, Mfalme Daudi Mringwari alitii amri ya mkongwe wao na kumwachilia Mwananinga baada ya kuhitimisha kikao hicho. Barua nyingine iliandikwa na Kadhi Mkuu inayosema hivi:

Utulivu ulipopatikana, Kadhi Mkuu alimwendea mwanamfaume na kumpatia kijigombo kilichoandikiwa maandishi...Ni kauli yangu ya kung'atuka! Nina maana nimeacha kazi! Tangu leo mimi si Kadhi Mkuu wa Shanga. Mwambie babako atafute mtu mwingine amkabidhi cheo hicho. (Siri Sirini 3 2014:7)

Kadhi Mkuu anasimulia kwa kutumia barua kustaafu kwake kuonyesha mapambano katika uongozi dhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari. Tukio hili lilitokea baada ya Kibwana Mwengo Bashee kupigwa na askari msikitini thibitisho la ukatili wa askari. Tukio hilo lilimkasirisha Kadhi Mkuu na kumwandikia Mfalme Daudi Mringwari barua. Ujumbe ulikuwa kuacha kazi kwake hivyo, kuwaacha watu na mshangao, mshtuko na kusawajika. Barua iliandikwa na Mfalme Daudi Mringwari. Inaarifu:

Mfalme Daudi akajibu kwa kumtuma mkubwa wake aende ngomeni na barua aliyoitia sahihi yeye mwenyewe, ya kuachiliwa kwa Kibwana. Kadhi Mkuu akaukubali utumwa huo, uliomfurahisha sana kwa hakika; akashika njia akaenda zake kutekeleza wajibu. (Siri Sirini 3 2014:244)

Msimulizi anaeleza kwamba Mfalme Daudi Mringwari aliandika barua ili Kibwana aachiliwe kudhihirisha msamaha. Kadhi Mkuu aliwajibika kutumwa kupeleka barua hiyo kuonyesha utiifu. Uongozi dhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari ulimtia Kibwana

kizuizini kwa kushiriki maandamano yaliyoitisha mabadiliko nchini Shanga. Tukio hili lilitokea baada ya uchunguzi wa mauaji ya Fumo Liyongo kukosa kuwaridhisha wananchi kuonyesha uongozi dhalimu nchini.

Usimulizi wa barua zilizoandikwa katika karatasi kama ujumbe mfupi au utungo na wasimulizi mbalimbali kama vile Mwananinga, Mwanakupona, Mwanalemba, Mwanaziza na Kadhi Mkuu umefanikisha usimulizi wa matukio mbalimbali katika riwaya hii.

4.4 Usimulizi penyezi

Usimulizi penyezi ni mbinu ya usimulizi ambapo msimulizi hujitokeza mara kwa mara na kutoa maoni, tathmini na mapendekezo au hata kuwauliza wasomaji maswali kama anavyofanya mwandishi wa riwaya ya *Can you Forgive Her?* (Wamitila, 2003). Mwandishi anaweza kutoa maoni yake kuhusiana na hali fulani au kumwelekeza msomaji. Upenyezi wa mwandishi ni sifa inayopatikana sana katika kazi za kifasihi. Usimulizi penyezi huigeuza kasi-hadithi ya hadithi. Usimulizi penyezi umetumika kuisimulia riwaya hii mfano:

Hatimaye akapendekeza kwamba ni muhimu wabadilishe jinsi ya kuitana. (Siri Sirini 1 2013:372)

Msimulizi alipendekeza wabadilishe mfumo wa kuitana majina katika hotuba yake aliyoitoa nchini Shanga baada ya kutoka Misri kuonyesha namna safari ya Misri ilivyombadilisha kiakili. Suleiman Mringwari alikuwa wa pili kutoa hotuba baada ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Baada ya kupendekeza wabadilishe jinsi ya kuitana, watu walitaka aeleze. Kwa hivyo, aliwaeleza kuwa huko Shanga kuna watu ambao hawakuitwa kwa majina yao abadani, bali waliitwa kwa vyeo vyao. Alifafanua kuwa hiyo haikuwa tabia nzuri na ilipaswa kukomeshwa. Suleiman Mringwari alipendekeza watu kuitwa kwa jina la kidini sambamba na lile la kitamaduni kama ilivyokuwa nchini Misri dhihirisho la mabadiliko.

Usimulizi penyezi unaonekana Osman Ali Kidhabi alipotoa maoni kuhusu arusi ya Mwanakupona:

Katika muktadha huo, mimi napendekeza ya kwamba Fumo Liyongo aruhusiwe kikamilifu lakini akiwa ndani ya ngome. (Siri Sirini 1 2013:85)

Mipango ya arusi ya Mwanakupona ilikuwa ikiendelea huku babake, Fumo Liyongo akiwa amefungiwa ngomeni. Katika kikao kilichopanga arusi, viongozi mbalimbali walitoa maoni yao. Osman Ali Kidhabi alipendekeza Fumo Liyongo kuruhusiwa kushiriki arusi ya bintiye akiwa ndani ya ngome ili asije akatoroka kudhihirisha ukatili wa uongozi dhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari. Pendekezo hili liliwashangaza Mfalme Daudi Mringwari na Mwanalemba hivyo arusi ilifanyika nje ya lango la ngome kama alivyopendekeza Osman Ali Kidhabi.

Usimulizi penyezi umejitokeza katika kifungu kifuatacho:

Napendekeza ya kwamba wachimba kaburi wapelekwe huko mwili ulikopatikana, leoleo, wakamchimbie kaburi chapuchapu, wamzike. Kisha Waziri wa Sheria aonane na jamaa za marehemu, awaambie jamaa yao alipata safari nyingine baada ya ile yetu ya Misri. (Siri Sirini 2 2014:116)

Msimulizi alipendekeza mwili wa Mfawidhi Kijumwa Mfaume kuzikwa mahali ulipopatikana. Alifafanua kuwa baada ya kuzikwa, Waziri wa Sheria angeonana na jamaa za marehemu na kuwadanganya jamaa zake kwamba alipata safari nyingine kuonyesha ukatili wa msimulizi. Mfawidhi Kijumwa Mfaume aliuawa kinyama na mwili wake kupatikana kichakani kudhihirisha unyama na usaliti wa uongozi. Kombo alionyeshwa mwili huo na mchungaji jirani yake na kuwajulisha wafuasi wake kudhihirisha mshikamano wa wafuasi wa Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Waziri wa Sheria alionyeshwa mwili huo naye akamjulisha Mfalme Daudi Mringwari katika kikao. Hata hivyo, pendekezo la Waziri Mkuu lilipingwa na Kadhi Mkuu, Imamu na Naibu Waziri Mkuu.

Usimulizi penyezi umetumika hivi:

Napendekeza wakamatwe.. watiwe mbaroni.. wawekwe korokoroni! (Siri Sirini 2 2014:154)

Msimulizi ambaye ni Waziri Mkuu alitoa pendekezo hilo kuhusu waliomuua Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Waziri wa Sheria alifanya uchunguzi kuhusiana na mauaji ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume na kumpelekea Mfalme Daudi Mringwari vidokezo vilivyoonyesha kuwa Kibwana Mwengo Bashee, Dhaidho, Shalo, Kombo na Osman Ali Kidhabi walionekana na Mfawidhi Kijumwa Mfaume mara ya mwisho. Ndipo Waziri Mkuu alipendekeza wakamatwe na wawekwe korokoroni. Malkia Mwanalibasi

alimaka kwa kuwa alimuona Osman Ali Kidhabi bila hatia kuonyesha ufiisadi wa Malkia Mwanalibasi hivyo, aliwashangaza Waziri wa Sheria na Mfalme Daudi Mringwari.

Usimulizi penyezi unajitokeza hapa:

Mimi napendekeza tupige mbiu ya mgambo, tuwaite wapiganaji wote, tuwaambie jemadari wao ameuawa. Uamuzi wa ni nini kitakachofanywa utapatikana katika kikao hicho. (Siri Sirini 3 2014:263)

Anayesimulia, Sheikh Omar Soba alipendekeza wapige mbiu ya mgambo kuwaita wapiganaji baada ya Kibwana Mwengo Bashee kumjulisha juu ya mauaji ya Fumo Liyongo na Mwinyi huko Shanga. Alipopiga mbiu ya mgambo, wapiganaji wa Ozi walikusanyika huku wakiimba nyimbo za vita kudhihirisha mshikamano wa wapiganaji wa Ozi na Fumo Liyongo. Sheikh Omar Soba alimkaribisha Kibwana Mwengo Bashee kuwaeleza kilichotokea. Baada ya maelezo, waliamua kulipiza kisasi. Waliingia vitani na Washanga huku wakiongozwa na Abanoye na Kibwana Mwengo Bashee. Kwa hivyo, vita vilimuondoa Mfalme Daudi Mringwari mamlakani.

Menzwa Biryā alitumia usimulizi penyezi kwa kupendekeza kwa wenzake wayatatue matatizo ya ubaguzi nchini kwanza. Anasema hivi:

Kwanza tuyatatue haya matatizo ya ubaguzi nchini mwetu. (Siri Sirini 3 2014:196)

Msimulizi alitoa pendekezo hili katika kikao ambacho Fumo Liyongo alikutana msituni na wafuasi wake alipoingia Shanga kubainisha ubaguzi uliokuwa katika nchi ya Shanga. Pendekezo hili liliungwa mkono na Kibwana Mwengo Bashee asilimia mia. Wafuasi hawa hawakuona uwezekano wa kufaulu kwa mapambano ya Shanga na Uswahilini kote. Kwa hivyo, Fumo Liyongo alitaka kujua waliomuunga mkono Suleiman Mringwari.

Usimulizi penyezi umetumiwa na Dhaidho anaposema:

Napendekeza wapelekwe uhamishoni! (Siri Sirini 3 2014:300)

Msimulizi anatoa pendekezo kuhusu Daudi Mringwari na mkewe Mwanalibasi. Anapendekeza kuhamishwa kwao baada ya kung'atulia uongozini kudhihirisha

mapinduzi na ujenzi wa jamii mpya. Daudi Mringwari aliondolewa mamlakani Waozi walipolipiza kisasi na kuvamia nchi ya Shanga wakiongozwa na Abanoye na Kibwana Mwengo Bashee. Tukio hili lilitendeka baada ya Fumo Liyongo kuuliwa kinyama na Suleiman Mringwari.

Kwa hivyo, usimulizi penyezi umefanikisha uelewaji wa matukio mbalimbali yaliyosimuliwa katika riwaya hii na wasimulizi mbalimbali kama vile: Suleiman Mringwari juu ya kubadilisha jinsi ya kuitana, Osman Ali Kidhabi kuhusu mahali ambapo arusi ya Mwanakupona ingefanyiwa, Waziri Mkuu juu ya kuzikwa kwa Mfawidhi Kijumwa Mfaume na kukamatwa kwa waliomuua, mwito wa wapiganaji wa Ozi na Omar Soba, Dhaidho kumhusu Daudi Mringwari na Menzwa Biryaa juu ya utatuzi wa suala la ubaguzi.

4.5 Usimulizi tautolojia

Usimulizi tautolojia ni mbinu ya usimulizi inayotumiwa kuelezea maneno au mawazo ya uziada katika usemi au maandishi fulani (Wamitila, 2003). Tautolojia huchekecha na huonyesha hamu ya mzungumzaji. Tautolojia iliyo na sifa ya uziada ni mbinu ya usimulizi iliyotumika kwa mapana katika riwaya hii kwa nia ya kutilia uzito maneno kwa mfano:

Hivi ni kusema ni makosa wewe Dhabina, Imamu hapa Naibu wa Waziri Mkuu, na mimi mwenyewe binafsi kuwa katika ngazi za uongozi? Mfawidhi alisaili. (Siri Sirini 1 2013:184)

Msimulizi alitumia maneno ‘mimi mwenyewe binafsi’ kutilia mkazo kuwa hakukuwa na makosa yake kuwa kiongozi. Tukio lilitokea kwenye kikao kilichoitishwa na Mfalme Daudi Mringwari katika gongwa lake. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alilaumiwa kwa kukutana na Kibwana Mwengo Bashee na wafuasi wake. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alijitetea na kusesitiza kuwa aliwashauri wafuasi wake kujitenga na mapambano ya mabavu dhahirisho la mabadiliko. Kwa hivyo, Mfalme Daudi Mringwari alimkosoa kwa kukutana nao bila kutafuta ushauri kutoka kwa wakubwa wake.

Usimulizi tautolojia mwingine ni:

Kwa jinsi hiyo, huu mwito ulikuwa unaashiria mtihani wa aina yake, ambapo kwamba kila mwenye kualikwa angeelekezewa darubini

kumulika yeye tu, binafsi yake, ili uwezo wake uonekane dhahiri.
(Siri Sirini 1 2013:169)

Mwandishi anasema ni ‘yeye tu binafsi yake’ akimrejelea Mfalme Daudi Mringwari ambaye aliitisha kikao katika gongwa lake kilichohudhuriwa na viongozi wote wa Shanga. Mada ilikuwa kutathmini mipango ya arusi ya Mwanakupona na uwajibikaji wa kila kiongozi kuashiria kutumia maneno hayo ya kusisitiza kudhihirisha umuhimu wa sherehe ya arusi. Viongozi wote waliokuwa pale hawangeweza kutabiri matokeo ya mazungumzo hayo hivyo kupatwa na hofu.

Usimulizi tautolojia umetumika hivi:

Wajuaje? Aliuliza mwanamfaume. Mimi binafsi yangu sikumuona hapo. (Siri Sirini 2 2014:64)

Osman Ali Kidhabi aliyatamka maneno haya katika kikao alichoitisha Mfalme Daudi Mfalme kuhusiana na kupotea kwa Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Osman Ali Kidhabi alitumia maneno ‘mimi binafsi yangu’ kusisitiza jinsi hakumuona Mfawidhi Kijumwa Mfaume katika baraza dhahirisho la uwongo wa Osman Ali Kidhabi hivyo kuwashangaza wote waliokuwepo.

‘Yeye mwenyewe binafsi yake’ ni Usimulizi wa tautolojia uliojitokeza katika kifungu hiki:

Kila mmoja hakuwa na hakika kama angeweza kukikabili yeye mwenyewe binafsi yake bila kulemewa. (Siri Sirini 2 2014:139)

Mwandishi alitumia uziada huu kuonyesha athari iliyowapata Mfalme Daudi Mringwari, Malkia Mwanalibasi na mwanamfaume kuhusiana na kifo cha Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Yalikuwa mauaji ya kikatili. Kwa hivyo, walikutana wote watatu kwenye sebule ya gongwa lao kila mmoja akitaafuta kumwegemea mwenziwe ilimradi ausahau mzigo huo waliouhisi mzito mno.

Usimulizi tautolojia umetumika hivi:

Ama sawasawa ni hivi afanyavyo huyu Daudi Mringwari bila kuona haya; yaani kuwatumia wanati kujitayarisha yeye tu mwenyewe binafsi yake? (Siri Sirini 3 2014:286)

Abanoye aliwaza kuhusu uongozi wa Shanga baada ya kuondolewa mamlakani kwa Daudi Mringwari thibitisho la mapinduzi. Abanoye aliajabia jinsi Daudi Mringwari alivyojilimbikizia mali ya wananchi kwa maslahi yake kuonyesha uongozi dhalimu. Abanoye alilinganisha uongozi wa babake Omar Soba katika nchi ya Ozi na ule wa Daudi Mringwari kumfanya ashangae.

‘Mimi mwenyewe binafsi yangu’ ni usimulizi tautolojia uliotumika katika usimulizi huu:

Leo hii Shanga yetu haina tofauti kabisa na nchi aliyoitawala mfalme dhalimu wa kale, Anzuruni, ambaye kadhia yake inasimuliwa kikamilifu katika shairi la Siri Sirini; shairi ambalo mimi mwenyewe binafsi yangu nimebahatika kulisoma. (Siri Sirini 3 2014:194)

Muhamad Juma Obo alitumia uziada huu katika kikao alichoitisha Fumo Liyongo huko msituni, Shanga. Msimulizi anasisitiza kulisoma shairi linalozungumzia dhuluma za Mfalme Anzuruni kuonyesha dhuluma katika uongozi. Wafuasi wake Fumo Liyongo walihudhuria kikao husika kujadili mikakati ya kuikomboa nchi yao ya Shanga. Muhamad Juma Obo alitaja dhuluma kuwa tatizo kubwa katika taifa dhihirisho la mabadiliko. Kwa hivyo, wote walikubaliana kupiga vita udhalimu katika nchi ya Shanga.

Usimulizi tautolojia unajitokeza ifuatavyo:

Akasema ya Mfawidhi hayajui vizuri, lakini kwa vile amewekwa mkumbo mmoja na mtu ambaye yeye binafsi anajua hawezi kamwe kuingia hatiani, yaani mwana wao wa pekee, hilo tosha lilifanya shutuma dhidi ya Mfawidhi kuwa batili aidha. (Siri Sirini 1 2013:368)

Mwandishi alitumia tautolojia ‘yeye binafsi’ katika mawazo ya Malkia Mwanalibasi. Tukio lilitokea baada ya wajumbe wanne wa Shanga kurudi Shanga kutoka Misri dhihirisho la uhusiano mwema baina ya mataifa. Osman Ali Kidhabu alimweleza Mfalme Daudi Mringwari mambo ya uongo kumhusu mwanamfaume na Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Mwanalibasi aliwaza kama mumewe angeweza kumtilia mwanawe shaka. Malkia Mwanalibasi alimshawishi Mfalme Daudi Mringwari kuzungumza na mwanawe kwanza ili wajue ukweli. Kwa hivyo, Mfalme Daudi Mringwari alikubali ushauri wa Malkia Mwanalibasi na kuwapa wajumbe fursa ya kueleza kilichojiri Misri.

Usimulizi tautolojia ‘wao wenyewe wawili’ unaonekana katika kifungu kifuatacho:

Kila mtu yalimshangaza hayo. Hakuna anayejua wivu huo ulianza lini, bali tu wao wenyewe wawili. (Siri Sirini 2 2014:148)

Mwanananga alitumia uziada huu kwa Fumo Liyongo nchini Ozi. Mwanananga alimtembelea mumewe Ozi na kumjulisha kuhusu mauaji ya kinyama ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume kuonyesha dhuluma katika uongozi. Mwanananga alimwambia Fumo Liyongo kuwa Mwanalemba alilia sana kusabababisha mumewe kumshuku kuonyesha kutoaminiana katika ndoa. Mwanananga alisisitiza kuwa wivu wa Waziri Mkuu kwa Mfawidhi Kijumwa Mfaume waliujua wao wawili hivyo Fumo Liyongo kujuta hakumuua Osman Ali Kidhabi alipopata nafasi. Usimulizi Tautolojia umetumika katika kifungu hiki:

Nasema hili ni janga kubwa kwangu mimi binafsi, kwenu nyinyi wazazi wangu, na kwa taifa zima la Shanga kwa jumla! (Siri Sirini 2 2014:143)

Suleiman Mringwari akirejelea kifo cha Mfawidhi Kijumwa Mfaume, alisisitiza kwamba kifo hicho kilikuwa janga kubwa kwake, kwa wazazi wake na kwa nchi ya Shanga. Osman Ali Kidhabi alilaumiwa kwa mauaji hayo. Mazungumzo haya yalikuwa baina ya Suleiman Mringwari na wazazi wake. Suleiman Mringwari alimshauri babake kutokubali makosa kwa kuwa mtawala haombi msamaha kuonyesha uongozi dhalimu. Suleiman Mringwari alimwambia babake kuhusu uongozi wa Khalikzanda, jinsi alimuua nduguye kwa sababu ya urithi dhihirisho la tamaa katika uongozi. Kwa hivyo, Mfalme Daudi Mringwari alizingatia wosia wa mwanawe.

Usimulizi tautolojia unapatikana kama inavyosimuliwa hivi:

Ningetaka tu tafutie jinsi mahsusi ya kuutatia. Tafutie utatuzi, maanake. Wewe mwenyewe binafsi yako, au umetumwa? (Siri Sirini 1 2013:55)

Mwanaziza aliyatumia maneno ‘wewe mwenyewe binafsi yako’ kwa Mwanalemba katika kasri la pili ya Mfalme. Fumo Liyongo alifungwa kwa tuhuma za uhaini. Mamake Mwanaziza na mkewe Mwanananga walikasirika na kuhamia huko. Mfalme Daudi Mringwari alimtuma Mwanalemba ili waweze kupata suluhu ya huo mgogoro kuonyesha migogoro ya familia. Ndipo Mwanaziza alitumia tautolojia hiyo kutaka kujua kama Mwanalemba alijituma au alitumwa. Mwanalemba alikubali kutumwa

dhihirisho la utiifu. Mwanaziza alimwonyesha Mwanalemba jinsi nduguye alikuwa kiongozi dhalimu na kumfananisha na Mfalme Anzuruni anayesimuliwa katika hadithi ya ‘Siri Sirini’ hivyo kumshtua Mwanalemba na kuanza kumchunguza nduguye.

Usimulizi tautolojia ‘yeye mwenyewe binafsi’ umetumika hapa:

Nimjuavyo mimi, yeye mwenyewe binafsi atahakikisha ya kwamba urafiki huo unanoga na kuzidi kunawiri kila uchao. (Siri Sirini 3 2014:321)

Kibwana Mwengo Bashee aliyatumia maneno hayo katika kikao kilichofanya uteuzi wa viongozi wapya wa Shanga. Kikao kilitoa pendekezo kwamba Abanoye arudi kwao Ozi. Walitambua kuwa Abanoye akirudi Ozi angeweza kuyaunganisha mataifa ya Ozi na Shanga na kuwa nchi moja yenye nguvu kuonyesha umoja wa kimataifa.

Uchunguzi umebaini kuwa msimulizi anaweza kutumia maneno yaliyo na sifa ya uziada kwa lengo la kutilia uzito maneno au mawazo. Usimulizi tautolojia umefanikisha usimulizi wa matukio mbalimbali katika riwaya hii kwa kuyasisitiza.

4.6 Usimulizi wa motifu ya safari

Motifu ni nguzo muhimu ya kiusimulizi inayojitokeza katika kazi za kifasihi (Abrams, 1999). Massoud (2013) anafafanua motifu kwa kueleza kuwa ni kipengele radidi cha kifani kinachotumiwa na wasanii katika kazi zao ili kutoa ujumbe fulani. Mifano ya motifu za kifasihi ni kama vile: Safari, msako, mtoto kigego, mwanamke shawishi, mzungu mweusi, mtoto wa ajabu, zimwi mla watu na mwali aliyekataa kuolewa. Motifu ya safari huwa na msingi wa kujisaka pale ambapo wanaosafiri hukumbana na matatizo mbalimbali. Riwaya nyingi huwa na motifu ya safari na msako kama vile riwaya ya *Siku Njema* (Walibora, 1996) ambapo maisha ya msimulizi, Kongowea Mswahili yu safarini ya kujitafuta, msako alioachiwa na mamake wa kumsaka baba aliyemzaa. Motifu ya safari ni sitiari inayojenga riwaya trilojia ya *Siri Sirini*. Safari mbalimbali katika riwaya teule zinaonyesha mfuatano wa mambo katika kutekeleza jukumu fulani. Kwa mfano:

Kijakazi Sada alifunga safari ya kwenda ngomeni kumpelekea Fumo Liyongo chakula. Kijakazi Sada aliaminika sana miongoni mwa wafanyikazi wengine kutekeleza wajibu huo kuonyesha uaminifu na uwajibikaji wa Sada. Katika safari hii, Mwananiga

alimtuma Kijakazi Sada chakula na waraka kumpelekea Fumo Liyongo. Waraka ulikuwa ‘Utenzi wa Mwanakupona’. Mwanakupona alimkabidhi mamake huo utenzi alipomtembelea Lamu. Alitaka mama au baba yake kuughani utenzi huo siku ya arusi yake. Mwanananga hangemtembelea bwanake ngomeni na ndiyo sababu alimtuma Kijakazi Sada kudhihirisha ukatili wa utawala. Utenzi haukumfikia Fumo Liyongo kwa sababu ulichukuliwa na askari-ngome kama alivyomjulisha Sada katika mazungumzo yao. Fumo Liyongo alikanganyika vipi Mwanakupona akawa msanii wa mashairi. Alimuomba Kijakazi Sada siku nyingine kumpelekea aina mbili ya chakula na kumfunza wimbo ambao angewaimbia mamake Mwanaziza na mkewe Mwanananga hadi wauelewe. Wimbo ni huu:

Kijakazi Saada nakutuma tumwa tumika
Kamwambie mama yu muinga hajalimuka
Afanye mkatekati tupa kuweka
Nikereze pingu minyo’o ikinyemuka
Niparage kuta na madari kiyakeuka
Niuwe rijali pindi wakiwana kuteka
Ningie ondoni ninyeppee ja mwana nyoka
Ningie mwituni ningurume ja simba buka
Nali mtu pweke nimeziye katika nyika
Si nduu si mbasi nimeziye kukupuka
Nduu ali mama awasiwe kinda.

Siri sirini 1 (2013:158)

Msimulizi anaomba tupa ili aweze kukata minyororo iliyomfunga na kuweza kutorokea msituni kuonyesha usaliti na unyanyasaji uliokuwa ngomeni. Ujumbe aliomtuma Fumo Liyongo kwa njia ya ushairi unaonyesha ushujaa wake wa kiakili na uelewa wa mamake na mkewe wa ushairi, uaminifu na uwajibikaji wa Kijakazi Sada. Kwa hivyo, safari ya Kijakazi Sada ilimpa Fumo Liyongo uhuru.

Mwanananga alifunga safari kwenda Lamu kama anavyoeleza msimulizi:

...baada ya Mwanananga kurudi salama salimini kutoka Lamu. Huko alikuwa amepelekwa na mambo mawili: kuondoa shaka juu ya msimamo wa Waamu kuhusu arusi ya binti yake na pili, kufanya mazungumzo ya mwisho na wanawe, Mwanakupona na Bauri. Pia, aliweza kuichukua fursa hiyo kuwajulia hali watoto wanne wa wafi yake, Mwanalemba, ambao walikuwa huko huko Lamu wakisoma chuo kimoja na hao wanawe. (Siri Sirini 1 2013:139)

Usimulizi unaeleza kwamba Mwanananga aliwatembelea wanawe Lamu kwa lengo la kuhakikisha arusi ya bintiye imefanikiwa kuonyesha uwajibikaji wa mama mzazi.

Aidha, kuwajulia hali watoto wa wifii yake kunadhihirisha mshikamano wa familia ya Mwanalemba na Fumo Liyongo. Watoto wao kusomea Lamu kunaonyesha umuhimu wa elimu na mabadiliko yanayoambatana na elimu. Mwanakupona alimkabidhi mamake utenzi alioutunga ili uweze kughaniwa siku ya arusi yake. Alipendekeza mamake au babake kuughani. Mazungumzo ya mama na mwana yalimsababisha Mwananinga kubadili misimamo yake ya awali kuhusu bintiye. Kwa hivyo, Mwananinga aliona Mwanakupona alikuwa amekomaa kimwili, kiakili na alikuwa tayari kuolewa na bwana aliyekuwa na chuo cha kwanza kufafanua wazi mabadiliko ya Mwanakupona juu ya masuala mbalimbali.

Safari ilifanywa na Mwanalemba kwenda kusini katika kasri ya pili ya Mfalme Daudi Mringwari. Mwanalemba alitumwa na kakake kuwapelekea Mwananinga na Mwanaziza ujumbe. Tukio hili lilitokea baada ya Fumo Liyongo kufungwa korokoroni kwa kosa la uhaini. Mwananinga na Mwanaziza walikasirika na kuhamia kusini. Katika safari hii, Mwanalemba alisindikizwa na watumishi waliomhudumia siku zote huku akichapuka chapuchapu ili kudumisha cheo chake kuonyesha utabaka. Mwendu wake wa kasi haukumnyima nafasi ya kufurahia mandhari ya shamba. Mwanalemba alishangaa sababu za waungwana kusongamana mjini, ilhali mashambani watu walikuwa hawapambanii nafasi ya makao kudhihirisha mgongano wa mifumo ya mjini na shamba.

Mwanalemba alifurahia makaribisho ya jamaa wake, kisha akawapa ujumbe wa Mfalme Daudi Mringwari katika kifungu hiki:

Kilichonileta ni mgogoro ulioikumba aila yetu. Ningetaka tuutafutie jinsi ya kuutatua. Tuutafutie utatuzi, maanake... Ninaamini kabisa, ndani ya moyo wangu, kwamba mgogoro huu unaweza kutatuliwa kwa njia ya mazungumzo. (Siri Sirini 1 2013:55)

Msimulizi anaeleza kwamba familia yao ilikumbwa na mgogoro uliosababishwa na kufungwa ngomeni kwa mpendwa wao Fumo Liyongo. Mfalme Daudi Mringwari alitaka wafanye mazungumzo ili kupata suluhu kudhihirisha jinsi ukatili unavyoweza kuleta mgogoro baina ya jamaa, lakini mazungumzo yanaweza kuleta upatanisho. Mwanaziza alimuuliza Mwanalemba kama aliwahi kusoma hadithi ya Mfalme Anzuruni. Mwanalemba alikubali kuisoma. Alijibu:

Nishawahi.. Siri L asirar... Anzuruni ni Mfalme dhalimu.
Anawadhulumu raia zake. Anatomia hirizi na imani za kishetani
kuwazindika na kuwagubika watu wake. (Siri Sirini 1 2013:59)

Msimulizi anafafanua udhalimu wa Mfalme Anzuruni anayesomwa katika hadithi ya ‘Siri Sirini’ kuonyesha ukatili wa viongozi. Mwanaziza aliufananisha uongozi wa Mfalme Anzuruni na uongozi wa Mfalme Daudi Mringwari. Msimulizi anaeleza bayana kwamba nguvu za kishetani zilitumika kuwatawala raia kudhihirisha imani ya ushirikina katika uongozi.

Wajumbe wa Shanga: Mfawidhi Kijumwa Mfaume, Suleiman Mringwari, Waziri Mkuu na Osman Ali Kidhabi walisafiri nchini Misri. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alikuwa kiongozi wao kwa sababu alisomea nchini Misri, alikuwa na uzoefu wa matembezi na ujuzi wa lugha ya Kiarabu kudhihirisha kusoma kwake. Nchi ya Misri iligharamia kila kitu kama maelezo yanavyosema:

Safari ya kuelekea Misri ilikuwa tofauti katika kila namna. Jambo la kwanza, utawala wa Shanga ulibahatika pakubwa mno kwa vile watawala wa Misri waliamua kugharamia kila kitu ilimradi tu waanzishe na kudumisha uhusiano bora na wenye manufaa yao na wenzao wa Shanga. (Siri Sirini 1 2013:244)

Msimulizi anafahamisha kuwa safari hii ilikuwa ya kudumisha uhusiano mwema kudhihirisha suala la mahusiano mema kati ya nchi husika. Mfalme Daudi Mringwari aliwatuma wajumbe hao ili nchi yake na ile ya Misri zipate kunufaika. Wageni na wenyeji walikutana katika bustani ya kifalme. Baada ya vitangulizi, Mfawidhi Kijumwa Mfaume alipatiwa nafasi ya kuzungumza kwa niaba ya wenziwe. Hotuba yake ililenga: Maendeleo na ustaarabu nchini Misri, watawala, dini na kuneemesha uhusiano baina ya nchi hizo mbili kuonyesha maendeleo, dini na mahusiano. Baada ya hotuba Mfawidhi Kijumwa Mfaume alishangiliwa na kupigiwa makofi na watu wote jukwaani huku wakamzingira kama ndiye Mfalme wa Shanga. Waziri Mkuu na Osman Ali Kidhabi walipuuzwa. Suleiman Mringwari alibebwa juujuu na kudekezwa wazi. Waziri Mkuu na Osman Ali Kidhabi walimshangilia Mfawidhi Kijumwa Mfaume kwa nguvu kama ndio mwanzo wamjue kuonyesha wivu. Kwa hivyo, kwa upande mwingine Waziri Mkuu na Osman Ali walijiona kuwa dhaifu.

Osman Ali Kidhabi alifunga safari ya kwenda nchini Ozi kumtembelea Fumo Liyongo. Alikuwa ametumwa na Malkia Mwanalibasi na Waziri Mkuu kwa lengo la kumwangamiza Fumo Liyongo kuonyesha ukatili wa viongozi hawa. Osman Ali Kidhabi alitumia mchezo wa kikoa cha makoma ili aweze kumuua Fumo Liyongo kama anavyomweleza:

Wapiganaji wako wamenikaribisha kula kikoa cha makoma pamoja nao; nikawatakabalia. Hata hivyo, nimewaaambia kwa vile mimi ni mgeni mno hapa, sitoki ila tu wewe ukiandamana nami, mwenyeji wangu. (Siri Sirini 2 2014:18)

Msimulizi anafanya hila ili aweze kumwangamiza Fumo Liyongo. Usimulizi unafafanua kwamba Fumo Liyongo alielewa mpango wa Osman Ali Kidhabi na kupendekeza zamu yake iwe ya mwisho kuonyesha ushujaa wa akili wa Fumo Liyongo. Zamu ya Fumo Liyongo ilipofika aliutafuta mti alioutaka na akabwaga makoma yote mabivu kwa kutumia mshale bila kuupanda kudhihirisha ushujaa wake wa kimwili. Wapiganaji walikusanya makoma na kwenda zao huku wakimwacha nyuma Fumo Liyongo na mgeni wake, Osman Ali Kidhabi. Fumo Liyongo alisisitiza kujua kutoka kwake Osman Ali Kidhabi aliyekuwa amemtuma Ozi kumwangamiza. Anasisitiza:

Niambie ni nani aliyekutuma kuniua, la sivyo kichwa chako kiovu ni halali yangu! ...Ni mtu msiyekuwa na uhusiano wa damu. (Siri Sirini 2 2014:22)

Msimulizi alitaka kujua aliyemtuma Kidhabi kumuulia Ozi. Fumo Liyongo akimkaba roho, akajaribu kujinasua lakini akashindwa. Alitepetea na kupweteka huku akitupatupa mateke kuonyesha ushujaa wa kimwili, kiakili na kivita wa Fumo Liyongo. Kwa hivyo, Osman Ali Kidhabi alimdokezea Fumo Liyongo mtu aliyemtuma kumuua.

Safari nyingine ilifanywa na Suleiman Mringwari kwenda Ozi kuonana na Fumo Liyongo. Suleiman Mringwari alitumwa Ozi na babake Mfalme Daudi Mringwari, Malkia Mwanalibasi, Waziri Mkuu na Waziri wa Sheria kwa nia ya kumshawishi Fumo Liyongo kurudi Shanga ili waweze kumwangamiza kuonyesha ushirikiano katika utekelezaji wa mauaji. Katika safari hii, Suleiman Mringwari alifanikiwa kumshawishi Fumo Liyongo kurudi Shanga kudhihirisha udanganyifu wa Suleiman Mringwari. Suleiman Mringwari alimsimulia Fumo Liyongo mafanikio ya safari ya Misri, tukio lililoonyesha mabadiliko yaliyomshangaza Fumo Liyongo.

Fumo Liyongo alimwuliza Suleiman Mringwari kuwa na nguvu za kiakili ili kuweza kupigana na adui. Fumo Liyongo alimweleza jinsi angeweza kutumia udhaifu wa mtu mwenye nguvu na kumuua. Fumo Liyongo alimfichulia siri ya udhaifu wa kitovu hivi:

Huhitaji mgunzu wa almasi kuchomea kitovu cha mtu yeyote yule.
Hata mgunzu wa shaba au chuma watosha. Kitovu kina uwazi ndani hakina misuli wala nyama tepetepe. Kama nilivyokueleza, hiyo ni njia wazi inayoelekea moja kwa moja utumboni. (Siri Sirini 3 2014:83)

Msimulizi anabainisha njia rahisi ya kuliua jitu. Si kwa nguvu ya mwili lakini kwa ushujaa wa akili. Tukio hili lilimjulisha Suleiman Mringwari namna ya kumwangamiza Fumo Liyongo. Mwandishi anatoa maelezo kwamba baada ya Suleiman Mringwari kufahamu siri hii, aliharakisha kuondoka Ozi huku akimwacha Fumo Liyongo akijitayarisha kurudi Shanga kuonyesha usaliti. Fumo Liyongo alirudi Shanga akiandamana na mwanawe Mwinyi kudhihirisha suala la malezi mema. Suleiman Mringwari alimuua Fumo Liyongo kwa kumdunga kitovuni kwa sindano ya shaba thibitisho la usaliti na ukatili wa Suleiman Mringwari baada ya Kidhabi kushindwa kumuua kwa hila ya mchezo wa kikoa. Mauaji haya yalisababisha vita baina ya Ozi na Shanga. Mfalme Daudi Mringwari aliondolewa mamlakani kuonyesha ujenzi wa jamii mpya chini ya uongozi wa Bauri wa Liyongo.

Malkia wa Sheba alifunga safari kama inavyoelezwa:

Alisafiri safari ndefu wee hadi kokolo, mbali huko Filistina!
Akaendajirahisisha kwa Mfalme wa huko siku hizo, Nabii Suleiman bin Daudi. Akarudi nyumbani na ujauzito haramu wa nje ya ndoa, bila hata aibu! Akajizalia mwanawe wa kiume ambaye hakutambuliwa na babake; akamwita Menelik. Huyu ndiye aliyeanzisha ukoo wa utawala wa Uhabeshi wenye mizizi yake Filistina, ambao ndio ulioko uongozini hadi wa leo! (Siri Sirini 1 2013:230)

Msimulizi anaeleza kwamba Malkia wa Sheba aliwadharau wanaume hivyo kukosa wa kumuoa kuonyesha changamoto za matabaka juu ya suala nzima la ndoa na urithi. Dhabina alimlinganisha Malkia wa Sheba na Mwanakupona aliyetunga shairi lililokuwa na ujumbe wa mapinduzi. Mfalme Daudi Mringwari aliamua ‘Utenzi wa Mwanakupona’ kusomwa na watu wote waliojua kufasiri mashairi na ukionekana muovu wajue la kufanya kuonyesha mabadiliko katika elimu na dini. Kwa hivyo,

Mfalme Daudi Mringwari alimtuma Mwanalemba kwa Mwanaziza na Mwananinga kuomba maoni yao kuhusu utenzi husika.

Mwananinga na Kadhi Mkuu walisafiri Ozi kumuona Fumo Liyongo. Baada ya kuvunja ngome, Fumo Liyongo alitorokea nchi ya Ozi kama mkimbizi kutangaza ukatili wa Mfalme Daudi Mringwari. Kadhi Mkuu na Mwananinga walikuwa wametumwa na Mfalme Daudi Mringwari ili kuwapatanisha kudhihirisha msamaha. Fumo Liyongo aliogopa akirudi Shanga angekamatwa tena lakini Kadhi Mkuu alimhakikishia usalama wake. Fumo Liyongo alimfahamisha Mwananinga nia yake ya kumuoa Abanoye katika usimulizi huu:

Nataka kumuoa Abanoye... sasa unadhani mimi nina moyo wa jiwe, sisikii vibaya?.Chozi la kushoto likamtoka Mwananinga. (Siri Sirini 1 2013:338-339)

Usimulizi unajulisha kwamba Fumo Liyongo alinua kumuoa mke wa pili, Abanoye, ombi ambalo lilimumiza moyo Mwananinga na kujihisi kusalitika. Fumo Liyongo alimpa Mwananinga sababu za kutaka kumuoa Abanoye, ili ampunguzie Abanoye dhiki kwa mapenzi aliyokuwa nayo kwake kuonyesha upweke. Mwananinga alikasirika na kuamua kurudi Shanga kudhihirisha wivu wa wanawake katika ndoa. Hata hivyo, kabla ya kuondoka, Mwananinga alimwandikia Fumo Liyongo barua akimkubalia kumuoa Abanoye kwa masharti makali aliompa.

Fumo Liyongo alisafiri nchini Shanga baada ya ushawishi wa Suleiman Mringwari. Aliandamana na mwanawe Mwinyi kama usimulizi unavyodokeza:

Liyongo alielekea mtoni akiandamwa na mwanawe wa kiume... hakushindikizwa na mtu mwingine yeyote ghairi ya Mzee Omar Soba. (Siri Sirini 3 2014:113)

Msimulizi anafahamisha suala la malezi mema. Fumo Liyongo aliandamana na mwanawe wa kupanga, Mwinyi huku Omar Soba akithibitisha mapenzi kwa kuhakikisha walivuka mto salama salmini. Fumo Liyongo na Mwinyi walikuwa wamebeba zana za kivita na vyakula. Mwinyi alipolemewa na mzigo Fumo Liyongo alikusanya vitu vyote alivyompagaza mtoto na kuzibeba kuthibitisha nguvu za kimwili. Safari ilikuwa na changamoto nyingi kama vile kupambana na chatu aliyeogofya kwa kuwa haikuwa rahisi kubuni mkakati ufaao wa kupambana naye. Fumo Liyongo alijua

kuwa chatu hutembea wawili wawili na kwamba hawagawani windo kuonyesha ujuzi. Fumo Liyongo alipambana na chatu na kumkatakata kwa msu huku akiketi na kukikanganua kichwa cha chatu kwa nguvu kilichokuwa bado kimemuuma mguu kuonyesha ushujaa wa mwili na akili. Fumo Liyongo alidhihirisha ushujaa wa kivita alipomweleza Mwinyi jinsi alivyopambana na wanyama wengi msituni na kuwaua.

Katika safari hii, Fumo Liyongo alimfunza Mwinyi mambo mengi kuhusu vyakula, dini, miti na manufaa yake kwa binadamu na mambo manne makuu: Kumjua Mungu, kuyajua mazingira, kuwajua jamaa, jamii, jirani na kujua haki ya mtu kudhihirisha ujuzi aliokuwa nao. Fumo Liyongo alifika Shanga na kuonana na mamake Mwanaziza na mkewe Mwananiga. Fumo Liyongo alifanya kikao na wafuasi wake huko msituni kuonyesha ushujaa wa mshikamano. Fumo Liyongo alikutana na Suleiman Mringwari huko msituni na kumuua kwa kumdunga kitovuni kwa sindano ya shaba kuthibitisha usaliti na ukatili wa mwanamfaume. Baada ya mazishi ya Fumo Liyongo, Kibwana Mwengo Bashee alienda Ozi na kumfahamisha Abanoye kuonyesha ushirikiano aliokuwa nao na Fumo Liyongo. Tukio hili lilisababisha vita baina ya Waozi na Washanga hivyo kuondolewa uongozini kwa mmabavu Daudi Mringwari na ujenzi wa jamii mpya ya Shanga.

Usimulizi wa motifu ya safari umewezesha kuona mawazo makuu yaliyolengwa na wasimulizi kama vile: Ushujaa wa kimwili, kiakili, kivita na mshikamano, ukatili, usaliti, malezi, mapenzi, mabadiliko, mauti na ujenzi wa jamii mpya. Usimulizi huu umehusiana na hatua za kuwajenga wahusika hivyo kufanikisha uelewa wa matukio mbalimbali katika riwaya hii.

4.7 Usimulizi wa nyimbo

Nyimbo ni utungo ulio na mdundo na mahadhi unaoweza kuimbika. Jamii nyingi za Kiafrika hutumia nyimbo katika shughuli zao (Ngure, 2003). Kwa mujibu wa Matei (2011) nyimbo hutambuliwa kwa: Hadhira inayotumbuizwa, muziki unaoimbwa kwa sauti na matumizi ya ala. Nyimbo hutumia lugha ya mkato inayoibua taswira na hisia fulani na hufungamana na muktadha fulani kama vile kazi, harusi, jandoni, siasa, vita, matanga na ibada (mtaje). Baadhi ya vifungu katika nyimbo hurudiwarudiwa huku nyimbo nyingi zikiandamana na uchezaji wa viungo. Nyimbo zinaweza kuwa mashairi

ambayo yanaimbwa kwa minajili ya kufanya kazi maalumu (Otieno, 2017). Nyimbo huimbwa na makundi ya watu ilhali ushairi hukaririwa au kughaniwa na mtu mmoja. Nyimbo ni muhimu katika usimulizi wa riwaya teule kwa sababu zinaonyesha hisia katika usimulizi na kueleza mambo ya siri baina ya wahusika kwa mfano Fumo Liyongo alimfunza Kijakazi Sada shairi lifuatalo:

Kijakazi Saada nakutuma tumwa tumika
Kamwambie mama yu muinga hajalimuka
Afanye mkate kati tupa kuweka
Nikereze pingu minyo'o ikinyemuka
Niparage kuta na madari kiyakeuka
Niuwe rijali pindi wakiwana kuteka
Ningie ondoni pindi ninyepepe ja mwana nyoka
Ningie mwituni ningurume ja simba buka
Nali mtu pweke nimeziye katika nyika
Si nduu si mbasi nimeziye kukupuka
Nduu ali mama awasiwe kinda.

Siri Sirini 1 (2013:158)

Tukio hili lilitokea ngomeni alipofungwa Fumo Liyongo kwa kosa la uhaini kuonyesha unyanyasaji wa uongozi dhalimu. Kijakazi Sada aliwajibika kumpelekea chakula au ujumbe kudhihirisha uaminifu. Mipango ya arusi ya bintiye Mwanakupona ilikuwa ikiendelea. Mwanakupona alitaka kuchangia ufanisi wa arusi yake hivyo kutunga utenzi. Alimpa mamake utenzi huo alipomtembelea Lamu na kupendekeza ughaniwe na baba au mamake. Mwanananga alimtuma Kijakazi Sada na utenzi huo kumpelekea Fumo Liyongo ngomeni. Askari ngome walimpokonya Sada utenzi. Kijakazi Sada alimwambia Fumo Liyongo kuhusu utenzi wa Mwanakupona thibitisho la ukatili wa akari-ngome. Fumo Liyongo alimfunza Kijakazi Sada wimbo na kumwuliza awaimbie mamake Mwanaziza na mkewe Mwanananga afikapo nyumbani hadi pale wangemudu kuuimba vizuri kuonyesha ushujaa wa akili. Maelezo ya wimbo huu ni kwamba Fumo Liyongo aliomba tupa ambayo angetumia kukata minyororo na kutorokea msituni. Fumo Liyongo alitumia tupa kukata minyororo na kutorokea nchi ya Ozi kudhihirisha mshikamano wa jamaa na marafiki siku ya arusi ya Mwanakupona.

Nyimbo zingine zilizoimbwa katika arusi ya Mwanakupona ni utumbuizo wa taarab. Utumbuizo wa taarabu uliwakusanya watu wote pahali pamoja mkabala wa lango la ngome. Taarab huimbwa katika sherehe rasmi na isiyo rasmi na zina mdundo wa beti na kila ubeti huwakilisha ujumbe maalumu. Miongoni mwa mambo yanayoangaziwa

katika taarab ni hadhi ya jamii, maadili, utamaduni na taswira za kijamii (Otieno, 2017). Watu waliohudhuria arusi walijua kwamba wakati wa kusikiliza falsafa ya Fumo Liyongo ulikuwa umefika kuonyesha umaarufu wa Fumo Liyongo katika ushairi. Aidha, watu walijizatiti kustaladhi mashindano makali ya majibizano baina ya Fumo Liyongo na washairi wengine wakinzani wake. Tukio hili liliwatia hamu ya kutaka kujua lile lingeshindaniwa. Malenga wengine kutoka maeneo nje ya Shanga walipewa nafasi ya kwanza kuwatumbuiza, kuwafurahisha na kuwaelimisha watu kudhihirisha umuhimu wa nyimbo katika jamii.

Fumo Liyongo aliwatumbuiza watu katika arusi ya Mwanakupona kwa shairi aliloliita ‘Waswifu wa Mwananiga’, alilolitunga na kuliimba hivi:

Mshairi alianza kuzisifu nywele za singa za mkewe;
akasifu kichwa kizima, kiungo baada ya kiungo,
penye midomo laini, macho malegevu, kope bainifu,
nyusi pembe za mwezi mchanga, kidevu mithili ya yai,
shingo ya upanga, akashuka chini, hatua kwa hatua, bila
kuruka kiungo hata kimoja...akapiga mzinga.

Siri sirini 1 (2013:198)

Maelezo haya yanadhihirisha mapenzi aliyokuwa nayo mwimbaji kwa mkewe, Mwananiga. Msimulizi alimsifu mkewe huku akitaja viungo vyote vya mwili wake. Msimulizi alitumia jazanda ya safina, nahodha na mzinga ili kuficha aibu kama asemavyo Otieno (2017) kwamba lugha hutumika katika mashairi kwa njia fiche. Fumo Liyongo aliwachekesha watu na ughani huo hivyo kufanikisha mradi wake.

Mwananiga aliwatumbuiza hadhira kwa wimbo. Mwananiga aliingia uwanjani wa nyimbo kwa mbwembe huku mumewe akimshika mkono imara kadri alivyoweza katika muktadha huo wa kubanwabanwa kuonyesha ukatili katika uongozi. Shairi lilikuwa la ngonjera, lenye kichwa: ‘Kisichoumbwa na Mungu’. Lilikuwa shairi mtindo wa majibizano, wahusika wakiwa mkufuu na mwanafuu. Fumo Liyongo alichukua nafasi ya mkufuu na Mwananiga akachukua nafasi ya mwanafuu. Shairi hilo liliwashtua watu kuanzia anwani hadi mwisho wa ughani. Walioghani walisisitiza kuwa kuna kitu kisichoumbwa na Mungu ambacho rangi yake ilikuwa nyeupe. Kila mmoja pale arusini aliamua Fumo Liyongo na mkewe pamoja na mtunzi walikuwa makafiri wakubwa kudhihirisha madharau katika imani ya dini. Kwa hivyo, watu walikasirika na kupendekeza Mwananiga atiwe ngomeni akampikie mumewe huko.

Fumo Liyongo alipewa nafasi nyingine ya kuimba kwa mara ya pili usiku ule. Alipoanza kughani watu wa Shanga walishangaa sana na wengine wakashikwa na uoga. Shairi aliloliteua ni lile lilimtia ndani ngomeni, ‘Takhmisa ya Liyongo’. Watu wengi wakawa hawakuwa na la kusema na walielekeza nyuso zao chini walingojea lolote ambalo lingetokea. Shairi lilikatizwa ghafla huku sauti kali ya lango likigongwa ikisikika. Lango lilianguka chini na Fumo Liyongo akatoka ndani ya ngome na kutoroka kuonyesha mshikamano wa familia ya Fumo Liyongo na wafuasi wake. Kwa hivyo, shairi hilo lilimpa Fumo Liyongo uhuru siku ya arusi ya bintiye, Mwanakupona.

Nyimbo ziliimbwa nchini Shanga na waandamanaji baada ya kukamatwa kwa Mwanananga kama inavyosimuliwa:

Shanga iliamkia fujo, vurumai, zahama! Maandamano yalizagaa kote, waandamanaji walivunja matawi ya miti wakayayumbishayumbisha juu ya vichwa vyao huku wakiimba nyimbo za kuwasifu viongozi wa ngazi za juu za taifa na kumsifu Fumo Liyongo. Nyimbo zingine zilimsifu marehemu Mfawidhi Kijumwa Mfaume na kupendekeza taasisi ya mahakama iliyopo ivunjiliwe mbali mara moja. Nyimbo zenye maudhui hii zilitoa agizo la kuanzishwa mahakama mpya ambayo itakayodumisha haki na kuhakikisha ya kwamba wale waliomuua Mfawidhi Kijumwa Mfaume pamoja na mabwana zao waliowatuma kufanya hivyo wote wamekamatwa na kuadhibiwa vikali! (Siri Sirini 2 2014:242)

Nyimbo hizi zinadhihirisha kutokuwepo kwa amani nchini Shanga kwa sababu ya maandamano. Washanga waliandamana kwa kukamatwa na kufungiwa korokoroni kwa Mwanananga kwa tuhuma za kuwa mtunzi wa ‘Siri Sirini’. Shairi hili liliukashifu uongozi dhalimu na kumsifu Mfawidhi Kijumwa Mfaume aliyeuliwa kinyama na uongozi katili. Nyimbo zilimsifu Fumo Liyongo aliyekuwa mkimbizi nchini Ozi baada ya kuvunja ngome na kujinyakulia uhuru. Wimbo mwingine uliamuru kuachiliwa kwa Mwanananga na waliomkamata kumuomba msamaha hadharani. Kwa hivyo, Mfalme Daudi Mringwari alifahamu maandamano hayo hayakuwa ya kawaida na aliandika barua ya kumwachilia Mwanananga.

Mwinyi aliubuni wimbo huu:

Safari ni mapambano, safari ni mapambano.
Na mapambano ni safari, mapambano ni safari.
Siri Sirini 3 (2014:151)

Msimulizi alikuwa katika muktadha wa safari. Mwinyi alikuwa safarini na babake Fumo Liyongo kutoka Ozi kurudi Shanga baada ya kushawishiwa na mwanamfaume. Mwinyi aliimba vizuri kwa urari sawa, mizani linganifu na uradidi mwanana kudhihirisha mapambano yanayoleta mabadiliko katika safari. Kwa hivyo, wimbo ulimsababisha Fumo Liyongo kujiuliza kimoyomoyo kama Mwinyi alikuwa Mwanakupona wa pili.

Mwanananga na Mwanaziza walimwimbua Fumo Liyongo mashairi ya kumbembeleza na kumtumbuiza ilimradi aachane na ukaidi wake. Matei (2011) anaeleza kuwa bembelezi hutumia lugha shawishi na huimbwa kwa mahadhi ya chini huku anayeimbiwa akionywa dhidi ya tabia hasi. Muktadha huu ni baada ya mwanamfaume kumdunga Fumo Liyongo kwa sindano ya shaba kitovuni kuonyesha usaliti na ukatili wa mwanamfaume. Hasira zilimpanda Fumo Liyongo na kumlenga mwanamfaume mshale uliompata kwa tako thibitisho la ushujaa wa kimwili. Fumo Liyongo alichukua mshale na kuuweka mahali pake bila kuona kwa uwazi, akajitayarisha kuvuta lakini akakata kamba. Wanawake walishindwa kuteka maji na kwa ushauri wa Kadhi Mkuu, Mwanananga na Mwanaziza walimwimbua Fumo Liyongo bembelezi ili aondoke mahali pale bila kujua alikuwa maiti kuonyesha mshikamano wa jamii. Mwanaziza aliacha kukariri na kumchapa mwanawe kwa ufito huku akianguka kama gogo.

Nyimbo za kivita ziliimbwa hivi na wapiganaji:

Wakaimba nyimbo za kondo na kupiga miguu chini huku wakicheza
na kujipiga vifua vyao kwa nguvu. Sauti zao zilipaa angani kwa
ukali na ghamidha. (Siri Sirini 3 2014:263)

Nyimbo hizi zinajitokeza pale Omar Soba alipiga mbiu ya mgambo na kuwaita wapiganaji wa Ozi baada ya kujulishwa kuuawa kwa Fumo Liyongo na Mwinyi. Kibwana Mwengo Bashee alienda Ozi na kuwafahamisha Abanoye na babake juu ya mauaji ya Fumo Liyongo na Mwinyi kuonyesha mshikamano wa Fumo Liyongo na mfuasi wake Kibwana Mwengo Bashee. Omar Soba aliwaita wapiganaji wa Ozi na kuwapasha habari hiyo. Raia wengi wa Ozi walifika mahali pale wakiwa na hamu ya kujua kilichoendelea. Omar Soba aliwaelezea ujumbe aliopewa na Kibwana Mwengo Bashee. Baada ya maelezo, watu walilia na kuamua kulipiza kisasi thibitisho la umoja na ushirikiano katika jamii husika. Wapiganaji wa Ozi waliingia vitani dhidi ya

Washanga na wakaamua kuongozwa na Abanoye na Kibwana Mwengo Bashee. Vita vilimuondoa Mfalme Daudi Mringwari mamlakani hivyo kuleta mabadiliko nchini Shanga.

Wimbo ufuatao uliimbwa na Abanoye:

Mwito, mwaitwa!
Waume njooni
Mwito, mwaitwa!
Waume njooni
Ikiwa hamji, swiswi twawajia
'Mevaa bendera mwanamke mzo
Kungusa tombo...Aah! Aah! Aah!

Siri Sirini 3 (2014:341)

Abanoye aliimba wimbo huu wakati yeye, Mwananinga, Mwanaziza na Mwanalemba walisubiri kuitwa katika kikao kilichofanya uteuzi wa viongozi kuonyesha mabadiliko katika uongozi. Wanawake hawa walikuwa wamechoka huku wakijawa na hasira. Abanoye aliwaambia wenzake kwamba huko kwao Ozi, kulikuwepo na wimbo uliosadifu muktadha wao. Wimbo ulikuwa wito kwa wanaume waliokuwa katika kikao, kuwatanabahisha kuhusu haki zao kwa sababu wasipowaita wangewaendea kuonyesha nafasi ya mwanamke katika uongozi.

Osman Ali Kidhabi aliimbiwa wimbo ufuatao:

Mkojozi! Naapelekwe pwani!
Mkojozi! Naapelekwe pwani!

Halafu watoto waliugeuza wimbo na kuimba mwingine mbadala mkumbo mmoja.

Mtu wangu, ana kidengele,
Leo, n'namnyoa nyele!
Kipara ngoto, maji ya moto
Kesho n'tamtia ngoto!

Siri Sirini 3 (2014:187)

Matukio haya yanatokea akilini mwa Mfalme Daudi Mringwari baada ya kufahamishwa kuwa Osman Ali Kidhabi alikuwa ametumwa Ozi kumwangamiza Fumo Liyongo kuonyesha usaliti wa Suleiman Mringwari. Suleiman Mringwari alimjulisha babake jambo hili katika kikao kilichojadili jinsi ya kumuua ya Fumo Liyongo dhihirisho la uongozi dhalimu. Suleiman Mringwari alimchekelea Osman Ali Kidhabi kwa kushindwa kumuua Fumo Liyongo nchini Ozi. Osman Ali Kidhabi

alikasirishwa na kicheko hicho na kusema kuwa aliyecheka mwisho huwa mshindi, kauli iliyomkera Mfalme Daudi Mringwari hivyo kuibusha mawazo ya wimbo huu. Wimbo ulimkejeli na kumfedhehesha Osman Ali Kidhabi kwa tabia ya kujilowesha usiku kitandani.

Usimulizi wa nyimbo umetumiwa kama burudani, kustarehesha na kusiona hadhira lengwa. Usimulizi huu umehamasisha watu katika jamii kwa kuwachochea ili kuungana pamoja na kutetea haki zao. Majukumu muhimu kama ya kushauri, kuonya, kukejeli, kutia moyo, kuelimisha na kubeza yamepitishwa hivyo kufanikisha uelewa wa matukio katika riwaya hii.

4.8 Usimulizi wa kirejeshi

Usimulizi wa kirejeshi ni usimulizi ambao unategemea wakati uliopita ili kufanya msimulizi kutafakari kuhusu yaliyotokea na kubainisha tofauti zilizopo kati ya jana na wakati uliopo (Wamitila, 2003). Usimulizi wa kirejeshi hutumiwa na msimulizi: Kutupa msingi wa hali ya mhusika kwa kuyamulika maisha yake ya awali, kubainisha misukumo ya wahusika mbalimbali na historia au maisha yake ya mbeleni na kuweka msingi imara ya kuendeleza dhamira na maudhui ya kazi inayohusika. Usimulizi wa kirejeshi unaweza kuainisha wazi kati ya msimulizi kama kijana na alivyo kama mtu mzima kama katika riwaya ya *Nguvu ya Sala* ambapo Susan anayasimulia na kuyatazama matukio yake kama msichana mdogo tofauti na alivyo kama mtu mzima (Wamitila, 2003). Riwaya teule imetumia usimulizi kirejeshi mfano Juma Obo kurejelea Mfalme Anzuruni aliyekuwa dhalimu:

Leo hii Shanga yetu haina tofauti kab'sa na nchi aliyoitawala amfalme dhalimu wa kale, Anzaruni, ambaye kadhia yake inasimuliwa kikamilifu katika shairi asili la Siri Sirini; shairi ambalo mimi mwenyewe binafsi yangu nimebahatika kulisoma. Huyu mtawala wetu hapa na mfalme Anzaruni wa karne hizo za kale ni sarafu moja kwa ya pili. (Siri Sirini 3 2014:194)

Tukio hili lilitokea katika kikao cha kwanza alichofanya Fumo Liyongo msituni baada ya kurudi Shanga. Mazungumzo kikaoni yalilenga uongozi wa nchi ya Shanga kuonyesha mshikamano wa Fumo Liyongo na wafuasi wake. Juma Obo alisema kuwa dhuluma lilikuwa tatizo kubwa katika taifa la Shanga na kufananisha Shanga na nchi iliyotawaliwa na mfalme Anzuruni ambaye kadhia yake inasimuliwa katika shairi la

‘Siri Sirini’ dhihirisho la uonevu katika uongozi. Juma Obo aliwauliza wenzake kupigana na madhalimu kudhihirisha mapinduzi. Uongozi wa Mfalme Anzuruni umerejelewa na Mwanaziza:

Tofauti ya dhalimu Anzuruni wa hadithi na Mfalme wa Shanga ni majina tu; hilo lifahamu, tena lifahamu sana. Watu hawa wawili imani zao ni moja, silaha zao ni moja na matendo yao ni mamoja. (Siri Sirini 1 2013:60)

Msimulizi anasimulia udhalimu wa Mfalme Anzuruni akiwa kusini alikokuwa amehamia baada ya kufungiwa ngomeni kwa mwanawe Fumo Liyongo. Mwanaziza alimwambia Mwanalemba maneno haya kumhusu kakake Mfalme Daudi Mringwari kuonyesha udhalimu katika uongozi wake kwa kutumia hirizi na imani za kishetani, ufisadi na kukamata wanawake kwa nguvu.

Usimulizi kirejeshi umetumika na Osman Ali Kidhabi kurejelea uzawa wake:

Nilizipata kwa mama. Mama yangu alikuwa kijakazi; mtumwa mwanamke manake! Utumwa tayari ni nongo mbi! Akamzaa mwana, mimi hapa. Mwana huyo hakujulikana iseye...yaani kumbe najisi kilichozawa na mwanamke mtumwa! Vipi nisionewe mtu mimi name mwembamba hapo kambani palipo karibu kukatika? (Siri Sirini 2 2014:180)

Msimulizi anaeleza uzawa wake katika mazingira ya mahakama ambapo Osman Ali Kidhabi alijitetea juu ya mauaji ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Osman Ali Kidhabi alirejelea uzawa wake kwa kuisitiza kutomuua Mfawidhi Kijumwa Mfaume, kwamba yalikuwa maonevu kwa vile wazazi wake hawakujulikana. Alieleza kuwa mamake alikuwa Kijakazi kama tunavyoelezwa:

Inasemekana ya kuwa Mfalme mzee alimpenda kijakazi mmoja, mamake Kidhabi. Wakafanya yao waliyofanya, kijakazi akashika mimba, Kidhabi akazawa. Ionekanavyo ni kuwa Daudi Mringwari, Mfalme aliye kitini sasa, aligundua uhusiano huo mapema sana. (Siri Sirini 2 2014:11-15)

Msimulizi anajulisha kuhusu uhusiano wa Osman Ali Kidhabi na Mfalme Daudi Mringwari. Osman Ali Kidhabi alifafanua kuwa hakuwa mwanaharamu wala mwanga na kumtaja shahidi wake kuwa Mfalme Daudi Mringwari. Kwa sababu ya maelezo hayo, Osman Ali Kidhabi aliachiliwa huru na mwenzake Shalo kupatikana na kosa la mauaji hayo hivyo kuhukumiwa kifo dhihirisho la mapendeleo katika mahakama.

Usimulizi kirejeshi umetumika kurejelea ‘Utenzi wa Mwanakupona’:

Kwa hakika nilivutiwa sana na mawazo yake kuhusu elimu tunayopaswa kuwapa vijana, akiwa yeye ni mmoja wao. Ana mapendekezo ya elimu, kwa menke zote mbili; yaani si ya wasichana peke yao, bali pia wavulana. Jambo lililonisisimua zaidi ni kwamba dhana zote alizonazo haziachani ghafla na mila, jadi na utamaduni wetu...mawazo yake ni ya kimapinduzi kiasi chake, hivi kwamba yana uwezo wa kuwabadilisha vijana na kuwasababisha kuwa na mtazamo wa kimapinduzi. (Siri Sirini 3 2014:318)

Maelezo haya yamerejelewa katika kikao cha uteuzi wa viongozi wapya nchini Shanga baada ya kuondolewa mamlakani kwa Daudi Mringwari kuonyesha ujenzi wa jamii mpya. Kibwana Mwengo Bashee alipendekeza Mwanakupona kupewa wadhifa wa Waziri wa Elimu kwa sababu ya mawazo yake kuhusu elimu ya jinsia zote mbili yaliyofichama katika utenzi wake. Mwanakupona aliandika utenzi huo akiwa na umri mdogo kuonyesha mabadiliko katika elimu. Mwanakupona aliandika utenzi husika ili kuchangia burudani katika arusi yake kuonyesha umuhimu wa sherehe ya arusi. Mwanakupona alipendekeza baba au mamake kuughani. Mfalme Daudi Mringwari alitaka kujua yaliyoandikwa katika utenzi wa Mwanakupona. Aliambiwa hivi:

Aaah, mambo ya kawaida tu, ya mama kumpa mawaidha binti yake; ya jinsi mwanamke aliyefunga ndoa anavyotakikana kuishi vyema na mumewe... Nadhani anafikiria siku za usoni; yaani baada ya kuolewa, ambapo inatarajiwa atapata mwana, kwa uwezo wa Muumba wake, kufuatia sheria za kimaumbile alizowekea viumbe vyake. (Siri Sirini 1 2013:177)

Msimulizi anafafanua kwamba Mwanakupona aliandika utenzi wa mawaidha kwa vijana wa jinsia zote. Mfalme Daudi Mringwari alipendekeza utenzi wa Mwanakupona kutumiwa kufunza madrassa yote ya Shanga thibitisho la mapinduzi katika elimu na utamaduni. Mfano mwingine wa usimulizi kirejeshi ulitumiwa na Washanga hivi:

Wale waliokuwa wamejitayarisha kuimba wimbo maarufu wa kulakia mashujaa; wimbo waliokuwa wameuzoea sana tangu zama za shujaa wa mashujaa:

Fumoo-loti...

Shindaa!

Fumo Liyongo...

Shinda shinda wote shinda!

Nchii, yetu...

Shanga!

Oh Shanga yetu...

Shinda shinda kote shinda!

Siri Sirini 1 (2013:351)

Wasimulizi ambao ni watu wa Shanga waliwasubiri mashujaa kutoka Misri kwa kurindimisha magoma bila kujua waimbe wimbo gani wa kuwakaribishia wageni mahashumu nyumbani. Washanga walikumbuka wimbo waliokuwa wakiambia Fumo Liyongo, ilhali walikuwa wameonywa vikali dhidi ya kuuimba. Wimbo ulihimiza uzalendo na mshikamano wa kitaifa na kumsifu Fumo Liyongo kwa uadilifu wake. Fumo Liyongo alikuwa shujaa aliyepigania nchi ya Shanga na kuifanya himaya kubwa lakini alifungwa ngomeni kwa kosa la uhaini kama asemavyo msimulizi:

Fumoloti amelifanyia mengi taifa letu. Siye huyu Fumoloti, yuyu huyu, aliyendokea kuwa jemadari hodari zaidi Uswahilini kote? Siye huyu Fumoloti aliyewashinda maadui zetu wote na kuipanua nchi yetu ndogo ikawa himaya pana yenye kuyunga? Sio huyu Fumoloti aliyeleta uhusiano mwema baina yetu na jirani zetu Uswahilini kote na, kwa hilo, akatufanya tuheshimike baina ya mataifa ya fahari, huku Uswahilini na hata ng'ambo? (Siri Sirini 1 2003:11)

Maelezo ya muktadha uliorejelewa ni kuwa shujaa Fumo Liyongo alipigania nchi ya Shanga kila wakati akipata ushindi kuonyesha uhodari na umaarufu wake. Fumo Liyongo alijenga uhusiano mwema na nchi jirani kudhihirisha ushujaa wake wa kimwili, kiakili na mshikamano. Nchi ya Shanga iliheshimika kwa sababu ya Fumo Liyongo ambaye walisaliti na kumfunga ngomeni kikatili kwa tuhuma za uhaini.

Usimulizi wa kirejeshi unaonekana Abanoye anaporejelea tukio la kubakwa:

Nitakwambia umuhimu mwingine wa mimi kuupata huo ujuzi wa kupigana. Ni imani yangu kuwa, kama ningekuwa najua kupigana pale hao maaluni waliponichafua, basi hawangefanikiwa katika mradi wao huo mwovu kupindukia. Ningepambana nao kiume na ningewashinda vibaya sana, sina shaka! Hawangefaulu kuniwachia hili kovu la najisi ya aushi waliloniachia! (Siri Sirini 1 2013:403)

Msimulizi anarejelea tukio ambalo alibakwa na wapiganaji watano kutoka mbari nyingine waliopambana nao ili kumvunja moyo baba yake dhihirisho la ukatili. Baada ya kumbaka, alishika mimba na kumzaa mtoto Mwinyi. Baadaye, Abanoye alipangiwa ndoa kwa mvulana muungwana ambaye alipendelea kumkumbusha kwamba alibakwa. Baada ya miaka miwili, Abanoye alipewa talaka. Alijifungua mtoto wa kike, Mize ambaye alikataliwa na babake kwa sababu ya jinsia thibitisho la taasubi ya kiume.

Usimulizi wa kirejeshi umetumika kurejelea familia ya Fumo Liyongo hivi:

Alianza na aila yake pana, hususan kuhusu uhusiano wa watu binafsi katika aila hiyo. Mamake alisema, alizaliwa na ndugu wawili, tumbo moja kwa baba na mama. Kifungua mimba na wazazi wao alikuwa mke. Huyu ndiye mama ya Kadhi Mkuu wa Shanga, Sheikh Zahid Majid Mngumi. Bibi huyu alifariki dunia zamani. Mdogo wa huyu alikuwa ni mume, naye ndiye mzazi wa Mfalme Daudi Mringwari. Yeye pia alifariki dunia. Mwanamme huyo ndiye aliyeondokea kuwa mfalme wa Shanga. Kwa upande mwingine, mamake Mwanalemba na kakake, yaani Daudi Mringwari, ambaye pia, alifariki dunia, ni shangazi lake Waziri Mkuu... Nishawahi kukusimulia, penginepo, ama? (Siri Sirini 3 2014:40-44)

Maelezo haya yanafafanua familia ya Fumo Liyongo. Mazingira haya ni baada ya Abanoye kumnasihi mumewe, Fumo Liyongo amwadithie matukio yote maishani mwake tangu utotoni au hata kabla ya uzawa wake. Fumo Liyongo alitoa maelezo ya ayali yake pana na kuzakania mlango wa Mwanaziza: Jinsi alishiriki unyago, uchumba, ndoa kwa Bauri na kujifungua kwa mtoto Fumo Liyongo kuonyesha mahusiano katika familia. Hapo awali Fumo Liyongo alikuwa amemtajia Abanoye watu wa aila yake bila ufafanuzi.

Uongozi wa Mwanaziza umerejelewa katika kikao kilichojadili uteuzi wa viongozi wapya nchini Shanga:

Wa pili ni Bi-mkubwa Mwanaziza. Nampendekeza nikizingatia umri wake mkubwa na ukomavu wake wa kiakili na kiruwaza. Vilevile naukazama uzoefu wake wa kushughulikia mambo aina aina yenye kuhusiana na uongozi, na pia mtagusano wake na watu na nasaba zote hapa kwetu, huko Pate na hata ng'ambo. Waaidha, sote twafahamu ya kwamba ana ujuzi wa kutosha katika uwanja huu wa uongozi. La ziada anajua Kiarabu kabisa! (Siri Sirini 3 2014:315)

Msimulizi anaeleza kwamba Mwanaziza alikuwa mzoefu katika uongozi hivyo kupendekezwa kupewa wadhifa katika serikali mpya ya Shanga dhahirisho la ujenzi wa jamii mpya. Mwanaziza alikuwa na uhusiano mwema na watu wa matabaka yote ndani na nje ya Shanga thibitisho la kiongozi mwema. Kikao kilijadili uteuzi wa viongozi wa Shanga baada ya kuondolewa mamlakani kwa Mfalme Daudi Mringwari. Bauri wa Liyongo alipewa wadhifa wa Mfalme kuonyesha mapinduzi na ujenzi wa jamii mpya. Usimulizi unaarifu kwamba kabla Mfalme Daudi Mringwari kuchukua uongozi, Mwanaziza alikalialia kiti cha kakake kwa lengo la kumshikilia hatamu mtoto Daudi hadi alipotimiza umri wa miaka kumi na minane na kutawazwa.

Kwa hivyo, usimulizi wa kirejeshi umefanikisha usimulizi wa riwaya hii kwa kuyamulika maisha ya awali ya wahusika, misukumo yao katika maisha na kutupa misingi ya matukio mbalimbali.

4.9 Usimulizi elekezi

Usimulizi elekezi ni usimulizi ambapo matukio ya baadaye ambayo wakati wake haujafika yanawasilishwa. Usimulizi huu hutokea pale ambapo tukio au matukio yajayo yanadokeza kabla ya kutokea kwake. Hii ni mbinu ya usimulizi ambayo kimsingi inachujua taharuki ya hadithi inayosimuliwa kwa kuwa inasimulia matukio kabla ya ulazima wake wa kiwakati (Wamitila, 2008). Naye Wambui (2018) anafafanua kuwa usimulizi elekezi huchukua sifa za ubashiri na hutumika zaidi katika bibilia. Usimulizi huu huweza kuhusisha kiambishi 'ta' au 'ki'. Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* imehusisha namna ya usimulizi unaotokea kabla ya matukio kutendeka katika sehemu mbalimbali kwa mfano:

Abanoye anamuomba Fumo Liyongo kumfundisha kupigana na silaha:

Nataka unifundishe kupigana nikitumia silaha ili niwe na uwezo wa kujitetea mimi mwenyewe binafsi, na aidha kutetea yeyote aliye mwendani wangu: baba, watoto wangu, wewe mume wangu, na kadhalika. (Siri Sirini 1 2013:402)

Msimulizi na bwanake walikuwa chumbani chao baada ya Fumo Liyongo kumpa habari za jamaa zake kama vile: Zahid Majid Mngumi, Mwanananga, Mwanakupona, Bauri, Daudi Mringwari na mkewe Mwanalibasi, Suleiman Mringwari, Mwanalemba na mumewe Abubakar Shahamey Makame na Mwanaziza. Maelezo mengine yalikuwa ya viongozi nchini Shanga kama vile: Mfawidhi Kijumwa Mfaume, Harun Rashid Dhabina, Osman Ali Kidhabi, Omar Said Famau na Muhammad Juma Obo kuonyesha mahusiano mema. Fumo Liyongo alimfundisha Abanoye kutumia silaha. Mafunzo ya kutumia silaha aliyopewa Abanoye yalimsaidia kupigania nchi yake ya Ozi kama inavyosimuliwa:

Kwa upande wake, kiongozi mwenyewe alitumia silaha aina tatu tu: panda, teo, uta na mishale. Alizitumia silaha hizi kwa ustadi mkubwa; kila alipolenga, alifaulu kukiwahi ndipo chenye kulengwa! Aliyemwahi yeye kwa silaha hafifu akamwangusha lakini akakosa kumwangamiza, huyo alimalizwa na walinzi wake waliokuwa karibu naye wakati wote. Walinzi hao walifurahia sana kazi yao hiyo ya kumlinda na, kumkamilishia mradi wake. (Siri Sirini 3 2014:274)

Msimulizi anajulisha kwamba Abanoye alitumia ujuzi wa kutumia silaha aliyofundishwa na Fumo Liyongo kulipiza kisasi mauaji ya kinyama ya mumewe Fumo Liyongo. Waziri Mkuu, Waziri wa Sheria na mwanamfaume walikuwa miongoni mwa walioaga dunia vitani dhahirisho la uzalendo. Daudi Mringwari akiong'olewa mamlakani huku uongozi mpya wa Shanga ukipewa Bauri wa Liyongo thibitisho la ujenzi wa jamii mpya.

Tukio kabla ya wakati wake limesimuliwa na Waziri Mkuu:

Si kwamba namdhanja... najua ni yeye tu! Daima ametamani sana kuniadhiri. Lengo lake ni kuhakikisha ya kwamba ameniaibisha kabisa kabisa machoni mwako, ilimradi ukinfuta kazi, nafasi yangu aichukue yeye. (Siri Sirini 2 2014:272)

Msimulizi alimpelekea Mfalme Daudi Mringwari shairi la 'Siri Sirini' ili aweze kulisoma. Mfalme Daudi Mringwari alilisoma na kudai maoni yao kulihusu. Waziri Mkuu alisema kwamba mtunzi wa shairi la 'Siri Sirini' alikuwa naibu wake, Omar Said Famau ili achukue nafasi yake ya kazi kuonyesha chuki. Mtunzi wa shairi la 'Siri Sirini' alikuwa akitafutwa ili aadhibiwe thibitisho la uongozi dhalimu. Omar Said Famau alipewa wadhifa wa Waziri Mkuu katika serikali mpya ya Shanga kama ilivyobashiriwa hapa:

Na mkubwa wake awe yule aliyekuwa naibu katika utawala uliopita.
(Siri Sirini 3 2014:317)

Tukio lililodokezwa lilitokea baada ya Waziri Mkuu kuaga dunia vitani baina ya Waozi na Washanga baada ya mauaji ya kikatili ya Fumo Liyongo. Mfalme Daudi Mringwari aliondolewa mamlakani. Kikao kilichojadili uteuzi wa viongozi katika serikali mpya kilimpendekeza Omar Said Famau kuchukua wadhifa wa Waziri Mkuu na naibu wake kuwa Mwanalemba aliyeandika 'Siri Sirini' dhahirisho la mapinduzi na ujenzi wa jamii mpya nchini Shanga.

Usimulizi elekezi unajitokeza katika kifungu kifuatacho:

Sijui kwa yakini... bali mwili wangu waniambia hatutaonana tena.
(Siri Sirini 3 2014:110)

Msimulizi alitumia usimulizi huu wakati Fumo Liyongo alikuwa akijitayarisha kurudi Shanga baada ya kushawishiwa na mwanamfaume dhahirisho la hila na udanganyifu.

Abanoye hakukubaliana na uamuzi wa Fumo Liyongo kurudi Shanga. Machozi yalimtiririka, mara akacheka, kisha akatumia kauli hiyo. Fumo Liyongo alirudi Shanga akiandamana na mwanawe Mwinyi. Suleiman Mringwari alimuua Fumo Liyongo huko msituni Shanga kwa kumdunga kitovuni kwa sindano ya shaba hivyo, Abanoye hakumuona Fumo Liyongo tena thibitisho la huzuni na upweke.

Usimulizi elekezi unapatikana hapa:

Nasema kweli wenzangu! Haitachukua muda mtavamiwa na makundi ya Wagalla. (Siri Sirini 3 2014:241)

Tukio hili lilitendeka baada ya uchunguzi kufanywa kuhusu mauaji ya Fumo Liyongo. Washanga hawakuridhika na matokeo ya uchunguzi yaliyotolewa na Waziri wa Sheria. Usimulizi unaeleza kwamba Mshanga mmoja alisema kuwa wangevamiwa na Wagalla. Baada ya mazishi ya Fumo Liyongo, Kibwana Mwengo Bashee alienda Ozi na kuwajulisha Abanoye na babake Omar Soba kuhusu mauaji hayo. Kwa hivyo, Wagalla chini ya uongozi wa Abanoye waliwavamia Washanga. Usimulizi unaarifu kwamba:

Siku chache baadaye, uvumi ukaenea Shanga mjini kuwa nchi imevamiwa na Wagalla. Watawala nyoyo zikawapasuka!... Tumevamiwa ndugu zangu! Tumevamiwa na wachokozi shirikene na wachochezi wasaliti! Wote hao ni adui zetu! Basi hatuna budi bali kupambana nao kiume na kuwarudisha huko kwao watokako, wakiwa wafu! (Siri Sirini 3 2014:268)

Mwandishi anaeleza kwamba Wagalla waliwavamia Washanga huku wakiongozwa na Abanoye na Kibwana Mwengo Bashee kuonyesha hatima ya kisasi na usaliti katika uongozi. Washanga wakiongozwa na Mfalme Daudi Mringwari walipanga mikakati na kukabiliana na Wagalla. Mapambano yalianza kwa dhati huku Washanga wengi wakiuliwa. Waziri Mkuu, Waziri wa Sheria na mwanamfaume ni miongoni mwa waliofariki. Mfalme Daudi Mringwari aliondolewa uongozini kuonyesha mapinduzi na mwamko mpya chini ya uongozi wa Bauri wa Liyongo.

Usimulizi elekezi umetumiwa na Matano hivi:

Mfawidhi anaamini ya kwamba utawala ukithubutu kumwangamiza mtu awaye yeyote yule kisiasa, basi na huo utawala wenyewe ungeporomoka na kuangamia kabisa, usiweze kukumbukika tena katika mapisi! (Siri Sirini 2 2014:35)

Msimulizi alikuwa miongoni mwa wafuasi wa Fumo Liyongo waliomtembelea nchini Ozi kuonyesha ukimbizi na mshikamano wa wafuasi wake. Fumo Liyongo na wafuasi wake walijadili uongozi wa Shanga huku Matano akitoa kauli hii. Utawala wa Shanga chini ya uongozi wa Mfalme Daudi Mringwari ulimwagamiza Fumo Liyongo tukio lililosababisha kuporomoka kwa utawala wa Daudi Mringwari. Utawala wa Shanga ulipewa Bauri wa Liyongo thibitisho la mapinduzi.

Usimulizi wa matukio kabla ya kutendeka umefanikisha usimulizi wa matukio mbalimbali katika riwaya hii kwa kujenga taharuki ya matokeo kama vile: Abanoye kufunzwa kutumia silaha, naibu waziri Mkuu kuchukua wadhifa, Abanoye kutomuona mumewe tena, Washanga kuvamiwa na uongozi wa Shanga kuporomoka.

4.10 Usimulizi wa muhtasari

Katika usimulizi wa muhtasari, muda wa usomaji unachukuliwa kuwa mfupi kuliko ule wa hadithi kama anavyodokeza Wambui (2018). Muhtasari hutumiwa kuharakisha hadithi kwa kuyaondoa maelezo mengine ambayo hayana maana au hayana mchango mkubwa katika hadithi (mtaje). Rimmon-Kenan (Wamitila, 2002) anakubaliana na mawazo haya kwa kueleza kuwa mwendo au muda wa kusimulia hadithi unaweza kufupishwa kwa kuibana matini au kwa kutumia kauli fupi fupi za matukio. Hali hii husababisha kasi au mwendo wa usimuliaji wa hadithi kuharakishwa. Wakati wa usimuliaji hadithi huwa fupi ilhali wakati matini huwa mrefu kama vile:

Baada ya kupelekwa mahakamani na kujitetea vyema, alisamehewa makosa mawili aliyokuwa ameshtakiwa kwayo: kosa la ujasusi, na la uvamizi wa nchi akitumia silaha hatari. (Siri Sirini 1 2013:322)

Mwandishi anajulisha jinsi Fumo Liyongo alivyopelekwa mahakamani, kujitetea na kusamehewa. Usimuliaji wa tukio hili umeharakishwa kwa sababu mshukiwa haonekani mbele ya mahakama au jaji aliyemsomea mashtaka. Maelezo ya tukio hili yamesimuliwa kwa muhtasari. Fumo Liyongo alitoroka ngomeni siku ya arusi ya Mwanakupona na kuhamia nchini Ozi dhihirisho la ukimbizi. Fumo Liyongo alifanya maamuzi mengi kuhusu malazi, chakula na jinsi ya kuingiliana na watu. Humo mafichoni, alibeba zana zake za kujilinda na wanyama na wavamizi. Siku moja alivamiwa na wapiganaji wa Ozi waliozingira kibanda chake. Aliwashambulia kwanza na mapigano yakaendelea kwa muda kuonyesha ujasiri. Aliamua kujinusu kwa

kuteremsha silaha zake chini na kukubali wamwongoze kuonyesha ushujaa wa kimwili na kiakili. Walimfikisha kijijini kwa mudir wao. Mudir alimuuliza kujieleza huku akimwita bintiye kusaidia kutoa tafsiri. Alipopelekwa mahakamani, usimulizi unatoa muhtasari jinsi alivyojitetea na kusamehewa kwa makosa yote mawili dhahirisho la haki na msamaha. Baada ya kusamehewa, Fumo Liyongo alipewa cheo cha Jemadari wa majeshi yote ya Ozi na makazi katika boma ya mzee Omar Soba. Kwa hivyo, Fumo Liyongo aliamua kuijenga nchi ya Ozi kama alivyoijenga nchi ya Shanga.

Usimulizi wa muhtasari unapatikana katika kifungu hiki:

Wakati wa kufungisha ndoa ulifika, maarusi wakakalishwa itakikanavyo, babe-mtu akamtoa mwanawe kistahiki, na Kadhi Mkuu akatimiza wajibu wake. (Siri Sirini 1 2013:377)

Msimulizi anasimulia matukio katika arusi kati ya Abanoye na Fumo Liyongo. Kufungishwa kwa ndoa hii na Kadhi Mkuu kumesimuliwa kwa kifupi. Jamaa wa Abanoye waliohudhuria arusi alikuwa babake, Omar Soba na watoto wawili wa Abanoye, Mwinyi na Mize. Mamake Abanoye na kaka zake wanne walikuwa marehemu thibitisho la uhasama wa mbari nchini Ozi. Maarusi waliruhusiwa kuingia nyumbani mwao huku wakitoa shukrani zao kwa Mungu dhahirisho la imani katika dini.

Kipengele cha usimulizi wa muhtasari kinajitokeza hivi:

Wakaenda, wakaketi kwenye mnazi wao, kama kawaida yao. Kombo akawaeleza jinsi alivyoigundua hiyo maiti. Akawapa maelezo kamili jinsi mambo yalivyokuwa hadi pale alipomwambia mchungaji asanzuke hapo, nayeye akaenda kuwatafuta. (Siri Sirini 2 2014:109)

Maelezo aliyoyatoa Kombo kwa wenzake yalikuwa kwa kifupi. Kombo aliwasimulia wenzake jinsi alivyopata maiti ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Kombo alipashwa habari ya maiti na mchungaji jirani yake. Kombo aliuona mwili huo na kuutambua kuwa wa Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Alimwuliza mchungaji kuchukua mifugo wake na kuondoka mahali pale dhahirisho la ujirani mwema. Kombo alienda mjini kuwatafuta wenzake na alipowapata wote aliwaeleza kwa kikamilifu aliyoyaona isipokuwa jina la mchungaji kuonyesha usiri. Wenzake walipendekeza maandamano lakini Kibwana Mwengo Bashee aliwakataza kuonyesha uongozi mwema. Badala yake alimjulisha Waziri Mkuu, Imamu na Kadhi Mkuu thibitisho la mshikamano.

Msimulizi anatumia muhtasari katika kifungu hiki:

Baada ya kitambo kirefu, wakarudi ukumbini na kusema wameyakubali mapendekezo na maamuzi yote ya wazee. (Siri Sirini 3 2014:345)

Kibwana Mwengo Bashee alitoa maelezo kwa kifupi. Ilikuwa baada ya vita baina ya Waozi na Washanga ambavyo vilimuondoa Daudi Mringwari mamlakani. Suleiman Mringwari, Waziri Mkuu na Waziri wa Sheria walikuwa miongoni mwa watu walioaga dunia vitani kudhihirisha uzalendo. Kikao kilichoongozwa na Sheikh Zahid Majid kilifanya uteuzi wa viongozi wa serikali mpya ya Shanga kuonyesha mabadiliko katika uongozi. Kibwana Mwengo Bashee aliwajulisha kwa kifupi Mwanaziza, Mwanananga, Mwanalemba na Abanoye waliyokubaliana ili waweze kutoa mapendekezo yao kuonyesha ujenzi wa jamii mpya.

Usimulizi mwingine wa muhtasari ni huu:

Ni kauli yangu ya kungátuka! Nina maana nimeacha kazi! Tangu leo mimi si Kadhi Mkuu wa Shanga. Mwambie babako atafute mtu mwingine amkabidhi cheo hicho. (Siri Sirini 3 2014:8)

Msimulizi anasema kwa kifupi bila maelezo mengi kwamba amestaafu. Maelezo haya yalitokea msikitini baada ya Kibwana Mwengo Bashee kupigwa na askari katika maeneo ya msikiti kwa kulisambaza shairi la ‘Siri Sirini’ kuonyesha ukatili na kukosa heshima katika eneo takatifu. Watu walishangazwa na uvunjaji wa sheria zote za dini na utu. Watu walipotulia, Kadhi Mkuu alimpatia mwanamfaume barua ampelekee babake. Alisema kwa kifupi kwamba ilikuwa kauli yake ya kuacha kazi thibitisho la msimamo thabiti.

Kwa hivyo, usimulizi wa muhtasari umefanikisha usimulizi wa matukio katika riwaya teule kwa kuyaharakisha kama vile: Fumo Liyongo kujitetea mahakamani Ozi, arusi kati ya Fumo Liyongo na Abanoye, mazungumzo kati ya Kombo na wenzake, uteuzi wa viongozi wapya wa Shanga na kustaafu wa Kadhi Mkuu.

4.11 Usimulizi udondoshi

Usimulizi udondoshi ni usimulizi unaoacha maelezo fulani. Wamitila (2002) anaeleza kuwa katika usimulizi udondoshi kuna mwanda nunge katika matini ilhali hadithi

yenyewe ina wakati fulani. Katika msingi huu wakati-hadithi na wakati-matini huwa tofauti kama vile riwaya ya *Utengano* (1980) ambapo maisha ya Musa yameondoshwa katika usimulizi baada ya kutengana na Kazija. Musa anaingizwa tena katika usimulizi hospitalini alipokuwa akifanya kazi na babake kupelekwa humo akiwa hali mahututi. Usimulizi udondoshi umedhihirishwa katika sehemu mbalimbali katika riwaya teule kwa mfano:

Liyongo alijikuta katika mazingira tofauti kabisa. Huku alikuta kulikuwa hakuna watu wengi wala miji mikubwa, bali kulikuwa na vijiji kadha wa kadha, baadhi yavyo vikubwa si haba. (Siri Sirini 1 2013:264)

Mwandishi anafahamisha maisha ya Fumo Liyongo nchini Ozi kama mkimbizi. Fumo Liyongo alitorokea nchi ya Ozi baada ya kuvunja ngome siku ya arusi ya Mwanakupona. Safari ya kwenda Ozi na changamoto safarini imeondoshwa katika usimulizi hadi Fumo Liyongo alipojikuta nchi ya Ozi katika mazingira tofauti bila watu wengi wala miji mikubwa kuonyesha ukimbizi. Alibaini kuwa wenyeji wa huko walitegemea mifugo hivyo kumlazimisha kufanya maamuzi mengi kama vile: Kutoharakisha kujitokeza kwa watu, kulala katika vibanda vya shamba akibahatika kuviona, kula matunda, ndege, nzige, kumbikumbi na wadudu wengine na wanadamu wa kwanza kutangamana nao wangekuwa wanawake kudhihirisha ushujaa wa akili.

Usimulizi udondoshi unajitokeza katika mazungumzo ya Abanoye. Anasema:

Tena vizuri sana! Niliishi huko miaka miwili mizima! ...babangu alinipeleka huko kusoma madrassa. (Siri Sirini 1 2013:315)

Maisha ya Abanoye kwa miaka miwili Lamu alikosomea madrassa yameondolewa katika usimulizi. Abanoye alimsimulia Fumo Liyongo maisha yake: Kwamba aliishi Lamu miaka miwili akisoma, kubakwa, ndoa, talaka na watoto wake Mwinyi na Mize kuonyesha ukatili. Maisha yake na mumewe muungwana kwa miaka miwili inadokezwa tu. Kwa hivyo, Fumo Liyongo aliamua kumuoa Abanoye na kuwa baba wa Mwinyi na Mize kudhihirisha utu wake.

Usimulizi udondoshi unajitokeza hivi:

Waziri akaeleza kila kitu! Kila kitu, yaani, yaani isipokuwa mambo fulani fulani ambayo wale waliowahi kwendaukagua mwili wa marehemu, waliokuwa ukumbini humo wakati huo, waliwaza kuhisi

mara moja kuwa mambo hayo yamedondoshwa. (Siri Sirini 2 2013:113)

Msimulizi anaeleza tukio ambalo mambo fulani yameondoshwa katika usimulizi wakati Waziri wa Sheria alimpa Mfalme Daudi Mringwari habari kuhusu kifo cha Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Mfawidhi Kijumwa Mfaume aliuliwa kinyama. Watu walioukagua mwili huo waliweza kuhisi kwamba mambo yalidondoshwa katika taarifa ya Waziri wa Sheria thibitisho la kukwepa haki. Watu ambao walikuwa kwenye kikao hawakujua ukweli uliokuwepo kwa wakati huo. Kwa hivyo, Mfalme Daudi Mringwari alipendekeza uchunguzi kamili kufanywa kuonyesha uwajibikaji.

Usimulizi udondoshi unaonekana kama ifuatavyo:

Mara moja mwenye kukabidhiwa amana akaituliza nadhari na kuiangalia vyema; yaani kuitulizia nadhari na kuitathmini barabara. Liyongo akakolwa na habari aliyoisoma. (Siri Sirini 2 2014:192)

Maelezo yanadokeza ya kuwa Fumo Liyongo alikabidhiwa shairi la ‘Siri Sirini’ na Mwanananga. Mwanananga alikuwa ametumwa na Mwanaziza kwa Fumo Liyongo ili awape ushauri kuhusu ujumbe katika shairi hilo. Usimulizi wa usomaji wa shairi hili na Fumo Liyongo umedondoshwa. Usimulizi unasema kuwa Fumo Liyongo alikolwa na habari aliyoisoma huku akitabasamu, akavuta pumzi kadri ya uwezo wake, kisha kuzishusha kwa kishindo kikuu. Fumo Liyongo alisema kuwa shairi hilo halikuwa utungo bali mzinga kuonyesha mapinduzi. Kwa hivyo, Fumo Liyongo aliwashauri kulisambaza shairi husika kwa tahadhari.

Mfano mwingine wa usimulizi udondoshi ni huu:

Huku nyuma Mfawidhi, Kibwana na wafuasi wake wakakimbilia hema alimokuwako Mwanakupona na nyanyake na kuwanyanyua juu kwa juu. (Siri Sirini 1 2013:203)

Msimulizi anaeleza kwamba arusi ya Mwanakupona ilitibuka baada ya babake Fumo Liyongo kuvunja lango la ngome na kutoroka. Maisha ya Mwanakupona baada ya kutibuka kwa arusi yake yamedondoshwa katika usimulizi hadi uongozi dhalimu wa Shanga ulipoondolewa mamlakani kuonyesha ujenzi wa jamii mpya kama usimulizi unavyodokeza:

...ikaingia habari ya kuwa Bauri wa Liyongo alikuwa amewasili akiandamana na dadake, Mwanakupona, na msafara mkubwa wa watu. (Siri Sirini 3 2014:359)

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa Mwanakupona alihusishwa katika usimulizi pale alifika Shanga kuchukua wadhifa wa Waziri wa Elimu. Maisha ya Bauri wa Liyongo pia, yamedondoshwa katika usimulizi hadi aliporudi Shanga kuiongoza baada ya kuondolewa mamlakani kwa mmabavu Daudi Mringwari dhihirisho la mapinduzi na ujenzi wa jamii mpya.

Uchunguzi umeonyesha kuwa usimulizi udondoshi kama vile: Safari ya Fumo Liyongo kwenda Ozi, maisha ya Abanoye Lamu, matokeo ya uchunguzi juu ya kifo cha Mfawidhi Kijumwa Mfaume, Fumo Liyongo kusoma shairi na maisha ya Mwanakupona baada ya kutibuka kwa arusi yake umefanikisha usimulizi wa matukio mbalimbali katika riwaya hii.

4.12 Usimulizi onyesho

Usimulizi onyesho kama anavyoeleza (Wamitila, 2002) ni namna ya usimulizi unaoleta sifa ya uigizaji katika matini ambapo wahusika huonekana wakizungumza mbele ya wasomaji wa kazi hiyo. Mazungumzo yanamwezesha msomaji kumwelewa mhusika fulani, jambo ambalo hutokana na ukweli kuwa mhusika huyo hufichuliwa vizuri. Matei (2011) anaeleza kwamba mazungumzo huwa ya aina mbili: Rasmi na isiyo rasmi. Mazungumzo rasmi huweza kupatikana kwenye sherehe za jandoni, harusi, maabadini, mazishi, siasa, posa na kortini. Katika mazungumzo maamkizi, shukrani, maagano na majina ya vyeo huwa muhimu kama anavyodokeza Ngure (2003). Katika onyesho, wakati- hadithi na wakati- matini huwa sawa, yaani hadithi inakwenda sambamba na usomaji wa anayehusika. Maneno ya wahusika huhusishwa moja kwa moja katika hadithi na hisia zao kuwekwa wazi mbele za wasomaji kama vile mazungumzo ya Mwanalemba na Mwanaziza:

Huko ndani mazungumzo ya dhati baina ya mtu na shangazi lake yakaanza; yakashika kasi na kunoga kipindi cha kufumba na kufumbua...kilichonileta hapa ni mgogoro ulioikumba aila yetu...Tofauti ya dhalimu Anzuruni wa hadithini na Mfalme wa Shanga ni majina tu; hilo lifahamu tena lifahamu sana. Watu hawa wawili imani zao ni moja, silaha zao ni moja na matendo yao ni mamoja...Nasi tuko tayari kusubiri majibu; tena yenye kuridhisha, kama ulivyotangulia kunena. (Siri Sirini 1 2013:54-62)

Mazungumzo kati ya Mwanalemba na Mwanaziza yalitokea kusini katika kasri ya pili ya Mfalme Daudi Mringwari. Mazungumzo haya yalifanyika baada ya Mfalme Daudi Mringwari kumtuma dadake Mwanalemba kwa Mwanaziza ili kusuluhisha mgogoro wa aila yao kuonyesha msamaha na maridhiano. Mgogoro huu ulitokana na kufungwa ngomeni kwa Fumo Liyongo hivyo kuwasukuma Mwanaziza na Mwananinga kuhamia kusini. Katika mazungumzo, Mwanaziza alimjulisha Mwanalemba ubaya wa Mfalme Daudi Mringwari. Mwanaziza alifafanua kwamba Mfalme Daudi Mringwari alikuwa mdhalimu na kumfananisha na Mfalme Anzuruni aliyesimuliwa katika hadithi ya ‘Siri Sirini’ dhahirisho la ufasidi katika uongozi. Mazungumzo haya yalimfanya Mwanalemba kumchunguza nduguye Mfalme Daudi Mringwari. Mwanalemba alimuomba Mfawidhi Kijumwa Mfaume kumsaidia kutafuta ukweli. Anamwambia:

Bila kukuficha, alisema yule bibi. Kuna jambo lililonikaa vibaya moyoni kwa mwiya wa masiku mengi tu...Ni mwovu. Anatendea watu maovu. Anatendea raia zake mambo maovu, hata wanawake, hasa wanawake... Sina shaka tushakubaliana sasa, kwa hivyo tufuate nyayo zetu turudi mjini, ama? (Siri Sirini 1 2013:100-104)

Maelezo yanasema kwamba Mwanalemba na Mfawidhi Kijumwa Mfaume walizungumzia jinsi ya kumchunguza Mfalme Daudi Mringwari kwa makosa ya: Uchawi, uporaji mali, kuwanyanyasa wafanyabiashara na ubakaji kuonyesha uongozi dhalimu. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alikubali kuanzisha uchunguzi huu dhidi ya Mfalme Daudi Mringwari.

Mfano mwingine wa usimulizi onyesho unadhihirika hivi:

Nimekuletea chakula, Mringwari akaanza. Najua, alisema Liyongo; akaendelea. Yule askari amekileta. Hangeweza kuutilia madharau utumishi wa mwanamfaume mwenyewe binafsi...Itumie fursa hiyo kujifunza mengi. Nataka ukirudi uwe umebadilika kiakili na kimawazo! Uwe mpevu katika mwelekeo na kila jambo kwa jumla. (Siri Sirini 1 2013:131-133)

Mazungumzo haya yanatokea wakati Suleiman Mringwari alimtembelea Fumo Liyongo ngomeni. Fumo Liyongo alifungiwa ngomeni kwa tuhuma za uhaini huku akinyimwa nafasi ya kujitetea kuonyesha ukatili katika asasi za utawala. Kijakazi Sada aliaminika kumpelekea chakula na ujumbe humo ngomeni. Suleiman Mringwari na Fumo Liyongo walizungumzia tabia ya askari ngome, arusi ya Mwanakupona na safari ya Misri. Fumo Liyongo alimshauri mwanamfaume kutompelekea chakula tena

ngomeni asije akadharauliwa kudhihirisha masuala la utabaka, ubaguzi na utawala. Kuhusu safari ya Misri, Fumo Liyongo alimuuliza mwanamfaume kuchukua fursa hiyo kujifunza mengi na kubadilika kiakili na kimawazo. Mwanamfaume walienda Misri na wajumbe wengine watatu na alirudi Shanga akiwa amebadilika. Alibadili msimamo wake juu ya Fumo Liyongo. Fumo Liyongo alishiriki mazungumzo tena na Suleiman Mringwari nchini Ozi:

Ndio kuna mambo yameenda kombo na yanazidi kuharibika. Ndiposa nimekuja Ozi kukuomba na kukutafadhalisha urudi nyumbani ukachangie katika kuyarekebisha kabla ha yajazorota kabisa... silaha ambayo unaweza kuitumia barabara kumdunga adui kwayo, japo liwe jitu. Mgunzu mwembamba, mfupi mathalan... Haya chapuka. (Siri Sirini 3 2014:66-85)

Maelezo ya dialogia hii ni kuwa Suleiman Mringwari alimtembelea Fumo Liyongo kama mkakati wa kumwangamiza. Mwanamfaume alikuwa ametumwa na wazazi wake, Waziri Mkuu na Osman Ali Kidhabi ingawa alimdanganya Fumo Liyongo kwamba alijituma kuonyesha ujanja. Mazungumzo yao yalilenga masuala mengi kama: Kifo cha Mfawidhi Kijumwa Mfaume, Kidhabi kwenda Ozi kwa nia ya kumwangamiza Liyongo, sababu za mwanamfaume kumtembelea Ozi, safari ya Misri, mabadiliko ya mwanamfaume na udhaifu wa kitovu. Suleiman Mringwari alipopata silaha ya kumwangamiza Fumo Liyongo, alirudi Shanga huku akimwacha Fumo Liyongo akijitayarisha kurudi Shanga baada ya kumhadaa kuonyesha usaliti.

Mazungumzo mengine ni haya:

Bwana wangu naomba unisamehe
Nikusamehe kwani umefanya nini Sada?
Si mimi, ni mwanamume hiyao!
Yule askari-ngome?
bwanayo waraka hunu. Kamjibu 'ndiyo n'tafanza.
Kilifika hiyao, kavitwaa rijali hiyao...kila kitu,
kimoya hayasaza!...Barabara kabisa!

Siri Sirini 1 (2013:156-158)

Mazungumzo haya yalifanyika ngomeni kati ya Fumo Liyongo na Kijakazi Sada. Fumo Liyongo alifungwa ngomeni kwa kosa la jinai. Kijakazi Sada aliaminiwa kumpelekea chakula na ujumbe. Katika muktadha huu Sada alimpelekea chakula na waraka uliokuwa 'Utenzi wa Mwanakupona'. Askari- ngome walimpokonya chakula na utenzi huo kudhihirisha ukatili wa askari-ngome. Fumo Liyongo aliwaza kuonyesha ushujaa

wa akili na kumtuma Sada na ujumbe kwa Mwanaziza. Askari- ngome hakufurahia mazungumzo hayo na kwa upevu wake wa akili Fumo Liyongo alimfunza Sada ushairi uliokuwa na ujumbe huo kuonyesha ushujaa wa akili. Fumo Liyongo alitumia ushairi kuomba tupa iliyomsaidia kuvunja ngome na kutoroka siku ya arusi ya Mwanakupona kuonyesha kutingishwa na kutiwa mashakani kwa uongozi dhalimu.

Kombo na mchungaji Ali wanazungumza hapa:

Kombo? We Kombo? Kombo? Kombo eeh! Nakwita hunisikii!.

Oh! Ni wewe Ali? Vipi?

Kombo aliamkua... Simjui. Nilimchunguza sana, kwa makini, lakini bado sikuwahi kumjua! Ni mtu gani basi? Na amezidi jinsi gani, mbona siri siri?

Siri ni ya nini? Mfu! Mfu? Leo una nini wewe? Hela nambie ni kitendawili gani hicho? Si kitendawili bali ni ukweli wa mambo!

Mtu ameuawa nadhani! Tena amechomwa! (Siri Sirini 2 2014:104)

Mchungaji Ali alifanya mazungumzo na jirani yake Kombo. Mchungaji Ali alikuwa akilisha mifugo wake alipoona kiwiliwili cha mtu bila kichwa. Alikichungulia na kuona kiwiliwili kilichokuwa cha mwanamme wa umri wa makamo. Mchungaji Ali alienda kwa jirani yake Kombo na kumjulisha kuonyesha ujirani mwema. Mchungaji Ali alimweleza Kombo na waliandamana kwenda kuona mfu. Kombo alikutazama mwili vizuri na kumtambua marehemu kuonyesha umakinifu wake. Kombo alimwuliza mchungaji kuchukua mifugo wake na kuondoka mahali pale. Kombo alielekea mjini alikowatafuta wenziwe mmoja mmoja hadi akawapata wote na kuwaongoza katika maskani yao, kwenye mnazi. Kwa hivyo, walipofika mnazini, walishangaa kuona dalili ya mgaragazo mkubwa dhihirisho la mshikamano miongoni mwa wafuasi wa Mfawidhi Kijumwa Mfaume.

Usimulizi wa mazungumzo umekuwa na jukumu la kuwasilisha ujumbe katika usimulizi. Usimulizi huu umewezesha kuwatambua na kuwasawiri wahusika huku tofauti zilizoko baina yao zikidhihirika. Hisia za wahusika wanaozungumza na jinsi wanavyoingiliana na kuhusiana zimewekwa wazi hivyo kuonyesha wasifu wao katika kazi hii.

4.13 Usimulizi uendelezaji

Usimulizi uendelezaji ni usimulizi ambapo msimulizi huyaangaza mawazo ya mhusika au ndoto (Wamitila, 2002). Katika usimulizi huu, wakati-matini ni mrefu kuliko wakati-hadithi. Usimulizi uendelezaji umetumika katika riwaya hii mfano:

Akagutuka usingizini na kuona sura ya mwanamke mzuri ajabu, mwenye weusi na mgwishu akimtazama kwa macho ya huruma! Akashangaa ni jinsi gani taswira hizi mbili zilivyoweza kusuhubiana na kusetana kabisa zikawa kitu kimoja. Vilimshangaza zaidi ya ziada alipokumbuka ya kwamba hivi ndivyo nusu ya matukio ndotoni mwake yalivyokuwa hasa siku chache zilizopita! Akafikiri na kuwaza zilikuwa njozi mbili halisi hizi au mwenge bayana wa uhalisia? (Siri Sirini 1 2013:272)

Msimulizi anaeleza ndoto aliyoota Fumo Liyongo. Fumo Liyongo alikuwa nchini Ozi baada ya kutoroka ngomeni na kujipata Ozi kama mkimbizi. Fumo Liyongo aliishi katika kibanda alikovamiwa na wapiganaji wa Ozi. Baada ya mapigano makali kati yake Fumo Liyongo na wapiganaji, Fumo Liyongo aliwaruhusu wampeleke walikodhamiria kuonyesha ushujaa wa kivita. Wapiganaji walimpeleka kwa mudir wao alikosimulia hadithi yake huku msichana wake, Abanoye akitoa tafsiri. Abanoye aliamrisha na babake kumtayarishia chakula na mahali pa kulala. Fumo Liyongo aliota akiwa amepolekewa mkewe Mwanananga huku wakiwa na siku mbili za kujistarehesha. Alipogutuka usingizini, aliona sura ya mwanamke mweusi akimwangukia kwa macho ya huruma. Aliamua kumwambia Abanoye kwamba alimpenda. Fumo Liyongo alionyesha mapenzi yake kwa Abanoye. Kwa hivyo, Fumo Liyongo na Abanoye walifunga ndoa.

Usimulizi uendelezaji umetumika katika kifungu hiki:

Akawaza: Au ni mimi niliyempeleka mwanamume wa watu kichinjioni? Sivyo? Kwa kutaka kunitii, akaingia mtegoni! Akakamatwa, akapelekwa kichinjioni, akaangamizwa! Mama yangu, mama yangu, mama yangu wee! Mbona uzito wa hatia unanilemea hivi jamani! Je, nina hatia? Bila shaka, bila shaka! Kwa ajili yangu, mwanamumengwa ameangamia! Laiti kama ningejua! Mola wangu mbona hukunimulikia kurunzi yako tukufu mapema nikaona lijalo mbele yangu? (Siri Sirini 2 2014:127)

Mawazo haya yanatokea wakati Mwanalemba alifahamishwa kuhusu mauaji ya kinyama ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Mwanalemba alilia, tukio ambalo

halikumpendeza mumewe. Mwanalemba aliwaza kwamba yeye ndiye alisababisha kifo chake kwa sababu alikuwa amemtuma kumchunguza Mfalme Daudi Mringwari kuonyesha usaliti katika familia. Mwanalemba alijiuliza kama alimpenda Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Kuona jinsi Mwanalemba alivyolia, bwanake alimshuku kuwa na uhusiano wa kimapenzi na marehemu thibitisho la kutoaminiana katika ndoa. Mwanalemba alimhakikishia bwanake kwamba aliziheshimu sheria zote za ndoa kudhihirisha mapenzi na uaminifu kwa wanandoa.

Usimulizi uendelezaji mwingine unadhihirika hivi:

Liyongo akapitwa na wazo lingine akilini mwanake. Akawaza: Nimejichongea? Nimo hatarini! Wala sidhani! Sina miye cha kukicha sina! Niche, nicheni! Ni mtego hunu, yeye nalomtegeya. Ikiwa yu mwerevu, akisha kunaswa, kwepuka tauepuka. Iwapo 'ye ni muinga, tangia ndani kitwa mbee akamatwa shingo ndi, ndi, ndi! Moo na moko tabanwa, kamwe n'de kutoka 'siwahi. Nami tateka zangu tekeo; koya noye, waingia ndia moya tusi'ngie tena abadani. Hapo shereheni nami tangia; vya ndia moya katu kutoikuta na wainga tuchandamana pamoya...leo na milele vi'vile! (Siri Sirini 3 2014:85)

Mawazo haya ya Fumo Liyongo yalitokea nchini Ozi. Suleiman Mringwari alitumwa na: Mfalme Daudi Mringwari, Malkia Mwanalibasi, Waziri Mkuu na Waziri wa Sheria kumshawishi Fumo Liyongo kurudi Shanga kwa nia ya kumwangamiza kuonyesha dhuluma na usaliti katika uongozi. Fumo Liyongo na mwanamfaume walizungumzia: Kifo cha Mfawidhi Kijumwa Mfaume, utawala wa Shanga, safari ya Misri na Fumo Liyongo kurudi Shanga. Fumo Liyongo alimfichulia mwanamfaume siri ya udhaifu wa kitovu kama silaha ya kuliua jitu. Baada ya kumtobolea mwanamfaume siri hii, Fumo Liyongo aliwaza kama mwanamfaume angeweza kuitumia siri hiyo kumuua. Mwanamfaume aliharakisha na kurudi Shanga. Fumo Liyongo alirudi Shanga akiandamana na mwanawe Mwinyi. Mwanamfaume alitumia siri ya kitovu na kumuua Fumo Liyongo thibitisho la usaliti na udanganyifu katika mfumo wa uongozi.

Usimulizi uendelezaji umetumika katika kifungu hiki:

Wazo likampitia akilini mwake. Akasikia sauti mumo akilini ikitangaza: Ozi yenu hiyoo..! Wala hamtaniona tena! Nikomeni!Naenda kulee.. kunakovutia na kupendeza, kule kwenye maendeleo ya kushangaza, kochokocho, tena yenye kutegemeeka! Nimechoshwa na Ozi na kukosa kwake maendeleo. Kutoka leo

nimepata uhuru kamili! Hakika sitapungukiwa na kitu. Nitaishi maisha ya starehe na uluwa, bila shaka! Mmeremeto ule? Nitaikosaje? (Siri Sirini 3 2014:150)

Mawazo haya ya Mwinyi yanatokea safarini. Fumo Liyongo na Mwinyi walikuwa safarini kutoka Ozi kwenda Shanga. Mwinyi alikuwa na hamu ya kufika Shanga ili awaone Mwanaziza na Mwanananga. Mwinyi alitamani maisha ya starehe ya Shanga. Alipoona majumba marefu ya ghorofa, alifikicha macho yake ili aone vizuri. Alitazama nyuma walikotoka na kuwaza jinsi Ozi haingemuona tena kwani alikuwa akienda kulikovutia kudhihirisha maendeleo, mabadiliko na mgongano wa shamba na mjini. Kwa hivyo, Mwinyi alimuomba babake waharakishe wafike Shanga.

Usimulizi uendelezaji unajitokeza hivi:

Akatoka. Alitoka huku akiwaza ‘yale niliyoyasikia ni sahihi, au akili yangu tu yanirubuni? Enh? Yanicheza shere akili yangu? Hakika kabisa hawapangi. (Siri Sirini 3 2014:202)

Mawazo haya yamo akilini mwa Mwanalemba wakati aliingia ghafla kwenye kikao kilichojadili maangamizi ya Fumo Liyongo baada ya kuwasili Shanga. Mwanalemba alimsikia Suleiman Mringwari akijigamba kwamba ndiye tu angemua Fumo Liyongo kuonyesha ukatili na usaliti wa Suleiman Mringwari kwa Fumo Liyongo. Maneno haya yalimfanya Mwanalemba kufikiria kama aliyasikia vizuri au akili yake ilimchezea. Mawazo haya yalimpeleka kwa Mwanananga. Walikimbia kumtafuta Fumo Liyongo ili wamjulishe mpango wa mwanamfaume lakini hawakufanikiwa kudhihirisha uhusiano mwema wa familia.

Kwa hivyo, usimulizi uendelezaji kama ulivyodhihirika katika: Ndoto ya Fumo Liyongo nchini Ozi, Mwanalemba kuwaza kuhusu Mfawidhi Kijumwa Mfaume, Fumo Liyongo kuwaza juu ya Suleiman Mringwari, mawazo ya Mwinyi kuhusu maendeleo ya Shanga na mawazo ya Mwanalemba juu ya aliyoyasikia umefanikisha uelewaji wa matukio mbalimbali katika riwaya hii.

4.14 Usimulizi mtuo

Usimulizi mtuo ni usimulizi unaotoa maelezo ya mandhari katika matini. Matendo yoyote ambayo hutokea katika kazi za kifasihi hufanyika mahali fulani na wakati fulani

kama anavyodokeza Wamitila (2002). Mandhari hutufichulia wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika. Katika ufafanuzi wake, Wamitila (2008) anaeleza kwamba mandhari huiathiri tabia za wahusika, uteuzi wa lugha na huweza kuhusishwa na matukio mbalimbali katika hadithi. Katika usimulizi huu hadithi huwa na wakati nunge kwa mfano mandhari ya shamba na ya mji:

Alishangaa kwa mara ngapi sijui, ni jinsi gani waungwana walivyostahabu kusongamana mjini, kwenye nyumba ndefu, kubwa na barabara nyembamba, ilhali huku mashambani watu walikuwa hawapambanii nafasi ya makao... wahamie mashambani. (Siri Sirini 1 2013:49-52)

Mwandishi anaeleza mandhari ya shamba na ya mjini kama alivyoyaona Mwanalemba. Mwanalemba alikuwa akipeleka ujumbe wa Mfalme Daudi Mringwari kwa Mwanaziza na Mwananinga kusini walikohamia baada ya Fumo Liyongo kutiwa ngomeni. Mwanalemba akiwa njiani, alifananisha maisha ya shamba na ya mjini. Mjini kulikuwa na msongamano, nyumba ndefu kubwa, barabara nyembamba, vichochoro vilivyokuwa na maji machafu, kinyesi cha punda, majirani wasiojuana na wanaokera. Shambani mlikuwa na hewa safi, ukosefu wa msongamano, uhuru, barabara pana, miti aina aina, matunda aina aina huku kufanya maisha kuwa rahisi. Mwanalemba aliyapendelea maisha ya shamba kuonyesha mgongano wa maisha ya shambani na maisha ya mjini. Alikuwa akimshawishi nduguye Mfalme Daudi Mringwari na mumewe Shahamey Makame kuhamia shamba bila mafanikio hivyo, Mwanalemba alipapenda shamba na wale waliokuwa ndani.

Mandhari ya bustani yamesimuliwa:

Bustani yenyewe ilikuwa na maajabu mengi. Jambo la kwanza, ilikuwa ina vivuta-nadhari kochokocho. Ilikuwa na maua ya aina aina tena ya kila rangi. Ndani ya bustani pia mlipatikana miti ya matunda waijuayo Washanga na mingi tu wasiojua. Miti hiyo ilikuwa imejaa matunda mabivu tayari kwa maandazi... Walikaribishwa katika sehemu ya bustani ambako jukwaa la aushi lilikuwa limejengwa. (Siri Sirini 1 2013:273-275)

Msimulizi anatoa maelezo ya bustani walikofanyia mkutano wa kwanza baina ya wajumbe wa Shanga na wenyeji wa taifa la Misri. Mkutano ulifanyika katika bustani kuu ya kifalme. Mapambo katika bustani yamesimuliwa kama vile: Miti iliyokuwa na maua ya kila rangi, aina nyingi za matunda, ndege wa kila aina na waliofurahisha kwa

nyimbo zao, mito iliyotiririka katika vinywa vya vichwa vya simba na sanamu za mafarao kama vile Malkia wa Hatsheput na Khalikzanda kuonyesha maendeleo nchini Misri. Hotuba ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume imeelezwa na jinsi alivyowatambulisha wenzake, masomo yake katika Zutafindaki ya Al-Azhar, maendeleo ya nchi ya Misri hasa katika taaluma ya maandishi, ustaarabu, unyunyizaji maji mashamba na dini thibitisho la maendeleo nchini Misri. Athari ya hotuba hiyo ilikuwa kubwa hivyo Mfawidhi Kijumwa Mfaume kushangiliwa na watu wote.

Kuna maelezo ya mandhari ya mahakama:

Sauti ilipasua, Mleteni mfungwa! Kutoka upande mwingine maneno haya yakasukumwa mbele na mkemo uliosikika kama mwengo: Mleteeni mfungwa! Mle ndani mlikuwa mmejaa watu wengi hata nafasi ya punje ya mchanga kudondoka kutoka juu haingeweza kupatikana...Mfungwa, umepatikana na makosa yote uliyoshtakiwa kwayo. Kwa ajili hiyo, mahakama imekupata na hatia. Hapa alipumua kidogo. Hukumu yako ni kuwa utafungwa maisha katika hali ya kinyama kabisa kwa vile wewe ulidhamiria kuleta unyama usiomithilika na maafa yasiyo kikomo nchini mwetu! (Siri Sirini 1 2013:1-8)

Usimuliaji wa muktadha huu unafahamisha msongamano katika mahakama wakati wa kutoa hukumu dhidi ya mfungwa, Fumo Liyongo. Ukatili unajitokeza Fumo Liyongo anapoitwa mfungwa kabla ya kuhukumiwa. Askari walimsukuma Fumo Liyongo huku upole wake ukidhihirika ijapokuwa alikuwa jitu. Fumo Liyongo alinyimwa nafasi ya kujitetea kwa makosa ya: Utovu wa uzalendo, uchochezi na uhaini. Ukatili wa hakimu unaonekana anapotafsiri shairi, ‘Takhmisa ya Liyongo’ visivyo. Fumo Liyongo alipatikana na makosa kwa mashtaka yote na kufungwa kifungo cha maisha katika hali ya kinyama kuthibitisha udhalimu katika uongozi wa Mfalme Daudi Mringwari.

Mandhari ya msimu wa masika yamesimuliwa na mwandishi. Msimulizi anajulisha kwamba mvua nyingi ilinyesha nchini Ozi baada ya Suleiman Mringwari kufaulu kumshawishi Fumo Liyongo kurudi Shanga. Usimulizi unaeleza kuwa mvua ilinyesha huku ikiwatesa wanadamu na mifugo waliokufa kwa wingi. Kukawa na magonjwa mengi, mito kufurika, nyumba na watu kusombwa na maji. Baada ya mvua kupungua Fumo Liyongo alipanga safari ya kurudi Shanga, akiandamana na mwanawe Mwinyi. Wakiwa safarini, Fumo Liyongo alimweleza Mwinyi kuhusu mazingira katika msitu.

Kwa hivyo, Mwinyi alielewa aina za miti, manufaa na hatari yake, aina za udongo na manufaa yake.

Mandhari ya sherehe ya arusi ya Mwanakupona yameelezwa hivi:

Baragumu zililia na Shanga nzima ikawaa! Walivyonena wavyele:
Mbiu ya mgambo ikilia ina jambo...Baadaye, hata hivyo, wengi walipata ujasiri, wakazitafuta njia za majumbani kwao halahala na kuzipata. (Siri Sirini 1 2013:188)

Msimulizi anaeleza matukio yalivyokuwa siku ya arusi ya Mwanakupona. Katika arusi, kulikuwepo na mpangilio mahsusi wa mambo kama vile: Milio ya ngoma kuashiria tukio fulani, taa zilizowaka maridhawa, mahema yaliyozagaa kote, mavazi ya waliohudhuria na burudani kuonyesha ufanisi wa arusi ya kifalme. Usimulizi unafahamisha kwamba wimbo wa mwisho katika arusi uliimbwa na Fumo Liyongo. Katika harakati za kuimba, Fumo Liyongo alivunja lango na kutorokea nchi ya Ozi kudhihirisha kushindwa kwa uongozi dhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari.

Kwa hivyo, usimulizi wa mtuo umeweza kutoa mwangaza kuhusu matukio mbalimbali yaliyosimuliwa katika hadithi na kuchangia katika mpangilio wa riwaya hii. Mandhari pia yameleta hisia fulani katika usomaji wa riwaya na usawiri wa wahusika.

4.15 Usimulizi wa idadimarudio

Usimulizi wa Idadimarudio hurejelea mara ambazo matukio hutokea katika hadithi na mara ngapi matukio hayo yanasimuliwa. Idadimarudio huhusisha urudiaji kwa kiasi fulani. Kulingana na Wamitila (2002), si lazima miundo ya sentensi na maneno yafanane tukio linaposimuliwa mara kadha kwa sababu muktadha au hata mahali tukio hilo linapotokea huwa tofauti. Riwaya ya *Dharau ya Ini* imesimuliwa kwa urudiaji huu (Wambui, 2018). Wana-Naratolojia wanabainisha aina tatu kuu za urudiaji wa tukio.

4.15.1 Usimulizi mosi

Katika usimulizi mosi tukio linaweza kutokea mara moja na kusimuliwa mara moja katika hadithi kama asemavyo msimulizi:

Akaweka sindano kwenye kitovu. Akaiziba kwa kiganja cha moto, kisha akasema: Tufanye sote wawili. (Siri Sirini 3 2014:221)

Muktadha huu unaonyesha jinsi mwanamfaume alivyomsaliti Fumo Liyongo na kumuua kikatili kwa kumdunga kitovuni kwa sindano ya shaba. Mwanamfaume alienda Ozi na kumshawishi Fumo Liyongo kurudi Shanga. Fumo Liyongo alimwambia mwanamfaume jinsi anavyoweza kuliua jitu na kumfichulia siri ya udhaifu wa kitovu. Mwanamfaume alitumia siri hii na kumuua Fumo Liyongo, tukio lililosababisha vita baina ya Waozi na Washanga huku Daudi Mringwari akipinduliwa. Tukio hili la kudunga limesimuliwa pale Osman Ali Kidhabi alimuua Suleiman Mringwari kwa kumdunga kwa mshale mgongoni katika bangu baina ya Waozi na Washanga:

Kufumba na kufumbua, Kidhabi akaonekana hapo hapo akiwa nyuma ya Suleiman Mringwari. Hima akachomoa mkuki na kushindilia mlengwa wake kwa nguvu zake zote! Mkuki ukaingia barabara mgongoni baina ya makombefua ya mhasiriwa!Ukapenya sawa sawa mpaka ukatokeza kidarini. (Siri Sirini 3 2014:279)

Msimulizi anafananua jinsi Osman Ali Kidhabi alivyomuua Suleiman Mringwari kwa kumdunga dhihirisho la ukatili wa Kidhabi. Wengine walioaga dunia vitani hivi alikuwa Waziri Mkuu na Mkuu wa Sheria. Mfalme Daudi Mringwari aliondolewa mamlakani na serikali mpya ya Shanga ikapewa Bauri wa Liyongo kuonyesha mabadiliko katika uongozi

Urudiaji mosi unajitokeza hapa:

Ushawahi kusoma hadithi ya Mfalme Anzuruni, mwanamize? (Siri Sirini 1 2013:59)

Mwanalemba aliulizwa na Mwanaziza kama aliwahi kusoma utungo wa ‘Siri Sirini’. Walikuwa shamba katika kasri la pili la Mfalme Daudi Mringwari ambapo Mwanalemba aliwapelekea ujumbe kutoka kwa Mfalme Daudi Mringwari. Mwanaziza alizungumzia udhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari na kumfananisha na Mfalme Anzuruni aliyehadithiwa katika shairi la ‘Siri Sirini’ kuonyesha uongozi dhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari. Tukio hili la kusoma hadithi ya Mfalme Anzuruni limesimuliwa pale mtunzi wa utungo wa ‘Siri Sirini’ alikuwa akitafutwa ili akamatwe.

Naam...kuhusu utungo huu wa ‘Siri Sirini’. Umewahi kuusoma? (Siri Sirini 2 2014:265)

Msimulizi alimuuliza Mwanalemba kwenye kikao kama alikuwa ameusoma utungo ambao mtunzi alikuwa akitafutwa aadhibiwe dhihirisho la unyanyasaji kwa kutumia

asasi za utawala. Mwanalemba alikubali kuusoma mara kadhaa na kupendekeza kufanywa kwa uchunguzi ili kuthibitisha au kukanusha ukweli wa yaliyoandikwa katika shairi hilo kuonyesha uaminifu na ujasiri wake.

Usimulizi mosi umetumiwa na mwandishi. Anasema hivi:

Mama alijikuta ameokota ufito, akamchapa kwa nguvu zake zote mwanawe kabla ya wenziwe kumzuia asifanye hivyo. Alipopata kipigo hicho Liyongo, ja gogo, fwaap, akagwa! (Siri Sirini 3 2014:235)

Fumo Liyongo aliaga dunia kisimani akiwa ameushika mshale tayari kuvuta kamba. Watu hawakujua alikuwa mfu. Wanawake walishindwa kuchota maji wakimwogopa. Mwanaziza na Mwananinga walimkariria mashairi na tenzi tumbuizi huku wakimsihi aondoke mahali hapo bila kufanikiwa thibitisho la mapenzi kwa jamaa yao. Mwishowe Mwanaziza alikasirika, akachukua ufito na kumchapa. Fumo Liyongo alianguka kama gogo kuonyesha ukatili wa uongozi. Kwa hivyo, Mwanaziza, Mwananinga na wote waliokuwepo walimlilia Fumo Liyongo. Tukio hili la kutumia ufito limerudiwa pale Mwanalemba alimuomba Mwanaziza kuchukua ufito na kuwacharaza. Anasema:

Samahani shangazi...! Kwa nini usichukue ufito na kutucharaza, sie wanao watovu wa adabu! (Siri Sirini 3 2014:323)

Abanoye alienda kwa Sheikh Majid Mngumi kuonana na jamaa zake. Mwananinga na Mwanalemba walimkumbatia na kumpiga pambaja na kumsahau Mwanaziza. Kuona hayo, Mwanalemba alimshauri Mwanaziza kutumia ufito na kuwacharaza kuonyesha mshikamano wa familia pana ya Fumo Liyongo. Kwa hivyo, walimuomba Mwanaziza msamaha na kuendelea na mazungumzo yao.

Usimulizi mosi mwingine ni:

Walipoonana, baada ya muda mrefu, watu wawili hao walijawa na furaha isiyo na kifani. (Siri Sirini 1 2013:130)

Mwandishi anajulisha kuwa Fumo Liyongo alifurahia kumwona Suleiman Mringwari baada ya kutengana kwa muda mrefu. Suleiman Mringwari alimtembelea Fumo Liyongo ngomeni na kumpelekea chakula. Fumo Liyongo alimuonya mwanamfaume dhidi ya kumpelekea chakula ngomeni kuonyesha mapenzi baina yao. Tukio hili limerudiwa na mwandishi. Anasema hivi:

Liyongo alifurahi zaidi ya ziada kumwona mwanawe mpendwa, mwana wa nduguye, baada ya kutenganishwa naye kwa muda mrefu kweli kweli. (Siri Sirini 3 2014:65)

Mwandishi anafahamisha kwamba Suleiman Mringwari alimtembelea Fumo Liyongo nchini Ozi tukio ambalo lilimfurahisha Fumo Liyongo thibitisho la mapenzi. Suleiman Mringwari alienda nchini Ozi kumshawishi Fumo Liyongo kurudi nchini Shanga na kuijenga kuonyesha ujanja kwa sababu usimulizi unaeleza kuwa lengo la kurudi Shanga lilikuwa aangamizwe.

Usimulizi mosi unadhihirika kama asemavyo msimulizi:

Hata kama ni pangoni! Ulikuwa hai, sio? Mbona hukujitayarisha vyema kwa utetezi? La hasha! Mfungwa sinene! (Siri Sirini 1 2013:7)

Hakimu alimnyima Fumo Liyongo nafasi ya kujitetea mahakamani nchini Shanga alikoitwa mfungwa kabla ya kuhukumiwa dhihirisho la ukatili katika asasi za uongozi. Fumo Liyongo alihukumiwa kifungo cha maisha katika hali ya kinyama. Tukio lingine la Fumo Liyongo kujitetea mahakamani ni:

Baada ya kupelekwa mahakamani na kujitetea vyema, alisamehewa makosa mawili aliyokuwa ameshtakiwa kwayo: kosa la ujasusi na la uvamizi wa nchi akitumia silaha hatari. Siri Sirini 1 (2013:322)

Mwandishi anaeleza kwamba Fumo Liyongo alijitetea katika mahakama ya Ozi na kusamehewa kwa makosa yote mawili kuonyesha utu wa washika dau katika mahakama ya Ozi. Tukio hili lilimfungulia Fumo Liyongo ukurasa mpya katika nchi ya Ozi. Fumo Liyongo alipewa cheo cha Jemadari wa majeshi yote ya Ozi na kuamua kujenga nchi ya Ozi kama alivyoijenga nchi ya Shanga dhihirisho la ushujaa wa kimwili, kiakili na mshikamano. Aidha, mudir wa Ozi, Omar Soba alimpa makao katika boma lake hivyo kumuoa bintiye mudir, Abanoye.

Uchunguzi umebainisha kuwa tukio linaweza kutokea mara moja katika hadithi na kusimuliwa mara moja katika simulizi kama inavyodhihirika na mifano iliyo hapo juu.

4.15.2 Usimulizi rudufu

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) huu ni usimulizi ambapo tukio linaweza kufanyika mara moja na likasimuliwa mara kadhaa katika usimulizi. Tukio linaposimuliwa zaidi ya mara moja si lazima miundo ya kileksia na kisintaksia ifanane. Sentensi na maneno yanaweza kubadilika kwa sababu tukio linaporudiwa huwa linarudiwa katika muktadha tofauti (Wambui, 2018). Mfano huu unaonekana pale mikutano ilifanyika kwenye mnazi uliopiga goti. Suala la mnazi kupiga goti limesimuliwa mara kadha katika usimulizi wa hadithi hii. Msimulizi anasema:

Mahali penyewe palikuwa na mnazi ulioanguka ulipokuwa mkinda, lakini haukudhoofu, bali ulikulia chini kwa chini, sambamba na ardhi. (Siri Sirini 1 2013:99)

Msimulizi anaeleza ya kwamba Mwanalemba na Mfawidhi Kijumwa Mfaume walikutana hapa mnazini na kufanya mazungumzo yaliyohusu kuchunguzwa kwa Mfalme Daudi Mringwari. Osman Ali Kidhabi aliwaona na kumdanganya Mfalme Daudi Mringwari jinsi alivyowafumania kwenye mnazi uliopiga goti katika hali ya mahaba. Anasema:

Huko ufukoni, mbali huko, kuna mnazi ulioanguka zamani lakini haukufa ulikua hivyo hivyo chini kwa chini kama mtambazi, kisha ukapiga goti, ukainuka. (Siri Sirini 1 2013:112)

Osman Ali Kidhabi anamsimulia Mfalme Daudi Mringwari jinsi alivyowakuta Mwanalemba na Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Mfalme Daudi Mringwari alikataa kuamini huo uwongo kuhusu Mwanalemba kuonyesha chuki aliyokuwa nayo Osman Ali Kidhabi kwa Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Kibwana Mwengo Bashee na wafuasi wake walifanya mikutano yao kwenye mnazi uliopiga goti. Mwandishi anasema:

Kwa hivyo kule kufika pale penye mnazi uliopiga goti kisha ukainuka, mapema kuliko mtu mwingine yeyote. (Siri Sirini 1 2013:385)

Mwandishi anatoa maelezo kwamba Shalo alifika mahali pa mkutano na kuwasubiri wenzake iwadhahirikie kwamba alikuwa pamoja nao katika harakati za ukombozi thibitisho la udanganyifu. Osman Ali Kidhabi aliwaambia Waziri Mkuu na Malkia Mwanalibasi jinsi aliwafumania Mfawidhi Kijumwa Mfaume na Mwanalemba penye mnazi uliopiga goti. Osman Ali Kidhabi anasema:

Hapo hapo nilipowafumania mara ya kwanza... hapo penye mnazi uliopiga goti! (Siri Sirini 2 2014:44)

Kibwana Mwengo Bashee anajulisha alipowakuta wawili hao wakizungumza kwa sauti ya chini kuonyesha walikuwa wakipanga mipango hatari dhidi ya uongozi wa Mfalme Daudi Mringwari. Vilevile, bwana aliyemwita Mfawidhi Kijumwa Mfaume kutoka kwake nyumbani usiku wa manane alimwongoza kwenye mnazi uliopiga goti:

Yule bwana aliongozwa mpaka akafikishwa pale wanapokutania kila mara wakiwa na haja ya kukutana. (Siri Sirini 2 2014:48)

Msimulizi anafahamisha alikopelekwa bwana aliyekuwa akiteswa. Bwana yule aliulizwa kukimbia, akafyatuka kama mshale kuelekea kwenye mnazi uliopiga goti kuonyesha ukatili:

Bwana huyo akafyatuka kama mshale kuelekea kwenye mnazi uliopiga goti. (Siri Sirini 2 2014:53)

Mwandishi aeleza jinsi bwana huyo alivyokimbia kwa kasi na kuelekea mahali walikozoea kufanyia mikutano. Kombo alisema kuwa Mfawidhi Kijumwa Mfaume alibururwa na watu wengi kudhihirisha ukatili wa waliomburura na aliyemuita nyumbani kwake usiku wa manane. Waliminyana naye huko mnazini. Kibwana Mwengo Bashee na wafuasi wake walienda kwenye mnazi wao kama kawaida yao.

Mfano mwingine wa usimulizi rudufu unajitokeza hivi:

Nilipokuwa Lamu, kulianguka kondo kali ya mbari, na kaka zangu wote wanne wakaangamizwa. (Siri Sirini 1 2013:375)

Abanoye alimweleza Fumo Liyongo kwamba alikuwa Lamu kwa muda wa miaka miwili akisoma madrassa. Abanoye alirudi nyumbani na kupata kaka zake wanne waliuliwa katika vita vya mbari kuonyesha migogoro ya mbari. Abanoye alitoa maelezo haya siku ya arusi yake kwa Fumo Liyongo kuibusha hisia za huruma. Tukio la masomo kufanyiwa Lamu linasimuliwa kuhusu watoto wanne wa Mwanalemba ambapo mwandishi anasema:

Pia, aliweza kuichukua fursa hiyo kuwajulia hali watoto wanne wa wafi yake, Mwanalemba, ambao walikuwa huko huko Lamu walikosoma chuo kimoja na hao wanawe. (Siri Sirini 1 2013:139)

Mwandishi anafahamisha kuwa watoto wa Mwanalemba walisomea Lamu walikosomea watoto wa Fumo Liyongo, Bauri na Mwanakupona kudhihirisha umuhimu wa masomo. Mwingine aliyesomea Lamu alikuwa Osman Ali Kidhabi:

Kidhabi alipelekwa kusoma, umri ulipotimu. Akaenda Lamu, na baadaye akaenda kote Uswahilini. (Siri Sirini 2 2014:12)

Fumo Liyongo alisimulia juu ya malezi ya Osman Ali Kidhabi, masomo na matembezi kuonyesha uhusiano wa Osman Ali Kidhabi na ukoo wa kifalme. Kidhabi alisafiri kote huko na baadaye akaenda kote Uswahilini alikojifunza mambo mengi kuhusu uchawi thibitisho la Osman Ali Kidhabi kuitwa mwanga.

Usimulizi rudufu unadhihirika katika maelezo haya:

Wekeni kichwa peke yake..kichwa pekee katika mdomo wa tanu.
Mwili waachieni wazee! (Siri Sirini 2 2014:54)

Msimulizi anasimulia maelezo aliotoa kuhusu mtu aliyeuawa na kukatwa kichwa. Kichwa kikawa kimetenganishwa na mwili kuonyesha unyama wa wauaji. Mtu aliyeuawa alikuwa Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Tukio hili lilifanyika baada ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume kuitwa nyumbani kwake na kutoka kabla ya kumuaga mkewe. Baada ya kumuua, walikata kichwa na kukiweka kwenye tanuri na mwili wakaachia fisi. Tukio la kuuliwa kwa kukatwa kichwa linasimuliwa hivi:

Jitu hilo la miraba minne lilimlenga shingo mfungwa kwa upande wa mgongoni na kumkata kichwa dharuba moja! Kwa dharuba moja tu, kichwa kikawa kwake na mwili kwake! (Siri Sirini 3 2014:267)

Shalo aliuliwa kwa kukatwa kichwa alipopatikana na kosa la uhaini. Shalo na Osman Ali Kidhabi walikuwa wamefungiwa ngomeni kwa mauaji ya Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Osman Ali Kidhabi alijitetea na kuachiliwa kuonyesha ufidadi katika asasi za utawala. Baada ya kifo cha Fumo Liyongo, Shalo alipelekwa barazani ambapo Osman Ali Kidhabi alitangaza kuwepo kwa jambazi lililotoroka ngomeni pamoja na Fumo Liyongo. Waziri wa Sheria alitangaza hukumu yake kuwa kifo. Askari walimuua Shalo kwa kumkata kichwa dharuba moja dhahirisho la ukatili wa askari. Mtu mwingine aliyekata kichwa alikuwa Waziri Mkuu kama yanaposimuliwa:

Dharuba moja tu, kichwa kikaangukia kwake na mwili kwake!
Viungo hivyo vikapapatika hadi vikaishia na nishati. (Siri Sirini 3 2014:280)

Kauli ya msimulizi inaeleza kwamba katika vita baina ya Waozi na Washanga Waziri Mkuu alilengwa na upanga, kichwa kikaangukia kwake na mwili kwake. Vita hivi

viliuporomosha uongozi wa Daudi Mringwari. Shanga ikapata kiongozi mpya kuonyesha ujenzi wa jamii.

Kuna usimulizi rudufu wa kupiga magoti kama inavyosimuliwa hapa:

Alikamatwa na vijana shababi wapiganaji hodari wa huko, nusura wamwue, lakini akawapigia magoti na kuwaomba wasimwue. (Siri Sirini 1 2013:383)

Msimulizi anamwambia Malkia Mwanalibasi kwamba Fumo Liyongo aliwapigia magoti wapiganaji wa Ozi ili wasimwue baada ya kutorokea huko kuonyesha udanganyifu kwa sababu Fumo Liyongo hakuwapigia magoti bali alipigana nao dhihirisho la ushujaa wa vita. Wapiganaji walimwongoza Fumo Liyongo hadi kwa mudir wao. Fumo Liyongo alipelekwa mahakamani nchini Ozi alikojitetea na kusamehewa kwa makosa yote. Mudir alimpigania Fumo Liyongo akapewa cheo cha jemadari wa majeshi yote ya Ozi. Osman Ali Kidhabi alimpigia Fumo Liyongo magoti:

Alipiga magoti na kulia machozi njia mbili mbili huku akiomba anusurishwe. (Siri Sirini 2 2014:22)

Osman Ali Kidhabi alienda Ozi kumuua Fumo Liyongo. Osman Ali Kidhabi alitumia kikoa cha makoma kumwamamiza lakini Fumo Liyongo alimwelewa na kupendekeza kwamba zamu yake iwe ya mwisho. Ombi lake lilikubaliwa na wenzake. Zamu ya Fumo Liyongo ilipofika, alibwaga makoma kwa kutumia mshale kuonyesha akili. Baada ya wapiganaji kuondoka, Fumo Liyongo alikuwa tayari kumuua Osman Ali Kidhabi. Fumo Liyongo alivuta kamba amuuu lakini Osman Ali Kidhabi alipiga magoti na kumuomba msamaha. Fumo Liyongo alimwachilia baada ya Osman Ali Kidhabi kumwambia aliyekuwa amemtuma Ozi kumuua. Tukio la kupiga magoti linatokea kisimani:

Akaharakisha kwenye mti wenye panda chini kabisa kooni. Akapiga magoti. Akaiimarisha mikono yake kwenye panda za mti huo, visugudi vyake vikiwa nanga. (Siri Sirini 3 2014:223)

Msimulizi anasema kuwa Fumo Liyongo alidungwa sindano ya shaba kitovuni akiwa amelala na mwanamfaume. Maumivu makali yalimshtua usingizini na kumsimamisha. Alichukua mshale wake na kulenga huku amepiga magoti dhihirisho la ujasiri. Fumo Liyongo aliaga dunia huku akijitayarisha kuvuta kamba. Fumo Liyongo na Mwanananga walipiga magoti huku wakikumbatiana alipowasili Shanga:

Wakakutana kwa kishindo kama kondoo wawili wanaopambana.
Wakakumbatiana. Wakapiga magoti na kuzidi kukumbatiana. (Siri
Sirini 3 2014:170)

Msimulizi anafafanua kuwa Fumo Liyongo alirudi Shanga na kuonana na Mwanaziza.
Mwanaziza alimkimbilia mwanawe kuonyesha mapenzi. Wote wawili walishindwa
kuzibana hisia zao hivyo kutokwa na michirizi ya machozi thibitisho la mapenzi.

Usimulizi rudufu mwingine ni wa kutokwa na machozi:

Sasa yeye akawa mara yuacheka, mara yualia alipokuwa akiutunga
utendi wake. Akawa yuacheka huku akilia! (Siri Sirini 1 2013:360)

Mwanakupona alitaka kuchangia katika ufanisi wa arusi yake. Alitunga utenzi akiwa
anacheka, mara yualia kwa kuchelea kuwa yaweza kumfika aliyoyaandikia
kudhihirisha umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike. ‘Utenzi wa Mwanakupona’
ulitumiwa kufunza madrassa yote ya Shanga thibitisho la mchango wa Mwanakupona
katika jamii ya Shanga. Wafanyikazi katika kasri la pili walimkumbatia Mwanalemba
huku wakilengwalengwa na machozi:

Iipotimu zamu yao, na wao nao wakamkumbatia mgeni wao huku
wakilengwalengwa na machozi. (Siri Sirini 1 2013:53)

Msimulizi anasema kuwa Mwanalemba alikaribishwa kwa heshima huku
waliomkaribisha wakilengwalengwa na machozi kuonyesha mapenzi kwa jamaa yao.
Tukio hili lilitokea wakati Mwanalemba aliwapelekea Mwanaziza na Mwanananga
ujumbe kutoka kwa Mfalme Daudi Mringwari dhahirisho la ushirikiano katika familia.
Walizungumza kuhusu udhalimu wa Mfalme Daudi Mringwari na kumfananisha na
Mfalme Anzuruni anayesimuliwa katika hadithi ya ‘Siri Sirini’. Tukio la kutokwa na
machozi lilitokea kwa Mwanananga:

Sasa machozi yalimtiririka Mwanananga kama vijito viwili
viendavyo kasi sana. Kuona hivyo, Liyongo naye machozi
yakamlengalenga, lakini yakabakia mwao mabwawani. (Siri Sirini
1 2013:339)

Kauli hii ya msimulizi inajulisha kuwa Mwanananga alitokwa na machozi. Tukio
lilitokea wakati Fumo Liyongo alimwambia Mwanananga lengo lake la kumuoa mke
wa pili, Abanoye, kudhihirisha usaliti katika ndoa. Fumo Liyongo alikuwa ametorokea
nchini Ozi na kupewa makazi na babake Abanoye, Sheikh Omar Soba. Mwanananga

alimkubalia Fumo Liyongo kumuoa Abanoye lakini kwa masharti kuonyesha imani katika dini. Abanoye alitokwa na machozi:

Na kwa mara nyingine, akaponyokwa na mpukutiko wa machozi yaliyopukutika pukupuku, kupukupu? (Siri Sirini 3 2014:113)

Suala la Abanoye kutokwa na machozi lilitokea Fumo Liyongo alipoamua kurudi Shanga baada ya kushawishiwa na mwanamfaume. Abanoye alihisi hangeonana tena na Fumo Liyongo kudhihirisha mapenzi. Kwa kweli hawakuonana tena kwa sababu mwanamfaume alimuua Fumo Liyongo huko Shanga kwa kumdunga kitovuni kwa sindano ya shaba kuonyesha usaliti na ukatili wa mwanamfaume. Mwanaziza alitiririkwa na machozi:

Mwanaziza, kimya kimya, akalia. Akatiririkwa na Machoziya raha, furaha na buraha pamwe na hamu na ghamu. (Siri Sirini 3 2014:172)

Mwanaziza alilia machozi ya furaha Fumo Liyongo aliporudi Shanga kuonyesha mapenzi ya mama. Tukio hili lilitokea baada ya Fumo Liyongo kurudi Shanga. Mwanaziza alimuuliza mwanawe kupanga mipango yake kwa uangalifu dhihirisho la ushauri kutoka kwa mama. Fumo Liyongo hakufuata ushauri wa mamake na mwanamfaume alimuua kwa kumdunga kitovuni kusababisha Mwanaziza kupasua kilio kikali.

Utafiti ulithibitisha kuwa matukio yanapotokea zaidi ya mara moja si lazima maneno yaliyotumika katika mazingira ya awali yafanane na matukio ya baadaye.

4.15.3 Usimulizi banifu

Usimulizi bainifu ni kigezo cha idadimarudio kinachoonyesha kuwa tukio linaweza kutokea mara kadha na kusimuliwa mara moja kama anavyodokeza (Wamitila, 2002). Tukio linalosimuliwa huwa limefanyika mara nyingi kisha kusimuliwa mara moja tu. Mwanalemba anasimulia vile alimshawishi kakake, Mfalme Daudi Mringwari na mumewe kuhamia shamba mara kadha wa kadha bila mafanikio. Mwanalemba anasema kuwa:

Hapo ni kabla hajaolewa. Alipoolewa, aliendelea na mradi wake huo huo wa kung'ang'aniakuhamia shamba, mara hii akijaribu kumshawishi mwanamume wa tatu kuwahi kuwa kiongozi wa nyumba yao katika maisha yake; yaani mumewe. (Siri Sirini 1 2013:52)

Usimuliaji huu unaonyesha kwamba haikuwa mara ya kwanza kwa Mwanalemba kufanya huo ushawishi. Kitendo hiki kilitendeka wakati Mwanalemba alikuwa akienda shamba katika kasri ya pili ya Mfalme Daudi Mringwari alikotumwa na Mfalme Daudi Mringwari na ujumbe kwa Mwanaziza na Mwanananga kuonyesha utiifu wake kwa kakake. Huku akitembea macho yake yaliangaza kila upande na kufurahia uzuri wa shamba, kama ilivyokuwa kawaida yake. Alishangaa kwa vile alimshawishi kakake kabla ya kuolewa na mumewe kuhamia shamba kulikokuwa na hewa safi bila mafanikio dhihirisho la mgongano wa shamba na mji.

Mfano mwingine wa usimulizi banifu ni:

Naja hapa, nakuta hakuna anayetubiri japo umenihakikishia, tena si mara moja, kwamba wenzako tayari wako hapa wakitungojea, kwa hivyo nichapuke tusichelewe! (Siri Sirini 2 2014:48)

Msimulizi anasema jinsi alivyohakikishiwa mara nyingi kwamba wenzake walikuwa wakiwangoja kuonyesha alihakikishiwa mara nyingi lakini usimulizi umesimulia mara moja. Kuna mtu aliyemwita huyo bwana kutoka nyumbani kwake usiku wa manane kudhibitisha ukatili. Bwana huyo alitoka kwa haraka bila kumuaga mkewe. Mtu huyo alimwuliza kuwa na subira huku akiwaita wenzake kwa kupiga kivoli, wakamchapa na kumuua.

Usimulizi banifu unajitokeza:

Mwana hutazama kishogo cha mvyelewe.... Si ndivyo ulivyotwambia baba... mara nyingi tena? (Siri Sirini 3 2014:167)

Mwinyi anamwambia Fumo Liyongo kuwa aliwafunza mara nyingi kwamba mtoto hutazama kishogo cha mvyele wake. Maneno ya Mwinyi yanafahamisha kwamba babake alikuwa amewafunza mara nyingi ila usimulizi umesimulia mara moja. Fumo Liyongo walifanya mazungumzo na Mwinyi wakiwa safarini kurudi Shanga. Mazungumzo hayo yalimfurahisha Fumo Liyongo kwa vile aliona Mwinyi alikuwa amekua tangu waanze safari.

Usimulizi banifu mwingine ni pale usimuliaji unasema kuwa Khalikzanda alihama mji kwa mara ya pili:

Khalikzanda alihama mji kwa mara ya pili. Siku chache baadaye, Mfalme Filipino wa Pili akauawa. (Siri Sirini 1 2013:309)

Msimulizi anaeleza kuwa Khalikzanda alihama kwao kwa mara ya pili kuonyesha kwamba alikuwa amehama tena hapo awali lakini tukio hilo halikusimuliwa. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alimsimulia mwanamfaume tukio hili walipokuwa nchini Misri. Siku moja wajumbe hawa walitembezwa jijini Khalikzandria. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alimsimulia mwanamfaume kuhusu Mfalme Filipino wa Pili na mwanawe Khalikzanda thibitisho la migogoro ya kifamilia.

Usimulizi banifu unaonekana katika kifungu hiki:

Naam, nakiri... Mara ya mwisho tulipopambana, bibi huyo alitangazwa mshindi... nikaadhirika, tena nikaathirika vibaya sana; nikufiche nini wifii? (Siri Sirini 1 2013:148)

Kitendo cha Malkia Mwanalibasi kuathirika kinasimulia kuwa mara ya mwisho alipopambana na Mwanananga katika sanaa ya uimbaji, Mwanananga alitangazwa mshindi kuonyesha Mwanananga alikuwa amemshinda mara nyingine. Tukio hili lilitokea wakati mipango ya arusi ya Mwanakupona ilikuwa ikiendelea. Malkia Mwanalibasi alikuwa akitunga wimbo ambao angeughani katika arusi ya Mwanakupona kuonyesha mshikamano katika familia. Mwanalibasi alinuia kumshinda Mwanananga katika uimbaji. Mwanalemba alimuuliza kuacha kisasi cha kisanaa.

Usimulizi banifu umeonyesha kwamba msimulizi anaweza kusimulia matukio mara moja ilhali matukio haya yalitokea mara nyingi. Badala ya kusimulia kila tukio msimulizi anaingiza kisa fulani kwa njia inayomfanya msomaji aelewe kuwa matukio hayo yalifanyika baada ya muda au siku baada ya siku. Usimulizi wa idadimarudio umefanikisha uelewaji wa riwaya hii kwa: Kusisitiza au kuyaweka mambo fulani wazi, kuwajua wahusika kutokana na sifa fulani ambazo zimerudiwa na kuviunga vipengele muhimu vya msuko.

4.16 Hitimisho

Uchunguzi umebaini kuwa riwaya trilojia ya *Siri Sirini* imetumia mbinu mbalimbali za kiusimulizi. Mbinu hizi ni kama vile: Usimulizi wa hotuba, usimulizi wa ki-itimamu, usimulizi penyezi, usimulizi tautolojia, usimulizi wa motifu ya safari, usimulizi wa

nyimbo, usimulizi kirejeshi, usimulizi elekezi, usimulizi muhtasari, usimulizi udondoshi, usimulizi onyesho, usimulizi uendelezaji, usimulizi mtuo na usimulizi wa idadimarudio.

SURA YA TANO

WAHUSIKA KATIKA RIWAYA TRILOJIA YA *SIRI SIRINI*

5.1 Dhana ya uhusika

Wahusika ni sehemu muhimu ya fani. Ni mojawapo wa misingi mikuu ya hadithi kwa sababu matendo na matukio yaliyomo katika hadithi hayawezi kuwepo bila ya wahusika (Wamitila, 2008). Wahusika ni watu, wanyama au vitu katika fasihi (Msokile, 1993). Msokile anafafanua kuwa wahusika wanasawiriwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Mwandishi huwasawiri wahusika kwa wasomaji wake kwa kutumia sifa walizonazo, jinsi walivyo, mambo wayapendao na wasiyoyapenda. Mohamed (1995) anawaeleza wahusika kama viumbe vya mawazoni vinavyoumbwa na mwandishi na kuibuka katika kazi yake ya fasihi. Anafafanua kwamba wahusika huhusika katika matendo na matukio kadha katika kazi husika. Anawaeleza wahusika kama viumbe vilivyochotwa katika maisha na huweza kuwa vivuli vya mawazoni ambavyo havina mshabaha sana na maisha halisi duniani.

Wahusika ni sehemu ya fani kama wanavyoeleza Njogu na Chimerah (1999). Wanafafanua kuwa wahusika ni viumbe vya sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kitamaduni na kisiasa. Wahusika aidha wanajadiliwa kwa namna wanavyoingiliana na maudhui. Hili hujitokeza kutokana na maneno, tabia na matendo yao. Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hawa huwa ni sehemu ya kazi nzima. Viumbe hawa huwa binadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema, wanayoyatenda na maelezo ya mhusika au msimulizi (Wamitila, 2002).

Wamitila (2008) anafafanua kuwa wahusika ni nyenzo kuu katika fasihi kwa sababu ndiyo jira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi husika. Mtazamo wa dhana ya wahusika hutofautiana kutegemea mkabala anaochukua mtafiti na nadharia ya fasihi inayohusika. Anaeleza kuwa mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni, ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za binadamu. Anaeleza kuwa mwelekeo wa

kuwahusisha wahusika wa fasihi na binadamu wanaopatikana katika hali halisi huathiri kwa kiasi fulani matarajio ya usawiri wa uhusika.

5.2 Uainishaji wa wahusika

Wahusika wanaopatikana katika riwaya ni wa aina mbalimbali. Wahusika hao hutofautiana kutokana na nafasi zao katika hadithi. Kunazo njia nyingi za kuainisha wahusika katika riwaya. Wahusika wana sifa zinazofungamana na majukumu mbalimbali. Kazi hii ilishughulikia njia mbalimbali za uainishaji, kisha kuchagua njia mwafaka ya kuainisha wahusika katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

Njogu na Chimerah (1999) wamewaweka wahusika katika kigezo cha sifa na nafasi. Katika kigezo cha sifa, wametambua wahusika wa miraba minne na wahusika wa mraba mmoja. Wahusika wa miraba minne wana sifa nyingi nzuri na mbaya. Maisha ya wahusika hawa yana tajriba na matukio mengi. Katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini* wahusika hawa ni kama vile: Mfalme Daudi Mringwari, Malkia Mwanalibasi na Suleiman Mringwari. Wahusika wa mraba mmoja wana sifa moja tu. Hawabadiliki kama vile Osman Ali Kidhabi. Katika kigezo cha nafasi (mtaje) wametambua wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Wahusika wakuu huchukua nafasi kuu katika kazi ya kifasihi. Wanatawala hadithi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Migogoro ya hadithi nzima inawahusu. Wahusika wasaidizi huhusiana kwa karibu sana na wahusika wakuu. Mwandishi huwatumia kumfafanua zaidi mhusika mkuu. Sifa za mhusika mkuu hubainishwa wazi kupitia maingiliano baina yake na wahusika wasaidizi. Wahusika wajenzi huwajenga wahusika wakuu na wahusika wasaidizi hivyo kukamilisha dhamira na usimulizi wa riwaya.

Naye (Madumulla, 2009) amewagawa wahusika katika makundi matano: Mhusika mkwezwa, mhusika wa kimapinduzi, mhusika jumui, mhusika wa kisaikolojia na mhusika wa kidhanaishi. Hiki ndicho kigezo ambacho kilitumika kuainisha wahusika katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*.

5.2.1 Mhusika mkwezwa

Kulingana na Wamitila (2008) mhusika mkwezwa ni mhusika anayepewa sifa fulani zinazomkweza juu ya wahusika wengine. Mhusika huyu anapewa akili yenye uwezo wa kutambua mambo ambayo wahusika wengine wanashindwa kuyatambua mfano wa

Karama, mshtakiwa aliyejitetea bila kutetemeka katika riwaya ya *Kusadikika*. Madumulla (2009) amemfafanua mhusika mkwezwa kwa kusema kwamba: Ana nguvu za ajabu, mjasiri, mwadilifu, mpole, matendo makubwa, lugha teule na mwenye akili nyingi kama vile:

5.2.1.1 Fumo Liyongo

Fumo Liyongo amekwezwa katika riwaya hii kwa ujasiri wake kama jemadari aliyepigania nchi yake kama anavyodokeza Mwanalemba:

Mna mtu mwenye bidii kazini kama yeye? Mna mtu anayestahiki sifa kwa kulifanya taifa litambulike kisawasawa Uswahilini kote na dunia nzima, kwa mapana na urefu wake, kama Fumoloti? (Siri Sirini 1 2013: 22)

Msimulizi anaeleza kuwa Fumo Liyongo ndiye mtu pekee aliyestahili sifa kwa kulifanya taifa la Shanga kutambulika Uswahilini na duniani. Fumo Liyongo ana bidii katika kazi, hakuogopa mbele ya maadui zake na alikuwa tayari kukabiliana nao kwa ushupavu kama inavyodhihirika alipopambana na wapiganaji wa Ozi. Anaeleza hivi:

Kuona hivyo Fumo Liyongo akatoka mbio mbio, Upinde mkono wa kushoto, fumo mkono wa kulia, mfuko ubavuni, podo mgongoni, kombeo amevalia shingoni mileli ikining'nia kifuani upande huu na huu (Siri Sirini 1 2013:268)

Mwandishi anajulisha jinsi Fumo Liyongo alivyojitayarisha kukaribiana na wapiganaji wa Ozi waliomvamia kibandani kuonyesha ushujaa katika vita. Usimulizi unaeleza kwamba Fumo Liyongo alipigana na wapiganaji wa Ozi mpaka pale aliamua kukomesha vita. Kwa hivyo, Fumo Liyongo aliteremsha silaha zake chini na kuwaruhusu wapiganaji kumwongoza walikokusudia dhihirisho la ushujaa wa akili.

Kilikuwa kitendo cha ujasiri Fumo Liyongo kutoroka ngomeni. Kibwana Mwengo Bashee na wenziwe walisherehekea tendo hili la Fumo Liyongo kukata minyororo, kuvunja lango la ngome na kujinyakulia uhuru wake binafsi. Mwandishi anasema:

Likasikika sauti kali la lango likigongwa dharuba moja la nguvu ajabu! Kufumba na kufumbua, lango likaanguka chini kwa mbele, karibu kumwangukia Mwanananga (Siri Sirini 1 2013:201)

Kauli hii inaeleza kwamba Fumo Liyongo alivunja lango la ngome na kuanguka chini. Ilikuwa siku ya arusi ya Mwanakupona ambayo Fumo Liyongo alijinyakulia uhuru

dhihirisho la ujasiri. Wafuasi wa Fumo Liyongo walikubaliana kwamba ilihitaji mtu mwenye usikawaida wa hali ya juu zaidi kuweza kufanikiwa kufanya kitendo hicho. Kibwana Mwengo Bashee na wafuasi wake wanasema kuwa tendo hilo la kijasiri lilingisha utawala dhalimu. Kitendo kingine cha ujasiri kinaonekana katika kifungu hiki:

Juu ya ulili, mtoto mgonjwa alikuwa amelala, akipumua mpwekompweko, kiwele kabisa. Iitaka moyo mgumu kuondoka na kumwacha nyuma katika hali hiyo, lakini Liyongo ni nani? (Siri Sirini 3 2014:108)

Mize, bintiye Fumo Liyongo alikuwa mgonjwa lakini Fumo Liyongo alipofunga safari ya kurudi Shanga akamwacha na mamake, tendo la ujasiri. Msimulizi anaeleza kuwa mtu aliye na moyo mgumu ndiye angetenda kitendo kama hicho. Ujasiri wa Fumo Liyongo unadhihirika alipovuka mto uliokuwa umefurika kwa kupambana na nguvu za maumbile. Katika safari, Fumo Liyongo alipambana na chatu na wanyama hatari kama simba, nyati na ndovu.

Fumo Liyongo ana uwezo mkubwa wa kimwili na nguvu nyingi. Katika safari yake ya kurudi Shanga, Fumo Liyongo alibeba vitu vingi kama vile: Silaha ja vile panda ya manati, teo, kifurushi cha mawe na vyakula. Mwanawe Mwinyi alipolemewa na safari, Fumo Liyongo alikusanya vitu vyote alivyokuwa amempagaza Mwinyi na kuzibeba yeye kama anavyosimulia msimulizi:

Alikusanya vitu vyote alivyokuwa amempagaza mtoto, vyote akavifungasha katika furushi moja, akajiongezea mwenyewe mzigo. (Siri Sirini 3 2014:116)

Msimulizi anafahamisha kwamba alibeba mizigo yote kumwezesha Mwinyi kutembea kwa haraka kuonyesha nguvu za mwili. Fumo Liyongo hali kadhalika alitumia nguvu za mwili kumkatakata chatu na kukikanganua kichwa kilichokuwa kimemuuma mguu.

Usimulizi unaarifu kuwa Fumo Liyongo alikuwa na nguvu za akili. Nguvu za akili zinajitokeza pale Fumo Liyongo alielewa ujanja wa Osman Ali Kidhabi. Msimulizi anasema:

Kikoa kikaendelea basi, tena bila matatizo yoyote wala kiunzi njiani. Ingawa hivyo, Liyongo aliona pana jambo halikukaa vizuri hapo. Tuhuma ikaujaa moyo wake na kumpandishia taharuki. (Siri Sirini 2 2014:21)

Osman Ali Kidhabi alifanya njama ya kumuua Fumo Liyongo kwa hila akitumia mchezo wa kioa. Osman Ali Kidhabi alikuwa ametumwa nchini Ozi kutekeleza wajibu huo na Malkia Mwanalibasi. Osman Ali Kidhabi alishirikiana na wapiganaji wa Ozi katika njama ya kula kioa kuonyesha ujanja wa Osman Ali Kidhabi. Kila mmoja wa wapiganaji alipanda juu ya mkoma na kuangusha makoma. Walikuwa na siri kuwa Fumo Liyongo apandapo mkoma, wamfume mishale na kumwanganiza. Fumo Liyongo alibaini njama yao na badala ya kupanda mkoma, aliangusha makoma kwa kutumia mishale thibitisho la nguvu za akili hivyo kutofaulu kwa njama ya Osman Ali Kidhabi.

Akili ya Fumo Liyongo ilimsaidia kutoroka ngomeni na kujinyakulia uhuru. Fumo Liyongo alitumia ushairi kumtuma Kijakazi Sada aliyempelekea chakula na ujumbe. Askari-ngome alimpokonya Kijakazi Sada chakula na waraka. Kijakazi Sada alimuomba Fumo Liyongo msamaha kwa sababu askari-ngome alimpokonya chakula na 'Utendi wa Mwanakupona'. Fumo Liyongo aliwaza na kumtuma Kijakazi Sada kwa mamake akiomba tupa ikiwa imewekwa ndani ya mkate wa wishwa. Fumo Liyongo angetumia tupa kukata minyororo na kutorokea msituni. Fumo Liyongo alimfundisha Sada wimbo na alipoona askari-ngome akiwatupia jicho la upekuzi mara kwa mara, alimwambia Sada acheze. Wimbo aliomfunza ni huu :

Kijakazi Saada nakutuma tumwa tumika
Kamwambie mama yu muinga hajalimuka
Afanye mkate kati tupa kuweka
Nikereze pingu minyo'o ikinyemuka
Niparage kuta na madari kiyakeuka
Niuwe rijali pindi wakiwana kuteka
Ningie ondoni ninyepepe ja mwana nyoka
Ningie mwituni ningurume ja simba buka
Nali mtu pweke nimeziye katika nyika
Si nduu si mbasi nimeziye kukupuka
Nduu ali mama awasiwe kinda.

(Siri Sirini 1 2013:158)

Fumo Liyongo anaonyesha akili nyingi kwa kufahamu udhaifu wa kitovu kama usimulizi unavyoeleza:

Huhitaji mgunzu wa almasi kuchomea kitovu cha mtu yeyote yule.
Hata mgunzu wa shaba au chuma watosha. Kitovu kina uwazi ndani,
hakina misuli wala nyama tepetepe. Kama nilivyokueleza, hiyo ni
njia wazi inavyoelekea moja kwa moja utumboni. (Siri Sirini 3
2014:83)

Fumo Liyongo anamwelezea Suleiman Mringwari njia rahisi ya kuliua jitu. Suleiman Mringwari alikuwa Ozi kumshawishi Fumo Liyongo kurudi Shanga kama jemadari wake. Mwanamfaume alitaka kujua namna ya kumwua adui. Fumo Liyongo alimfichulia siri ya udhaifu wa kitovu. Inasikitisha kwa sababu Suleiman Mringwari alimuua Fumo Liyongo kwa kumdunga kitovuni kwa sindano ya shaba aliporudi Shanga kuonyesha ukatili na usaliti wa Suleiman Mringwari.

Nguvu za mshikamano na kundi au jumuiya ni sifa nyingine ya Fumo Liyongo. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba shujaa huwa na maadui, pia huwa na watu wanaompenda na wafuasi. Maisha ya shujaa husheheni matatizo na hufikia kikomo pale anapotimiza lengo lake. Fumo Liyongo anahusiana vizuri na jamaa na marafiki zake. Alipomtuma Kijakazi Sada kwa mamake, alitimiziwa matakwa yake yaliyofanikisha kutoroka kwake ngomeni kama asemavyo msimulizi:

Ya arusi kutofuata mkondo waliokuwa wameupanga, na mno mno hasimu wao mkuu, Liyongo wa Bauri, kuvunja ngome na kutoroka! Mawili hayo yaliwaaibisha sana! Na mpaka sasa wanajiuliza ni vipi Liyongo aliweza kuikata minyororo thabiti yote waliyokuwa wamemfunga kwayo! Hata mimi binafsi yangu bado najiuliza iliwezekanaje! (Siri Sirini 2 2014:133)

Muktadha huu unaeleza jinsi Fumo Liyongo alivyofaulu kutoroka ngomeni. Fumo Liyongo alipelekewa tupa ngomeni ikiwa imewekwa ndani ya mkate wa wishwa. Marafiki zake, Mfawidhi Kijumwa Mfaume, Kibwana Mwengo Bashee na wafuasi wake waliufahamu mpango huo kuonyesha mshikamano wake na watu. Kwa hivyo, Fumo Liyongo alitoroka ngomeni siku ya arusi ya Mwanakupona na kuhamia nchi ya Ozi kama mkimbizi. Nchini Ozi, Fumo Liyongo alifanywa jemadari wa majeshi yote ya Ozi na kuoa bintiye mudir wa Ozi, Abanoye. Fumo Liyongo alikuwa na mshikamano na wapiganaji wa Ozi na alipouawa kinyama na mwanamfaume, Ozi iliingia vitani na Shanga. Mfalme Daudi Mringwari aliondolewa mamlakani na uongozi wa Shanga ukapewa Bauri wa Liyongo kuonyesha ujenzi wa jamii mpya.

Umaarufu wa Fumo Liyongo unajitokeza kisimani alipopiga magoti, mshale tayari kufuma. Msimulizi anasema kuwa wanawake walishindwa kuteka maji kisimani kwa kuogopa kushambuliwa na Fumo Liyongo. Wanawake hawa walimpenda na kumtakia mema Fumo Liyongo. Wanawake wengi waliangusha na kupasua nyungu zao wakilia

na kudai ya kuwa Fumo Liyongo alitaka kuwaua. Wapiganaji walibwaga mikuki yao na kukimbilia usalama wao. Viongozi nao walishindwa kumkabili Fumo Liyongo kudhibitisha nguvu za kimwili na kivita za Fumo Liyongo. Baada ya mamake kutangazia wenzake kwamba Fumo Liyongo alikuwa amekufa, wanawake wote walilia kwa nguvu kumlilia marehemu, mtu mwema, mkembe, mnyenyekevu na mwenye kupendwa na watu wengi. Watu wote mashambani na mjini waligubikwa na simanzi na huzuni ya kumpoteza Jemadari Liyongo; mfalme mstahiki asiyewahi kukikalia kiti cha enzi.

Mazishi ya Fumo Liyongo yalifuata sheria na utamaduni wa Kiislamu, pamoja na heshima zote stahiki ya mfalme anapopungwiwa mkono wa buriani. Hakuna aliyeweza kuyapinga matayarisho hayo kudhihirisha ushujaa wa mshikamano wa Fumo Liyongo na wanajamii. Mfalme Daudi Mringwari alighadhabishwa na heshima ya hali ya juu aliyotunukiwa marehemu kuonyesha wivu. Watu wengi waliohudhuria mazishi hayo walisema kwamba hata Mfalme Daudi Mringwari angefariki siku hiyo, hangetunukiwa nusu ya heshima aliyotunukiwa marehemu Fumo Liyongo. Watu waliohudhuria mazishi walitoka Uswahilini kote kuonyesha kwamba Fumo Liyongo alikuwa mtu mwema wa aina yake ingawa hakuwahi kuapishwa Mfalme.

Fumo Liyongo ni bingwa wa kisanaa. Katika arusi ya Mwanakupona ilipangwa kwamba, mwao, ngoma ya Fumo Liyongo ichezwe kwanza na mafundi stadi wa ngoma hiyo. Fumo Liyongo alikuwa ndani ya ngome, amefungwa silisili shingoni, miguuni na mikononi lakini sauti yake ikinguruma kama simba dhihirisho la dhuluma katika uongozi. Fumo Liyongo aliimba kwa ujuzi, upendo na uwezo wake huku akiwafurahisha waliohudhuria arusi kwa minajili ya kumuona baada ya kusikia sifa zake za wajiji na fani. Fumo Liyongo aliwatumbuiza watu kwa kughani shairi aliloliita ‘Waswifu wa Mwanananga’, utungo uliokisifu kila kiungo cha mwili cha mkewe Mwanananga.

Wimbo wa mwisho arusini ulikuwa wa Fumo Liyongo kwa mara ya pili usiku ule. Fumo Liyongo alipoanza kughani, watu wa Shanga walishangaa na kushikwa na hofu. Shairi lilikuwa ‘Takhmisa ya Liyongo’. Shairi husika ndilo lilimtia Fumo Liyongo ngomeni kama usimulizi unavyodokeza mishororo michache mfano, ‘Ninga mwana

kozi shirikene na mwana tope'. Kulingana na tafsiri ya usimulizi, kozi ni ndege wa kuwinda wenye makucha makali. Hakimu alimwuliza Fumo Liyongo pale mahakamani mtu aliyedhamiria kuwinda kuonyesha ukatili wa hakimu. Mfano mwingine ni 'Natetea haki na cheo'. Hakimu alitafsiri kwamba Fumo Liyongo alimaanisha kwamba cheo kilikuwa haki yake na 'Mwanangu mbonaye mbuziyo ukemetwe pembe na mkami akimkama' ambapo msimulizi alitafsiri kuwa mwanamfaume alifananishwa na mbuzi, mkami akiwa Fumo Liyongo yaani kiongozi. Ni vizuri kufahamu kwamba shairi lilitungwa kwa jazanda hivyo hakimu alitafsiri visivyo na kumfunga Fumo Liyongo kwa kosa la uhaini.

Ubingwa wa ngoma unadhihirika katika tukio hili:

Akajibwaga uwanjani na kudemka midemko ya kwao ya mwao na goma aliyoundokea kuizoea na kuwa hodari nayo. (Siri Sirini 1 2013:377)

Tukio hili lilitokea siku ya arusi ya Fumo Liyongo na Abanoye. Fumo Liyongo alikuwa ameomba apewe fursa ya kuwaghania waliohudhuria arusi utenzi wa binti yake, lakini ombi hilo lilikataliwa kiungwana. Wenye kupanga walikubaliana kwamba haingeonekana vizuri bwana-arusi kushiriki kitendo ambacho kingemtoa jasho. Utamu wa ngoma ulipozidi, Fumo Liyongo hakuzuiliwa huku akijikwatua kama kijana na kushangiliwa na watu wengi.

Fumo Liyongo alikuwa wa nasaba bora ya ufalme. Usimuliaji unaarifu kuwa mamake Fumo Liyongo, Mwanaziza, alikuwa dadake Mfalme mkongwe wa Shanga. Mwanaziza alimlea Fumo Liyongo pamoja na watoto wa kakake, Mwanalemba na Mfalme Daudi Mringwari baada ya kufiwa na mama yao bila ubaguzi. Msimulizi anasema:

Ni kwamba mamangu, Mwanaziza, alikalia kiti cha kakake sasa, kwa lengo la kushikilia hatamu mtoto Daudi wakati nchi nzima ilipomsubiri kwa hamu na uvumilivu akuekue angaa (Siri Sirini 3 2014:45)

Kauli hii ni dhihirisho kwamba Fumo Liyongo alizaliwa katika familia ya kifalme. Mwanaziza aliendelea kutimiza wajibu wa mfalme, babake Fumo Liyongo, Mzee Bauri, akiwa ubavuni mwake akitoa ushauri. Mzee Bauri aliaga dunia mara tu Daudi Mringwari alipokalia kiti chake na kutawazwa.

Kwa hivyo, Fumo Liyongo ni mhusika mkwezwa kwa vile amekwezwa kuliko wahusika wengine katika riwaya teule huku akionyeshwa kuwa na nguvu za ajabu za kimwili na kiakili, ujasiri, usanii, mshikamano na jamii, ujemadari na nasaba bora.

5.2.2 Mhusika wa kimapinduzi

Mhusika wa kimapinduzi ana mwamko mkubwa juu ya utu wake na jamii yake na ana ufahamu mpana wa maisha (Madumulla, 2009). Madumulla anamfafanua zaidi mhusika huyu kwa kusema kuwa madhumuni yake ni kupigania mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa, kitaifa na kimataifa na yuko radhi kujitoa mhanga kubadilisha maisha ya wanyonge. Sifa za mhusika wa kimapinduzi zinahusishwa na mtu anayeweza kupatikana katika maisha halisi. Wahusika Mdoe na Sikamona katika riwaya ya *Zawadi ya Ushindi* ni mifano mizuri, wanachochewa na nia ya kutaka kubadilisha jamii yao ambayo inaongozwa na viongozi walafi na wananchi wengine wenye tamaa ya kupata mali kwa njia zisiso halali (Ali, 2015). Mifano ya wahusika hawa katika riwaya teule ni:

5.2.2.1 Fumo Liyongo

Fumo Liyongo alimuomba Suleiman Mringwari kubadilika kiakili na kimawazo akitoka Misri. Alimwambia:

Itumie fursa hiyo kujifunza mengi. Nataka ukirudi uwe umebadilika kabisa. Uwe umebadilika kiakili na kimawazo!Uwe mpevu katika mwelekeo na kila jambo kwa jumla.(Siri Sirini 1 2013:133)

Fumo Liyongo alifungiwa ngomeni kwa kosa la uhaini. Suleiman Mringwari alimtembelea na kumwarifu kuhusu safari yao ya kwenda Misri. Walizungumzia masuala mengi hasa ukatili wa askari-ngome na arusi ya Mwanakupona. Fumo Liyongo alimshauri Suleiman Mringwari kutompelekea tena chakula ngomeni kuonyesha utabaka. Suleiman Mringwari alirudi kutoka Misri akiwa amebadilika kimtazamo.

Fumo Liyongo alitaka mapinduzi kama asemavyo Shalo:

Lakini Liyongo alitaka mapinduzi, sivyo? Shalo alishikilia uzi wake. Mapinduzi baridi lakini, siyo ya majambia na mafumo. (Siri Sirini 1 2013:96)

Msimulizi anaeleza kwamba Fumo Liyongo alitaka mabadiliko. Mabadiliko aliyoyataka Fumo Liyongo hayakuwa ya kutumia silaha za kivita kuonyesha ushujaa wa kiakili. Fumo Liyongo alipendelea mapinduzi ya amani na msimulizi hakuelewa sababu za utawala kumfungia ngomeni. Aidha anadhihirisha mabadiliko alipomwambia Sheikh Omar Soba kwamba katika mustakabali wa mapambano, ilikuwa vyema kujivinjari kabla ya shambulizi la kwanza thibitisho la ujasiri. Mabadiliko yanajitokeza pale alikusudia kumtumia mwanamfaume kuendeleza mipango yake ya mabadiliko. Anasema:

Nakusudia kumtumia kwa minajili ya kuendeleza mipango yangu ya mabadiliko. Hata yeye ana tamaa zake, sio? Au unadhani hangependa kuchukua hatamu za uongozi; leo wala si kesho? (Siri Sirini 2 2014:190)

Fumo Liyongo alitaka mabadiliko na alilenga kumtumia mwanamfaume. Fumo Liyongo alikuwa nyumbani mwake Ozi akishiriki mazungumzo na mkewe Abanoye. Dialojia yao ililenga nchi ya Shanga na watu aliowasaidia Fumo Liyongo kuajiriwa nchini Shanga kama vile Dhabina na marehemu Mfawidhi Kijumwa Mfaume. Fumo Liyongo alitaka kutumia watu wa familia yake kumsaidia kubadilisha Shanga kuonyesha mshikamano wa familia. Fumo Liyongo alifahamu hatima ya mapinduzi, kwamba katika mapambano, watu wengi huangamia kwa kutolewa kafara. Anasema hivi:

Katika mapambano, wengi ni sharti waangamie kwa kutolewa kafara, hususan wanapojitoa mhanga. Mwishowe, hata hivyo, ukombozi hauna budi kupatikana. Si tu, kila mwenye kuangushwa tiati anazidi kuhamasisha nia kuu ya wakereketwa ya kujikomboa. Ukombozi haufuzu ila muda wake unapotimu! (Siri Sirini 2 2014:190)

Msimulizi alijua kwamba katika mapambano watu wengi hufa kwa kutolewa kafara dhihirisho la utawala dhalimu. Murithi (2017) anasema kuwa dalili za udhaifu wa utawala hujitokeza katika uvumi, malalamiko, maandamano na migomo na mwishowe hulipuka na kuwa mapinduzi. Ni katika harakati hizi ambapo Fumo Liyongo alisema kuwa watu huangamizwa lakini mapinduzi hupatikana kuonyesha ujenzi wa jamii mpya. Fumo Liyongo aliamua kuwafundisha wanawe mafunzo yenye manufaa baada ya ukombozi. Fumo Liyongo aliwaambia wafuasi wake kwamba aliwaunga mkono viongozi waliotaka mabadiliko kamili kama asemavyo:

Sasa hebu nikawatayarishie chakula ilhali nyinyi mkiendelea kujadilia mikakati bora ya kupata wapiganaji, na vile vile mikakati bora ya mapambano yatakayotuletea ushindi. (Siri Sirini 3 2014:199)

Tukio hili lilitendeka wakati Fumo Liyongo alirudi Shanga na kukutana na wafuasi wake msituni kuonyesha mshikamano na watu waliomuunga mkono. Fumo Liyongo alikutana nao ili kufanya mikakati ya mapambano. Katika kikao, walizungumzia wanaharakati wengine kama Mwanalemba, Mwanaziza na Suleiman Mringwari aliyenuia kuunganisha eneo zima la Uswahilini na Barazinji yote. Fumo Liyongo alitaka mabadiliko kamili, basi hawakuwa na budi ila kuwa na mikakati bora.

Kwa hivyo, Fumo Liyongo ni kielelezo cha mhusika wa kimapinduzi kwa vile alijitoa mhanga ili Washanga wapate mabadiliko. Baada ya kifo chake, Shanga iliingia vitani na Waozi na kumuondoa mamlakani mmabavu Daudi Mringwari huku Bauri wa Liyongo akipewa uongozi wa Shanga.

5.2.2.2 Mwanakupona

Mwanakupona ni bintiye Fumo Liyongo. Mwanakupona alitunga ‘Utenzi wa Mwanakupona’ kama mchango wa kufanikisha siku ya arusi yake. Utenzi unawauliza wanawake kuwahudumia waume zao kwa utiifu, lakini wasifanye yale yaliyokatazwa na Mungu. Msimulizi anatomia Utenzi wa Mwanakupona kama silaha ya mabadiliko katika jamii iliyotawaliwa na jinsia ya kiume dhihirisho la taasubi ya kiume. Mwanakupona alitaka mmoja wa wazazi wake kuughani utenzi huo siku ya arusi yake, siku ambayo ni muhimu sana kwa wanandoa. Anaeleza :

Arusi ya Mwanakupona ilikuwa inakaribia, na kila mmoja alijitolea kushughulika upeo wa uwezo wake, ili kuifanikisha vilivyo sherehe hiyo. Ama kwa kusema kweli, kila mmoja alijitolea zaidi ya matarajio ya wenziwe. (Siri Sirini 1 2013:119)

Msimulizi anaeleza kwamba kila mtu alijitolea kufanikisha arusi ya Mwanakupona kuonyesha ushirikiano katika jamii. Mwanakupona aliandika utenzi huu akiwa shuleni Lamu alikosomea. Maneno aliyoyatumia katika utenzi aliyapata kutoka kwa mwalimu wake wa kike aliyenawirisha mawazo yake kudhihirisha umuhimu wa suala la elimu.

Menzwa alisema kuwa utenzi huo ulikuwa na uwezo wa kuleta mabadiliko ya kijamii kama anavyosimulia:

Sasa huu, ijapo hauwezi kuleta mabadiliko ya kisiasa nchini, na hilo sina hakika nalo, nina hakika unaweza kuleta mabadiliko ya kijamii, kama tu vile tunavyohitaji mabadiliko ya kisiasa. Kupata aina moja ya mabadiliko na kukosa ya pili si kupata mabadiliko kamwe huko. (Siri Sirini 1 2013:166)

Kauli hii ya Menzwa inaonyesha mabadiliko yaliyosababishwa nchini Shanga na utungo wa Mwanakupona. ‘Utenzi wa Mwanakupona’ ulibadilisha mfumo wa elimu nchini Shanga. Waziri wa Sheria alilinganisha Uhabeshi na Shanga, iliyokuwa na wasichana wenye vipawa vya utunzi wa tendi za kuwapa mawaidha binti zao ambao bado kuwazaa. Kwa jinsi hiyo hawangeepuka mapinduzi. Kibwana Mwengo Bashee alisema mawazo ya ‘Utenzi wa Mwanakupona’ ya kimapinduzi yalikuwa na uwezo wa kuwabadilisha vijana na kuwasababisha kuwa na mtazamo wa kimapinduzi. Anafafanua hivi:

Kwa hakika nilivutiwa sana na mawazo yake kuhusu elimu tunavyopaswa kuwapa vijana, akiwa yeye ni mmoja wao. Ana mapendekezo ya elimu, kwa menke zote mbili; yaani si ya wasichana peke yao, bali pia wavulana. (Siri Sirini 3 2014:318)

Msimulizi anadokeza mawazo yaliyojadiliwa katika utenzi husika yanaelimisha vijana wa kike na wa kiume kudhihirisha mabadiliko katika elimu na jamii. Kibwana Mwengo Bashee alipendekeza Mwanakupona kupewa wadhifa wa Waziri wa Elimu katika serikali mpya ya Shanga kuonyesha ujenzi wa jamii mpya inayowajumuisha vijana katika uongozi.

5.2.2.3 Dhaidho Sengo Biri

Dhaidho Sengo Biri ni mmoja wa wafuasi wa Fumo Liyongo. Msimamo wake kuhusu mabadiliko unapatikana katika kifungu hiki:

Iwapo mabadiliko tuyafikiriayo ni ya Shanga pekee, basi hatuwezi kufanikiwa kiasi kikubwa vile! Mabadiliko ya maana ni lazima yapatikane Uswahilini kote, tokea Mukadisho huko kaskazini, hadi Bukini kusini. (Siri Sirini 1 2013:67)

Dhaidho Sengo Biri anasimulia kwamba mabadiliko ya maana yalipaswa kupatikana Uswahilini kote. Anafafanua kwamba mabadiliko ya namna hiyo yanaweza kuwa ya aushi, mabadiliko ya bara lao. Dhaidho Sengo Biri aliona kitendo cha kuusambaza

‘Utenzi wa Mwanakupona’ kuwa hatua ya kimapinduzi. Dhaidho Sengo Biri ni mwanamapinduzi aliyetaka Fumo Liyongo awaongoze au waongozwe na Mfawidhi Kijumwa Mfaume ambaye hakuwa na damu ya kifalme kuonyesha mshikamano wa wafuasi wa Fumo Liyongo. Vilevile, Dhaidho alifafanua kuwa watawala wa Shanga walichukia mabadiliko na aliona haja ya kuelimisha matesa wenzao kuhusu uraia bora, haki za kiraia na haja ya mabadiliko kama asemavyo hapa:

Ah! Wewe nawe! Si kuelimisha matesa wenzetu kuhusu uraia bora, haki za kiraia na haja ya mabadiliko. (Siri Sirini 1 2013:220)

Kwa hivyo, Dhaidho Sengo Biri ni mhusika wa kimapinduzi kwa vile alifikiria mabadiliko ya uongozi nchini Shanga, mabadiliko Uswahilini kote na elimu ya mabadiliko kwa matesa wao.

5.2.2.4 Mfawidhi Kijumwa Mfaume

Mfawidhi Kijumwa Mfaume alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje nchini Shanga na mfuasi wa Fumo Liyongo. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alipendekezwa na Fumo Liyongo kupata cheo hicho. Hii ndiyo sababu Mfawidhi Kijumwa Mfaume aliwaambia wafuasi wake kwamba yeye alikuwa matunda ya mabadiliko. Mfawidhi Kijumwa Mfaume aliwaomba wafuasi wake kuwa na subira katika kudai mabadiliko:

Nataka mnifahamu, tena vizuri sana. Mimi nafahamu fika kuwa mtakayo nyinyi ni mabadiliko; mabadiliko yenye kufungamana na maendeleo. (Siri Sirini 1 2013:93)

Mfawidhi Kijumwa Mfaume alifafanua ya kwamba wafuasi wake walipenda mabadiliko yaliyo na maendeleo na kuwauliza kuwa na subira katika madai yao. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alipenda mabadiliko yaliyosababishwa kwa njia ya amani, siyo mapigano na kuwaeleza kwamba mabadiliko yaliyoletwa na kumwaga damu hayakuwa mabadiliko bali maasi yaliyotanguliza maafa. Aidha, alipendekeza wawe na mapambano yaliyo na manufaa, mapambano ya kupingana na maneno yaliyojaa busara bila kupigana kwa zana hatari dhihirisho la mzalendo mpenda amani. Mfawidhi Kijumwa Mfaume anadhihirisha mapinduzi alipowauliza wafuasi wa Fumo Liyongo kumpigania apate uhuru bila kupigana na watawala waliokosa kumwelewa. Mfawidhi Kijumwa Mfaume anaonyesha mabadiliko wakati alipanga njama ya kumtorosha Fumo Liyongo kutoka ngomeni kama anavyosimulia msimulizi:

Huku nyuma Mfawidhi, Kibwana na wafuasi wake wakakimbilia hema alimokuwamo Mwanakupona na nyanyake na kuwanyanyua juu kwa juu. Wengine katika kundi hilo wakawakimbilia wana wa

yule mwanamke aliyekuwa akiyalilia makinda yake. (Siri Sirini 1 2013:203)

Mwandishi anajua kuwa Mfawidhi Kijumwa Mfaume na wote waliompenda Fumo Liyongo walishirikiana kumtorosha ngomeni. Kijakazi Sada na Mwanaziza, mamake Fumo Liyongo walikuwa miongoni mwa waliotekeleza wajibu huo kuonyesha mshikamano wao. Mfawidhi Kijumwa Mfaume alitaka mabadiliko ambayo yangefanya unyama walioshuhudia siku ya arusi ya Mwanakupona kuwa kumbukumbu mbaya katika mapisi ya Shanga kama usimulizi unavyosema:

Hawa watu ni watu wa aina gani lakini? Binadamu mwenzi, tena nduguyo, umvue utu wake kabisa hadharani! Sasa ni aibu gani hii tuliyoipata? Maishani sijasikia kisa kama hiki chetu cha Shanga cha baba ya bibi-arusi kusherehekea arusi ya binti yake huku akiwa amefungwa minyororo miguuni, mikononi na shingoni? (Siri Sirini 1 2013:213)

Msimulizi anazungumzia ukatili uliyofanyiwa Fumo Liyongo siku ya arusi ya Mwanakupona. Arusi ilifanywa nje ya ngome huku Fumo Liyongo akiwa amefungwa silisili miguuni, mikononi na shingoni thibitisho la dhuluma kwa mfungwa. Watu waliohudhuria arusi kumuona Fumo Liyongo walistajabishwa na kitendo hiki. Mfawidhi Kijumwa Mfaume hakufurahishwa na tukio hili na kupendekeza mabadiliko ambayo yangekomesha unyama huo nchini hivyo kumsawiri Mfawidhi Kijumwa Mfaume kama mhusika wa kimapinduzi.

5.2.2.5 Menzwa Biry

Menzwa Biry anajitokeza kama mwanamabadiliko kwa kutaka mabadiliko kamili siyo aina moja ya mabadiliko kama anavyosema:

Kupata aina moja ya mabadiliko na kukosa ya pili si kupata mabadiliko kamwe huko! Menzwa aliteta. Ni kujidanganya tu, wala haitachukua muda mrefu ila tutarudi pale pale tulipoanzia! (Siri Sirini 1 2013:167)

Kauli ya Menzwa Biry inadai mabadiliko kamili. Menzwa Biry alitaka mabadiliko ya kisiasa na kijamii. Menzwa Biry alishangazwa na Mfawidhi Kijumwa Mfaume kusema ya kuwa alikuwa mwanamabadiliko ilhali alionekana akiandamana sako kwa bako na majahili kama Osman Ali Kidhabi. Akili yake Menzwa Biry ilimwambia

kuwa kulikuwa na uhusiano wa aina moja au nyingine katika ‘Utenzi wa Mwanakupona’ na mapambano yao katika kifungu hiki:

Mimi akili yangu inaniambia ya kwamba ni lazima pawe na uhusiano wa aina moja au nyingine kati ya ‘Utenzi wa Mwanakupona’ na mapambano yetu, la sivyo huyu Kibwana hangetwambia tuusambaze. (Siri Sirini 1 2013:220)

Msimulizi alifahamu uhusiano wa utenzi husika na mapambano. ‘Utenzi wa Mwanakupona’ ulionyesha mabadiliko ya kijamii kwa menke zote. Kibwana Mwengo Bashee aliwauliza wafuasi wake akiwemo Menzwa Biryu kuusambaza ili watu wote nchini Shanga wapate kuusoma, kunufaika na kubadilika kumsawiri Menzwa Biryu kama mhusika wa kimapinduzi kwa vile alishikilia mapinduzi.

5.2.2.6 Kibwana Mwengo Bashee

Kibwana Mwengo Bashee ni mfuasi wa Fumo Liyongo. Kibwana Mwengo Bashee ni mwanamapinduzi aliyetaka mabadiliko bila vita kama anavyosimulia:

Sisi hatuna haja ya kuvunja sheria. Haja yetu ni kuhakikisha ya kwamba taifa letu limefanikiwa kufanya mabadiliko yenye kuendeleza maislahi ya raia wote, bila bila damu kumwaika. (Siri Sirini 1 2003: 161)

Maneno ya Kibwana Mwengo Bashee yanafahamisha jinsi alivyoniua kupingana bila kupigana na kumwaga damu. Kibwana Mwengo Bashee anafafanua kuwa haja yao ilikuwa kuhakikisha taifa lao limebarikiwa kufanya mabadiliko kwa maslahi ya raia wote ishara ya kukomaa katika siasa. Kibwana Mwengo Bashee anadhihirisha mabadiliko alipousambaza ‘Utenzi wa Mwanakupona’ ambao ungewasaidia kuwatumbukiza viongozi katika mjadala uliohusu jamii walioongoza vibaya. Anasema hivi:

Nimesema hauna maudhui ya siasa, moja kwa moja. Utatusaidia kwa kuwatumbukiza viongozi katika mjadala unaohusu jamii wanayoongoza vibaya. (Siri Sirini 1 2013:168)

Msimulizi anaeleza kwamba ‘Utenzi wa Mwanakupona’ ulikuwa na mafunzo ya tabia njema na kwamba uliweza kusababisha mabadiliko ya kijamii. Kibwana Mwengo Bashee ni mwanamabadiliko aliyechangia kumtorosha Fumo Liyongo ngomeni kuonyesha manufaa ya mshikamano. Kibwana Mwengo Bashee na wafuasi wake walisherehekea sana tendo la Fumo Liyongo kukata minyororo, kuvunja lango la

ngome na kujinyakulia uhuru. Waliona tendo hilo kama lilingisha na kutia mashakani uongozi dhalimu. Osman Ali Kidhabi alimwita Kibwana Mwengo Bashee amiri jeshi wa kikosi kilichoendeleza mipango ya mapinduzi. Kibwana Mwengo Bashee aliamua kumuunga mkono kiongozi wa mabadiliko, Fumo Liyongo bila kujificha. Kubainika kwake kama mwanamabadiliko kulisababisha baadhi ya viongozi wa Shanga kupendekeza ahamishiwe nchi nyingine kama mkimbizi ili akose fursa ya kueneza kasumba yake ya kupinga serikali kuonyesha ukaragosi. Kibwana Mwengo Bashee alipendekeza mtindo mpya wa kuongoza Shanga ili kudumisha haki na utu, sio kudunisha dhihirisho la mabadiliko. Hali kadhalika uongozi wa Kibwana Mwengo Bashee na wengine katika serikali mpya uliwaachilia wafungwa wote thibitisho la ujenzi wa jamii mpya hivyo, kumsawiri kama mhusika wa kimapinduzi.

5.2.2.7 Mwanalemba

Mwanalemba ni dadake Mfalme Daudi Mringwari na binamuye Fumo Liyongo. Mwanalemba anaonyesha mabadiliko kwa kuwatuma watu kwa nduguye Mfalme Daudi Mringwari ili kumchunguza wapate ukweli kuhusu tabia yake. Mwanalemba alitunga shairi la 'Siri Sirini' lililowafunua macho na kuwakunjua masikio Washanga. Usimulizi unasema hivi:

Jambo la kwanza, yeye ndiye mhusika mkuu aliyetufahamisha maadili yaliyofichama katika utungo wake muthmini wa 'Siri Sirini'. Hiyo ndiyo hatua ya maana kabisa, hatua muhimu kupindukia kwetu sisi Washanga wote. Ilitufunua macho na kutukunjua masikio. (Siri Sirini 3 2014:316)

Msimulizi alimtaja Mwanalemba kama mwanamapinduzi wa dhati mwenye kupendelea mabadiliko. Utungo husika unakumbukwa kwa kumrejelea Anzuruni, Mfalme dhalimu aliyewadhulumu raia zake kwa kutumia hirizi na imani za kishetani kuwazindika na kuwagubika. Mwanalemba alimfananisha Mfalme Anzuruni na Mfalme Daudi Mringwari wa Shanga kwa kusema:

Tofauti ya dhalimu Anzuruni wa hadithini na Mfalme wa Shanga ni majina tu; hilo lifahamu, tena lifahamu sana. Watu hawa wawili imani zao ni moja, silaha zao ni moja na matendo yao ni mamoja. (Siri Sirini 1 2013:60)

Msimulizi hakuona tofauti ya Mfalme Anzuruni na Mfalme Daudi Mringwari wa Shanga kudhihirisha udhalimu katika utawala nchini Shanga. Msimulizi anapendekeza

kutangazwa kwa fatwa juu ya utawala wa Mfalme Daudi Mringwari na kupangwa kwa mapinduzi ili kuikomboa nchi kuonyesha ujenzi wa jamii mpya. Mwanalemba anaendeleza mabadiliko kwa kumuita mumewe, mkongwe wa taasubi tasa za ujanadume zilizoyadidimiza matumaini ya mabadiliko. Mwanalemba alipewa wadhifa wa naibu Waziri Mkuu wa Shanga kwa sababu ya kufichua maovu yaliyotendeka katika jamii hivyo kumsawiri kama mhusika wa kimapinduzi.

5.2.2.8 Mwanaziza

Mwanaziza ni mamake Fumo Liyongo. Mwanaziza anaonyesha mabadiliko kwa kufurahia ujumbe katika shairi la ‘Siri Sirini’. Anasema:

Ikipitishwa kuwa ni silaha tosha, mapambano yataanza! Na hayatakoma hadi udhalimu ukomeshwe kabisa kabisa! (Siri Sirini 2 2014:167)

Mwanaziza alisoma shairi husika, akaliita asali na kuona mwanga baada ya giza. Msimulizi alifafanua kwamba utungo husika ulikuwa silaha ya kupambana na utawala dhalimu nchini Shanga. Mwanaziza anaonyesha mabadiliko katika uongozi pale alikubali kuwa mwenyekiti katika kikao kilichojaza nafasi za viti vilivyobakia katika serikali mpya ya Shanga. Mwanaziza alieleza kuwa Utamaduni ilikuwa idara katika Wizara ya Elimu na kwamba wangeiga mifano bora toka mataifa ya Uswahilini kama vile Lamu na Pate. Usimulizi unadokeza:

Utamaduni uko pamoja na Elimu; yaani ni idara ya wizara hiyo. Tutaiga mifano bora toka mataifa ya Uswahilini, kama vile Lamu, Pate na kwingineko, tuoanishe na nguzo zetu muthmini za utamaduni wetu asili wa papa hapa Shanga. (Siri Sirini 3 2014:354)

5.2.2.9 Malkia wa Sheba

Waziri wa Sheria wa Shanga alitumia kielelezo cha Malkia wa Sheba kuthibitisha maovu yaliyofichama katika ‘Utenzi wa Mwanakupona’. Madai ya Waziri wa Sheria yalikuwa ‘Utenzi wa Mwanakupona’ ulikuwa na uwezo wa kusababisha mapinduzi nchini Shanga. Anasema hivi:

Hebu waulize Wahabeshi! Au hujasikia maishani mwako watu wakimtajataja sana Malkia ya Sheba? Wadhani alikuwa mwanamume huyo? Alikuwa mwanamke bibi, mwanamke kama wewe tu! Mwanamke aliyejiona yuko juu sana ya wanaume wote Uhabeshi nzima hata akaondokea kuwadharau. (Siri Sirini 1 2013:229)

Msimulizi anadhihirisha kwamba wanawake wakipewa mamlaka wanaweza kuleta mabadiliko katika jamii na kuwadharau wanaume. Kulingana na Waziri wa Sheria wanawake wanapaswa kutawaliwa na wanaume. Waziri wa Sheria anafafanua kwamba Malkia ya Sheba:

Alisafiri safari ndefu wee hadi kokolo, mbali huko Filistina!
Akaendajirahisisha kwa Mfalme wa huko siku hizo, Nabii Suleiman bin Daudi. Akarudi nyumbani na ujauzito haramu wa nje ya ndoa, bila hata aibu! Akajizalia mwanawe wa kiume ambaye hakutambuliwa na babake; akamwita Menelik. Huyo ndiye mtoto aliyeanzisha ukoo wa utawala wa Uhabeshi wenye mizizi yake Filistina, ambao ndio ulioko uongozini hadi wa leo. (Siri Sirini 1 2013:230)

Msimulizi anaonyesha jinsi Malkia wa Sheba alileta mabadiliko nchini Uhabeshi kwa kupata mtoto wa kiume nje ya ndoa. Ukoo wa Menelik ulichukua uongozi Uhabeshi kusababisha mabadiliko uongozini hivyo kumsawiri kama mhusika wa kimapinduzi.

5.2.2.10 Abanoye

Abanoye ni mke wa pili wa Fumo Liyongo. Abanoye alikuwa amri jeshi katika vita baina ya Waozi na Washanga baada ya mauaji ya kikatili ya Fumo Liyongo. Msimulizi anasimulia:

Mishale ikanyesha upande wao, kila kipembe, kama mvua ya masika. Ati ati ilipoenea ya kwamba viongozi upande wa Waozi ni watu wawili waliobandikwa lakabu za ‘msaliti’ na ‘mkisasi’, watetezi wa Shanga wakaghadhabika kupindukia! (Siri Sirini 3 2014:270)

Kauli ya msimulizi inaeleza kuwa viongozi upande wa Ozi walikuwa ‘msaliti’ na ‘mkisasi’. ‘Msaliti’ alikuwa Kibwana Mwengo Bashee, mfuasi wa Fumo Liyongo aliyeenda Ozi kumfahamisha Abanoye kuhusu mauaji ya mumewe, Fumo Liyongo na mwanawe, Mwinyi nchini Shanga. Kibwana Mwengo Bashee alikuwa ameulizwa na utawala wa Shanga kuhama Shanga kuonyesha udhalimu. ‘Mkisasi’ alikuwa Abanoye. Abanoye alitumia ujuzi wa zana za vita aliofunzwa na mumewe ili kuweza kujitetea na kuwatetea aliowapenda. Abanoye alitumia panda, teo, na uta na mishale kwa ustadi na aliwaamrisha wapiganaji wake kwa Kigalla. Vita hivi vilimuondoa uongozini mmabavu Daudi Mringwari huku Bauri wa Liyongo akichukua uongozi dhihirisho la mapinduzi nchini Shanga.

Katika historia ya nchi ya Kenya kuna baadhi ya wanawake majagina waliopigania uhuru kama vile: Mekatilili wa Menzwa aliyeongoza jamii ya Giriama na Wangu wa Makeri (Yenjela, 2015). Yenjela anafafanua kwamba Wangari Maathai ambaye amesimulia hadithi yake katika *Unbowed* ni mwanamapinduzi aliyepigania uhifadhi wa mazingira wakati wa enzi ya hayati Rais Daniel Moi hivyo kukubali mchango wa wanawake katika uongozi. Mwanalemba alimshukuru Abanoye kwa kuwakomboa ilhali Abanoye alimjibu kwamba huo ulikuwa wajibu wake kama anavyosimulia:

Hilo lilikuwa jukumu langu kwa watu wa kwao mume wangu.
Ulikuwa wajibu wangu mahsusi, kwa hakika. (Siri Sirini 3
2014:324)

Msimulizi anadhihirisha kwamba ulikuwa wajibu wake kuwakomboa Washanga kutokana na uongozi dhalimu wa Daudi Mringwari, uongozi uliomuua mumewe kikatili pamoja na mwanawe Mwinyi ambaye mwili wake haukuwa umepatikana. Abanoye alipigana na mfumo wa jamii iliokosa kumtetea alipobakwa na wapiganaji watano. Anaeleza:

Watano ndugu yangu... Wapiganaji kutoka mbari nyingine iliyokuwa haiishi kupambana na mbari yetu. Walinibaka, wanaume hao, sio kwa sababu ya tamaa yao ya ujana dume, bali mintarafu ya kumwudhi baba yangu tu.(Siri Sirini 1 2013:318)

Abanoye alimsimulia Fumo Liyongo jinsi alivyodhulumiwa kwa kubakwa na wanaume watano. Wanaume hao walikuwa wapiganaji kutoka mbari nyingine waliopigana na mbari yao. Babake Abanoye, Omar Soba alikuwa mudir hivyo walimbaka Abanoye ili kumwumiza babake kuonyesha ukatili wa wapiganaji. Abanoye alichekwa na kila mtu katika jamii, wakamdharau, wakambeza na kumzomea kila walipomuona. Abanoye alijipigania kwa kuwaua thibitisho la kisasi. Anasema hivi:

Kama una maana ya wale afriti walionibaka, basi hao yakupasa ujue tayari niliwaangamiza. Tena kitambo sana! (Siri Sirini 1 2013:402)

Msimulizi alikiri kuwaua mmoja mmoja wanaume waliombaka kumsababishia dhiki katika maisha yake na maisha ya babake. Abanoye hakumsimulia Fumo Liyongo njia aliyoitumia kuwaua kuonyesha usiri. Abanoye alitaka ujuzi zaidi wa kutumia silaha na ndipo alimuuliza Fumo Liyongo kumfunza kuzitumia. Abanoye alisema kuwa kama angekuwa na uwezo wa kupigana katika vita, basi hangebakwa.

Abanoye alikubali kubadilishiwa jina na familia ya Fumo Liyongo. Msimulizi alimuuliza:

Je unaukubali mpango huu Malkia wa Kigalla, ambaye huku Uswahilini utakuwa ukiitwa Mwanaaba na Mwananoye pamoya? Naukubali kwa moyo wangu wote! Alinena Abanoye. Waaidha nayakubali na tayari nayapenda majina yangu ya Kiswahili. (Siri Sirini 3 2014:353)

Maelezo haya yanaarifu kuwa Abanoye alibadilishiwa jina lake la Kigalla na kupewa jina la Kiswahili. Mwanaziza ambaye alikuwa mkubwa wa umri katika familia na mamake Fumo Liyongo ndiye alipendekeza jina jipya. Abanoye alikubali kuitwa Mwanaaba au Mwananoye thibitisho la kukubalika kama mmoja wa familia yao hivyo kusawiriwa kama mhusika wa kimapinduzi.

5.2.2.11 Suleiman Mringwari

Suleiman Mringwari ni mwanawe wa pekee wa Mfalme Daudi Mringwari. Suleiman Mringwari alimsikiza sana Mfawidhi Kijumwa Mfaume walipokuwa nchini Misri. Safari ya Misri ilimbadilisha Suleiman kama vile Madhubuti katika riwaya ya *Kidagaa Kimemuozea* (2012) alivyobadilika alipokwenda masomoni Urusi. Katika barua aliyomwandikia babake, Madhubuti alijitambulisha kwa jina la mamake Zuhura kuonyesha mabadiliko. Suleiman Mringwari alibadilishwa na safari ya Misri. Suleiman Mringwari na wenzake walipewa nafasi ya kuwahutubia hadhira baada ya kurudi Shanga. Katika hotuba yake, Suleiman Mringwari alipendekeza mabadiliko ya jinsi ya kuitana katika kifungu hiki:

Akaeleza ya kwamba huku Shanga kuna watu wasioitwa kwa majina yao abadani, bali watu hao huitwa kwa vyeo kama vile Waziri Mkuu. Akasema ni jambo la kujivunia kwa mtu yeyote kuitwa kwa jina lake la kidini sambamba na lile la kitamaduni. (Siri Sirini 1 2013:372)

Msimulizi alitaka mfumo wa kuitana majina ubadilishwe kama walivyofanya Wamisri thibitisho la mabadiliko kiimani na kimsimamo. Suleiman Mringwari hakupendelea namna Washanga walivyoitana kwa vyeo dhihirisho la utabaka na ubaguzi. Suleiman Mringwari alisisitiza umuhimu wa mtu kuitwa kwa jina la kidini na la kitamaduni kuonyesha imani ya dini na utamaduni. Suleiman Mringwari alimtembelea Fumo Liyongo ngomeni kabla ya safari ya Misri. Walizungumzia masuala mengi hasa safari ya Misri, arusi ya Mwanakupona na ukatili wa askari-ngome. Fumo Liyongo alimshauri

mwanamfaume kutumia fursa ya kusafiri nje ya Uswahili kujifunza mengi na akirudi Shanga awe amebadilika kiakili na kimawazo dhihirisho la mabadiliko. Kwa sababu hiyo, Suleiman Mringwari alimuomba Mwanaziza kumwita kwa jina lake kamili na hakuona ubaya wa kumuoa Kijakazi Sada kwa sababu mwenyezi Mungu hakubagua.

Suleiman Mringwari alitaka kuishi miaka mingi ili kuweza kuibadilisha Shanga iwe kama Misri au zaidi. Suleiman alimshawishi Kibwana Mwengo Bashee na Dhaidho Sengo Biri kumuunga mkono katika azma yake ya kuibadilisha Shanga katika utawala. Suleiman aliwaomba wamuunge mkono ili aweze kuibadilisha Shanga na mwambao mzima wa Uswahilini na kujumuisha Barazinji nzima. Anajitokeza kama mwanamabadiliko kwa kumfunza Mwinyi janja za mapambano kama anavyoeleza:

Nataka kukufunza mambo mawili matatu ya kiutu-uzima. Nina maana ya janja za wapambanaji stadi. Somo la kwanza: Chochote kionekanacho dhaifu usidhani ni dhaifu. Na ndio maana naamini kikamilifu kuwa wewe utasaidia sana katika mapambano haya. (Siri Sirini 3 2014:217)

Msimulizi alitaka kumfunza Mwinyi ujanja katika mapambano. Walikuwa msituni Suleiman alipokuwa amempa Fumo Liyongo chakula kilichomfanya kulala. Suleiman alinuia kumtumia Mwinyi kiujanja katika harakati za kumuua Fumo Liyongo ili apate kuiongoza Shanga dhihirisho la ukatili, ulaghai na usaliti katika kuleta mabadiliko hivyo kumsawiri kama mhusika wa kimapinduzi.

5.2.2.12 Mfalme Filipino wa Pili

Mfalme Filipino wa Pili ni babake Khalikzanda aliyepambana na Falme na kuzishinda kama alivyosimulia Mfawidhi Kijumwa Mfaume:

Kwa miaka mingi, babake Mfalme Filipino wa pili, alikuwa amepambana na Falme kadha wa kadha nje ya Masedonia na kuzishinda.(Siri Sirini 1 2013:306)

Msimulizi alimwarifu Suleiman Mringwari wakiwa Misri jinsi Mfalme Filipino wa pili alivyopigana na kupata ushindi. Mfalme Filipino wa pili aliadhifu Falme zilizomsaliti na kuwarudisha katika himaya yake kuonyesha ukakamavu katika uongozi. Mfalme Filipino wa pili aliendeleza mabadiliko kwa kumuoa mke wa pili, Kliopatra ili apate mrithi halali kama inavyodokezwa:

Babake mkubwa Malkia Kliopatra akamwita Khalikzanda ‘mwanaharamu’, mwana wa kuchanganya damu; akadai sio Mmasedonia halisi. Akazidisha madai na kusema ya kuwa Khalikzanda, baadaye, atakuja aungane na watu wa kwa mamake, wapambane na utawala wa Masedonia wa halali na kumpindua. (Siri Sirini 1 2013:307)

Mfalme Filipino alioa Kliopatra kwa ushawishi wa Jemadari Atalasi, mjombake Kliopatra. Mamake Khalikzanda, Olimpiasi, alitoka Epirusi. Kwa vile Mfalme Filipino aliogopa kupinduliwa na Khalikzanda na watu wa mamake, alioa Mmasedonia ili kupata mrithi halali kuonyesha ukabila. Kitendo hiki cha kumuoa Kliopatra kilibadilisha mfumo wa mambo nyumbani kwake kwani Khalikzanda alipuuzwa na kutengwa kuonyesha ubaguzi. Mfalme Filipino wa pili aliandaa dhifa ya kusherehekea mwaka mmoja tangu kuzaliwa kwa mwanawe Kliopatra. Jemadari Atalasi alimpuuzwa Khalikzanda huku Khalikzanda akikasirika na kumwagia pombe. Mfalme Filipino wa pili alikasirika na kwa sababu alikuwa amebadilisha mtazamo wake kwa Khalikzanda, alimshambulia hivyo kuonyeshwa kama mhusika aliyeleta mabadiliko ya jamii kitamaduni na kisiasa.

5.2.2.13 Khalikzanda

Khalikzanda alipindua utamaduni kuhusu ndoa na urithi kwa kuoa Muajemi:

Kwa sababu ya vile yeye mwenyewe binafsi alivyobaguliwa, baina ya mambo mengine. Kinyume kabisa, hakuo Mmasedonia wala hata Mzungu kama yeye kamwe. Aliamua kuyakabili hayo mateso yake ya wali kwa kumuoa Muajemi, na kisha akawashawishi majemadari wake wote nao pia waoe wasichana wa Kiajemi. (Siri Sirini 1 2013:312)

Maneno ya msimulizi yanaonyesha kuwa Khalikzanda alibadilisha mfumo wa ndoa nchini Masedonia. Baba yake, Mfalme Filipino alioa mke wa pili, Kliopatra kwa sababu mamake hakuwa Mmasedonia. Khalikzanda alibaguliwa na babake. Baada ya kifo cha babake, Khalikzanda alioa Muajemi na kuwashawishi majemadari wake wote kuoa wasichana wa Kiajemi na walikubali. Alifanya mabadiliko uongozini kama usimulizi unavyoeleza:

Hivyo ndivyo Misri ilivyofanya. Hivyo ndivyo Mtukuka Ali Kizanda alivyofanikiwa kuyaingiza mataifa mengi ya Ulaya, Asia na hata Misri ya kale katika himaya yake, chini ya utawala wake. (Siri Sirini 2 2014:214)

Msimulizi anaeleza namna Khalikzanda alivyobadilisha Masedonia kwa kuyaingiza mataifa ya kigeni. Khalikzanda aliteka mji mmoja baada ya mwingine kufanya Misri kuwa taifa moja kubwa. Aidha, Khalikzanda aliwaadhibu wasaliti wote waliompa ngumu babake kama vile Watharasia waliojitenga mara tu baada ya habari ya kifo cha Mfalme Filipo kuwafikia dhihirisho la kisasi. Khalikzanda aliua kila kitu na wengine akawauza kwa walioshiriki biashara ya watumwa. Khalikzanda alienda Misri kupigana nao lakini walimkaribisha kama mkombozi hivyo kumsawiri kama mhusika wa kimapinduzi.

5.2.2.14 Halfani Muyaka

Halfani Muyaka alikuwa waziri wa kwanza kuangamizwa na utawala wa Mfalme Daudi Mringwari. Halfani Muyaka ni mwanamabadiliko aliyebadilisha sheria tasa na hasi, sheria za kizamani za Shanga kwa kasi sana hivyo kuonyeshwa kama mhusika wa kimapinduzi.

5.2.3 Mhusika wa kisaikolojia

Kwa mujibu wa Madumulla (2009) mhusika wa kisaikolojia ni mhusika mnyonge kimwili na kiakili, anayekata tamaa na anayehitaji msaada wa jamii. Mhusika huyu hukumbana na matatizo mengi ya kijamii na anatia huruma kwa msomaji. Wamitila (2008) anaeleza kwamba mhusika wa kisaikolojia huonyeshwa kwa undani zaidi na labda hata misukumo ya kisaikolojia ya matendo yake kuonyeshwa kwa njia wazi. Mama Ntilie katika riwaya ya *Watoto wa Mama Ntilie* ni mhusika wa kisaikolojia kulingana na yale anayopitia kutoka kwa mumewe Lomolomo na kufukuzwa kwa watoto wake shule kunapelekea kutumia akili yake zaidi ili apambane na hali na kumiliki nafsi yake isiathirike kisaikolojia (Ali 2015). Riwaya trilojia ya *Siri Sirini* ina wahusika wa aina hii. Mfano:

5.2.3.1 Abanoye

Abanoye alipitikiwa na mambo mengi maishani yaliyomtesa kama anavyomsimulia Fumo Liyongo hivi:

watano ndugu yangu... wapiganaji kutoka mbari nyingine iliyokuwa haaishi kupambana na mbari yetu. (Siri Sirini 1 2013:318)

Msimulizi anaeleza jinsi alibakwa na wanaume watano tukio linaloibua huruma kwa msomaji. Wapiganaji waliombaka walitaka kumwudhi babake, Omar Soba aliyekuwa mudir wa Ozi. Abanoye anafafanua kuwa baada ya kubakwa alichekwa kwa muda mrefu na wasichana, wavulana, baba zao, mama zao, nyanya zao, na babu zao tukio ambalo lilifanya maisha yake kuwa jehanamu kuonyesha huruma. Abanoye alidharauliwa waziwazi, akambeza na kuzomewa na watu kila walipomwona kuibua hisia za huruma.

Abanoye alilazimika kuolewa na mvulana mtoto wa muungwana wa kwao Ozi. Ndoa hii ilikuwa ya kupanga. Ndoa yao ilikuwa na matatizo kuanzia mwanzo. Mumewe Abanoye alimkumbusha Abanoye kwamba alibakwa na kwamba alimuoa kwa sababu hakutaka kuwavunja moyo wazazi wake. Mumewe alimuita Abanoye kila aina ya matusi lakini Abanoye alivumilia kwa vile hakutaka kumuudhi babake kwa kurudi nyumbani tukio linaloonyesha huruma. Abanoye anaeleza kuwa mumewe hatimaye alimpa talaka tatu dharuba moja kwa kosa la kubakwa na kutiwa dosari dhahirisho la unyonge kwani hangejitetea. Kwa miaka miwili aliokuwa ameolewa, Abanoye hakushika mimba na lawama ilikuwa kwake. Alipotilikiwa, Abanoye alikuwa na mimba ya miezi miwili. Abanoye alijifungua mtoto wa kike, Mize aliyekataliwa na babake sababu ya jinsia thibitisho la ubaguzi kwa misingi ya jinsia.

Upweke ulimkumba Abanoye baada ya kufiwa na mamake na kaka zake wanne. Abanoye anasimulia:

Nilipokuwa Lamu, kulianguka kondo kali ya mbari, na kaka zangu wote wanne wakaangamizwa. Yalikuwa mauaji ya halaiki, kwa hakika. Baba akanitumia ujumbe nisiharakishe kurudi nyumbani... tayari: babangu, mimi mwanawe wa pekee, na vitoto vyangu viwili. (Siri Sirini 1 2013:375)

Msimulizi ni mpweke kwa vile mama na kaka zake walikuwa wafu. Waliuliwa kikatili katika kondo ya mbari thibitisho la unyonge aliokuwa nao Abanoye. Abanoye alilazimika kukaa Lamu kwa miaka miwili alikoenda kusoma madrassa kuonyesha suala la imani katika dini. Tukio la kuuawa kwa jamaa zake lilisababisha Abanoye kusherehekea arusi yake kwa Fumo Liyongo bila fahari ya kujumuika na familia. Fumo Liyongo pia alimuoa Abanoye ili kumuondolea dhiki kama anavyomsimulia mkewe Mwanananga katika kifungu hiki:

Nataka kumuoa Abanoye. Kwa nini? Kwa sababu ... Kwa kuwa....
Sijui ni kwa nini....! Nadhani ni kwa sababu...nataka kumpunguzia
dhiki! (Siri Sirini 1 2013:338)

Fumo Liyongo anamweleza mkewe Mwanananga ya kuwa lengo la kumuoa Abanoye lilikuwa kumpunguzia dhiki kudhihirisha huruma. Ni kweli Abanoye alikuwa amekubwa na matatizo mengi hivyo alihitaji mtu wa kumsaidia kuubeba mzigo hasa majukumu ya kuwalea watoto. Hata hivyo, ndoa ya Abanoye kwa Fumo Liyongo haikuwa suluhisho kwa matatizo yake. Fumo Liyongo alishawishiwa na Suleiman Mringwari kurudi Shanga ili kuiongoza. Fumo Liyongo alirudi Shanga akiandamana na mwanawe Mwinyi na kuuawa na Suleiman Mringwari kwa kumdunga kwa sindano ya shaba kitovuni huku akimwacha Abanoye na uja uzito wa miezi miwili kuonyesha huruma.

5.2.3.2 Osman Ali Kidhabi

Osman Ali Kidhabi ni mwana wa kijakazi aliyefanya kazi katika nyumba ya babake Mfalme Daudi Mringwari kama usimulizi unavyodokeza:

Inasemekana ya kuwa Mfalme mzee alimpenda kijakazi wake mmoja, mamake Kidhabi. Wakafanya yao waliyofanya, kijakazi akashika mimba, Kidhabi akazawa. Ionekanavyo ni kuwa Daudi Mringwari, Mfalme aliye kitini hivi sasa, aligundua uhusiano huo mapema sana. (Siri Sirini 2 2014:11)

Fumo Liyongo alimsimulia Abanoye kuhusu watu wa Shanga akianzia na hasimu wake, Osman Ali Kidhabi. Fumo Liyongo alimsimulia Abanoye uvumi kuhusu babake Osman Ali Kidhabi, kwamba baada ya mamake Daudi Mringwari kufa, Mzee Mringwari alifanya mahusiano na kijakazi hivyo kuzaliwa kwa Osman Ali Kidhabi kuonyesha mahusiano ya kimapenzi hayana tabaka. Mfalme Daudi Mringwari alijua uhusiano huo na akautumia ipasavyo kujinufaisha. Usimulizi unajuza kuwa Osman Ali Kidhabi alilelewa kingwana huku akienda Lamu na Uswahilini kote alikojifunza uchawi. Osman Ali Kidhabi alizoa vya halali na vya haramu kote huko kuonyesha unyonge wa Kidhabi kwa kuwa mamake alikuwa kijakazi.

Mfalme Daudi Mringwari alikumbuka maisha ya utoto ya Osman Ali Kidhabi. Anasema:

Kidhabi huyu huyu, zamani zao alipokuwa akiota usingizini na kulegeza misuli yake; alivyokuwa akijilowesha chapachapa na maji ya haja ndogo, akarovya nguo zote kitandani. (Sirini 3 2014:187)

Mwandishi anaeleza jinsi Osman Ali Kidhabi alikuwa mnyonge kwa kuota na kujilowesha kitandani. Osman Ali Kidhabi alitoa ufundo kama kibofu chake kilikuwa kimeoza huku akiendelea na usingizi wake mnono hadi asubuhi. Msimulizi anafafanua maisha ya unyonge ya Osman Ali Kidhabi alipokuwa mtoto kwa kukumbuka namna alivyofedheheshwa kwa kufungwa kiunoni mtungo wa majongoo hai marefu, meusi yenye miguu mingi akiwa uchi. Osman Ali Kidhabi alibebeshwa nguo yake ya kujifunika aliyoifanyia haja ndogo kuonyesha huruma. Osman Ali Kidhabi aliimbiwa nyimbo kwa sauti kubwa za kumfedhehesha na kumkejeli thibitisho la unyonge.

Osman Ali Kidhabi alitumia unyonge huu kujitetea mahakamani kama anavyosema:

Nilizipata kwa mama. Mama yangu alikuwa kijakazi; mtumwa mwanamke manake! Utumwa tayari ni nongo mbi! Akamzaa mwana, mimi hapa. Mwana huyo hakujulikana iseye...nongi mbi nyingine hiyo katika jamii iliyojikita kwenye kuiheshimu aila ya baba na mama wenye kuoana kirasmi. (Siri Sirini 2 2014:180)

Kauli ya Osman Ali Kidhabi inaeleza kwamba alionewa sababu ya kuwa na nongo mbi, taka mbaya mwenye uchafu. Msimulizi anafafanua kuwa nongo mbi hizo alizitoa kwa mamake aliyekuwa kijakazi dhihirisho la tabaka la kimaskini. Osman Ali Kidhabi anafafanua kwamba alionewa kwa sababu hakuzaliwa katika familia kamili iliyo na baba na mama kuonyesha unyonge katika uzawa wake. Osman Ali Kidhabi aliangaliwa vibaya na jamii kwa sababu alikuwa mwanaharamu thibitisho la unyonge. Katika hali hii ya kujitetea Osman Ali Kidhabi alitoa tangazo hili:

Sasa nina tangazo hapa; na nisikeni vizuri sana ...Kuanzia leo nataka mjue kwamba mimi si mwanaharamu! Hakuna mwanaharamu duniani, asilani! Hakuna mwanaharamu kwa vile hakuna mtu asiyekuwa na baba! ...kuwa nilijizaa mwenyewe jamani, ama? (Siri Sirini 2 2014:180)

Osman Ali Kidhabi alijitetea kwa kueleza matatizo mengi aliyopitia kama vile kuitwa mwanaharamu. Osman Ali Kidhabi alifafanua kwamba hakuwa mwanaharamu kwa sababu hakujizaa na kwamba alikuwa na baba na mama ingawa watu wengi hawakumjua kudhihirisha huruma. Osman Ali Kidhabi alijitetea kwa kusema kuwa

yeye alikuwa kiumbe mnyonge na hangeweza kuwa mwanga hivyo kuwa kielelezo cha mhusika wa kisaikolojia.

5.3 Hitimisho

Uchunguzi ulibaini kuwa usimulizi katika riwaya teule umetumia wahusika wengi. Wahusika hawa wamekuwa nguzo muhimu katika kuendeleza matukio mbalimbali katika hadithi hii na wameainishwa kama: Mhusika mkwezwa, mhusika wa kimapinduzi na mhusika wa kisaikolojia.

SURA YA SITA

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.1 Muhtasari

Lengo la utafiti lilikuwa ni kuchunguza mbinu za usimulizi katika riwaya trilojia ya *Siri Sirini*. Huu ni utafiti wa kifasihi uliohusisha kusoma, kuchambua na kuhakiki matini tatu za *Siri Sirini* na kuwasilisha matokeo ya uchunguzi kwa kuyapanga katika sura. Utafiti una jumla ya sura sita. Sura ya kwanza ilijadili: Usuli wa utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti ambayo yalilenga mbinu za usimulizi na usawiri wa wahusika, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, na maelezo ya istilahi. Sura ya pili ilihusu mwauo wa maandishi ambayo ni: Usimulizi katika fasihi, riwaya ya Kiswahili, dhana ya riwaya trilojia, riwaya trilojia ya *Siri Sirini* na msingi wa nadharia. Sura ya tatu ilihusu mbinu za utafiti. Katika sura hii vipengele vifuatavyo vilijadiliwa: Mpangilio wa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, maadili ya utafiti, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

Sura ya nne na tano ilihusu uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Sura ya nne ilijadili mbinu mbalimbali za usimulizi zilizotumika kuisimulia riwaya hii na kutambua mbinu zifuatazo: Usimulizi wa hotuba, usimulizi wa ki-itimamu, usimulizi penyezi, usimulizi tautolojia, usimulizi wa motifu ya safari, usimulizi wa nyimbo, usimulizi kirejeshi, usimulizi elekezi, usimulizi muhtasari, usimulizi udondoshi, usimulizi onyesho, usimulizi mtuo, usimulizi uendelezaji na usimulizi wa idadimarudio. Sura ya tano ilijadili usawiri wa wahusika kwa kutumia matendo yao, jinsi wanavyosema kujihusu, jinsi wahusika wengine wanavyosema kuwahusu na jinsi msomaji anavyosema kuwahusu. Wahusika walionyeshwa kuwa muhimu katika uendelezaji wa matukio katika hadithi. Aidha, wahusika walisawiriwa kama: Mhusika mkwezwa, mhusika wa kimapinduzi, na mhusika wa kisaikolojia. Sura ya sita ni muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

6.2 Hitimisho

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya naratolojia. Nadharia hii ilituliwa kwa sababu ya vigezo vya kimsingi katika kulichunguza suala la usimulizi na kipengele cha wahusika. Vigezo hivi vilikuwa mihimili mikuu katika uchunguzi huu. Uchunguzi wa madhumuni ya kwanza ulibaini kuwa riwaya trilojia ya *Siri Sirini* imetumia mbinu

mbalimbali za usimulizi katika kuisimulia kama vile: Usimulizi wa hotuba, usimulizi wa ki-itimamu, usimulizi penyezi, usimulizi wa nyimbo, usimulizi wa motifu ya safari, usimulizi tautolojia, usimulizi muhtasari, usimulizi udondoshi, usimulizi uendelezaji, usimulizi onyesho, usimulizi mtuo na usimulizi wa idadimarudio. Uchunguzi wa madhumuni ya pili ulitambua kuwa riwaya teule imetumia wahusika ambao wamekuwa nguzo muhimu katika uendelezaji wa hadithi ya *Siri Sirini*. Wahusika wamesawiriwa kama: Mhusika mkwezwa, mhusika wa kimapinduzi na mhusika wa kisaikolojia. Matokeo haya yanatazamiwa kumsaidia msomaji kuuelewa muundo wa riwaya teule kwa kuzingatia kipengele cha usimulizi na kuelewa ujumbe unaowasilishwa katika simulizi. Utafiti utafaidi jamii ya wasomi na waandishi wa kazi za kibunifu za Kiswahili kuelewa zaidi dhana ya usimulizi na nafasi yake katika utunzi. Utafiti utaonyesha jinsi nyingine ya kuichanganua riwaya kwa kutumia nadharia ya naratolojia mbali na mbinu zingine kama zile za kimtindo, kimaudhui na za lugha. Vilevile, matokeo ya utafiti yataongezea marejeleo katika uwanja wa uhakiki wa fasihi ya Kiswahili na kutumika na watafiti wa kazi za kibunifu.

6.3 Mapendekezo

Utafiti huu ulishughulikia mbinu mbalimbali za usimulizi zilizotumika kuisimulia riwaya trilojia ya *Siri Sirini* na jinsi wahusika walivyosawiriwa. Nadharia ya naratolojia ilitumika katika uchunguzi huu. Mapendekezo ni kwamba tafiti zaidi zifanywe kuchunguza mbinu za usimulizi katika tungo zingine za fasihi andishi. Hali kadhalika riwaya trilojia ya *Siri Sirini* inaweza kutafitiwa kwa kutumia nadharia zingine tofauti na nadharia ya naratolojia.

MAREJELEO

- Abrams, M. H. (1999). *A Glossary of Literary Terms*. (Seventh edition). San Antonio: Earl Mcpeek.
- Ali, A. R. (2015). Kuchunguza Dhana zilizobebwa na Wahusika na zinazolandana na Majina yao: Uchunguzi katika Riwaya ya *Kiu* na *Kiuyahaki*. Tasnifu ya M.A(isiyochapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Ali, J. A. E. (2017). Kuchunguza Dhamira katika Riwaya ya *Kiu* ya Mohamed Suleiman Mohamed. Tasnifu ya M.A(isiyochapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Arege, T. I. M. (2012). Narration in Swahili Narrative Poetry: an Analysis of *Utenzi wa Rasi'l ghuli*. Tasnifu ya Phd (isiyochapishwa). University of Nairobi.
- Ayramo, S. M. (2011). 'Narrative' in Serious or Learning Game Design Research. Working with Stories: Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from 2nd European Narratology Network Conference; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Bal, M. (1999). *Narratology: Introduction to the Theory of Narrative*. (Second edition). London: University of Toronto Press.
- Barthes, R. (1966). *An Introduction to the Structural Analysis of Narrative*. London: Routledge.
- Bernkopf, A. (2011). Between Stage and Literature: Romance Ballet's Narrative Strategies. Working with Stories: Narrative as a Meeting place For Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2nd European Narratology Network; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Bertoncini, E. (2000). The Opposition Between Open and Closed spaces in Mohamed S. Mohammed's short story 'Uhuru wa Siku Moja': *Kongamano la kimataifa Kiswahili 2000 proceedings uk 34-43*.
- Bom, A. K. (2011). Hans Christian Anderson: A story of Experience. Working With Stories: Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2nd European Narratology Network Conference; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Burundi, R. N. (2011). Usimulizi wa *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*: Tasnifu ya M.A.(isiyochapishwa) Chuo Kishiriki cha Chuka.
- Chimerah, R. M. (1995). *Nyongo Mkalia Ini*. Nairobi: Oxford University Press.
- Chimerah, R. M. (2013). *Siri Sirini 1*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Chimerah, R. M. (2014). *Siri Sirini 2*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Chimerah, R. M. (2014). *Siri Sirini 3*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

- Chirila, S. (2011). Tension and Paradox in the Construction of Collective Identity through Narrative in Toni Morrison's *paradise*. Working with Stories: Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2nd European Narratology Network Conference; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Drach, I. (2011). Montage Techniques in the Novel *Berlin Alexanderplatz* by A. Döblin and the film *Berlin Alexanderplatz*. Working with Stories: Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2nd European Narratology Network Conference; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Elshout, H. (2011). No Learned Rhetorical Figures. Working with Stories: Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2nd European Narratology Network Conference; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Engberg, A. (2011). Life stories and Christian Zionist Ideology. Working with Stories: Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2nd European Narratology Network Conference; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Eslamich, R. (2016). Pastiche in Paul Auster's *The New York Trilogy*. Retrieved from <http://dx.org/10.7575/aic.all.v.7n.5p197>. Accessed on October 2018.
- Fakih, S. J. (2017). Kutathmini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Utengano na Kamwe si Mbali Tena*. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Fisher, W. R. (1984). Narration as a Human Communication Paradigm. The Case of Public Moral Argument. Retrieved from *Communication Monographs volume 51, (1) 1-22*. Accessed on July 2014.
- Fludernik, M. (2009). *An Introduction to Narratology*. New York: Routledge.
- Ghosh, S. (2016). Ferdinand De Saussure and the Development of Structuralism. Retrieved from *International Journal of Sociology and Social Anthropology 1 (1);59-64*. Accessed on Dec.2017.
- Grund, C., & Wesley, W. (2011). Narrative and Music. Working with Stories. Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2nd European Narratology Network Conference; Kolding: Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Habib, M. A. R. (2011). *Literary Criticism from Plato to the Present: An Introduction*. Malden, MA: Wiley-Blackell.
- Haji, A. V. (2018). Kutathmini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo na Asali Chungu: Utafiti Linganishi*. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

- Harmon, W., & Hugh, C. (2000). *A Handbook to Literature*. (Eight edition). New Jersey:Prentice Hall.
- Kavuria, P. N. (2008). Dhuluma dhidi ya Watoto katika Riwaya za Kiswahili. Tasnifu ya M.A. (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Kilonzo, P. K. (2015). Ujitambuzi na Utambulisho wa Kijinsia katika Riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kimani, N. (1987). *Uhakiki wa Riwaya za Visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Kimaru, H. (2016). African Writers Watered Seed of my 1,062-page Kiswahili to me. In Lifestyle. Saturday Nation. Nairobi: Nation Media Group.
- Koboldt, D. (2018). Writing a Trilogy: Essential Tips for Crafting a Three- Part Series. Retrieved from <https://writersdigest.com>. Accessed on Feb19, 2018.
- Lilywhite, K. (2018). *Nairobi Museum to Host Exhibition on Origins of Quilting*. In Art Talk. Saturday Nation. Nairobi: Nation Media Group.
- Longhorn (2013). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Madsen, K. (2011). New Family Narrations. Working with Stories: Narrative as a Meeting Place for Theory, Analysis and Practice; Proceedings from the 2nd European Narratology Network Conference; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Mtule Educational Publications Ltd.
- Maina, M. (2019). *Storytelling to Unravel Our History*. Retrieved from <https://www.nation.co.ke/>. Accessed on 7/1/2019.
- Maosa, N. (2017). Let us bring back the Magic of Storytelling. In *Readers corner*. Saturday Nation. Nairobi: Nation Media Group.
- Massoud, S. M. A. (2013). Maudhui na Fani katika Tamthilia za Kiswahili: *Utafiti Linganishi wa Tamthilia za Mashetani na Kivuli Kinaishi*. Tasnifu ya Phd (Isiyochapishwa) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Matei, A. K. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mayaka, G. (1991). Ukengeushi wa Wasomi katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mbatiah, M. (1997). Uchunguzi wa Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona na Mzingile* katika *MULIKA NA 24uk 1-11*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.


- Mlacha, S. A. K. (1996). Utamaduni wa Mwafrika katika Riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka* katika *MULIKA NA* 23uk24-35. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mohamed, S. A. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za nathari ya Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mohochi, E. S. (2000). Usimulizi wa Riwaya ya *Nyongo Mkalia Ini*. Retrieved from *Nordic Journal of African Studies* 9(2): 49-59. Accessed on August 2015.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Publishers Ltd.
- Murithi, J. S. (2017). Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed. Tasnifu ya Phd (isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Musee, A. D. (2007). Matumizi ya Majazi kama Mkakati wa Kuepuka Upiganaji Marufuku katika Riwaya za Mkangi: *Mafuta na Walenisi*. Tasnifu ya M.A(isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Mwangi, E. (2013 January). Kiriamiti goes to the movies. In Big Screen. Saturday Nation. Nairobi: Nation Media Group.
- Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa shule za sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Njogu, K., & Chimera, R. M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Norlyk, B. (2011). The Strategic use of Narrative and Nattative Elements in Corporate Communication & Corporate Genres. Working with Stories: Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2nd European Narratology Network Conference; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.
- Nyamete, F., Buliba, F. A., & Kamau, N. G. (2016). Ufafanuzi wa Vichocho vya Migogoro ya Kindoa kama Vinavyosawiriwa katika Riwaya ya *Kidagaa Kimemuozea*. Retrieved from *International Journal of Advanced Education and Research*.VOL 1: Issue 9 uk19-27. Accessed on 25/12/2018.
- Ochenja, R. (2008). Sifa zinazofanya Riwaya za Walibora Kubainika Zaidi kama Maigizo kuliko masimulizi ya nathari. Tasnifu ya M.A(isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.

- Odegaard, E. E. (2011). Narrative Practices as a Site for Studying Conditions for Children's Cultural Formation. Working with Stories: Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2nd European Narratology Network Conference; Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Ong'ondi, B. E. (2005). Uhakiki wa Usimulizi katika Riwaya ya *Walenisi* ya Katama Mkangi. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Otieno, O. (2017). Profesa Chimerah. It is the Season of Harvest for Kiswahili in the Region. In Book Review. Saturday Nation. Nairobi: Nation Media Group.
- Otieno, O. J. (2017). Uchanganuzi Kipragmatiki wa Sitiari katika Nyimbo za Taarab: Mfano wa Mzee Yusuf na Mwanahawa Ally. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Kisii.
- Publication Manual of the American Psychological Association (sixth Edition). 750 first Street NE, Washington DC 2000.
- Qureshi, A. (2014). 'A Taste of Expressive Storytelling'. In Lifestyle: Sunday Nation. Nairobi: Nation Media Group.
- Rice, K. (2018). Chimamanda Ngozi Adichie and Beyond: The Best Books on Nigeria. Retrieved from <https://www.penguinrandomhouse.com>. Accessed on July 26, 2018.
- Robert, S. B. (1966). *Kusadikika*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Rono, P. (2013). Uhakiki wa Kimaudhui na Kifani wa *Kidagaa Kimemuozea*. Tasnifu ya M.A(isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Sabula, M. A. (2014). Nafasi ya Wanawake katika Uhifadhi wa Mazingira katika Riwaya ya *Nakuruto: Mtazamo wa Fasihi ya Ufeministi wa Kiekolojia*. Tasnifu ya M.A (isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Senkoro, F. (1988). Uhakiki wa Riwaya ya *Shida* katika *MULIKA NA 20* uk 30-34. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Shahbaz, P. (2011). Symbolic Feminine Role in Indo-Persian Narratives. Working with Stories: Narrative as a Meeting place for Theory, Analysis and Practice: Proceedings from the 2ndEuropean Narratology Network Conference;Kolding. Retrieved from www.narratology.net/node/86. Accessed on July 2014.
- Shitemi, J. M. (2011). Uhakiki wa *Utenzi wa Siri li Siriali*. Tasnifu ya M.A(isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Swaleh, A. (1997). The Image of Woman in S. A Mohamed's *Tata la Asumini* katika *JUZUU 60* uk 25-30. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Todorov, T. (1971). The 2 Principles of Narrative. *Diacritics, Vol, 1, No.1 (Autumn 1971)*uk 37-44. Retrieved from <http://www.jstor.org/stable/466558>. Accessed on August 2018.

- Traore, F. A. (2001). Taarab and Swahili Prose. Retrieved from *Swahili Forum VIII AAP 68* uk123-128. Accessed on July 2014.
- TUKI (2006). *English-Swahili Dictionary* (Third Edition). Dar-es Salaam: TUKI.
- Vonyoli, A. J. (2004). Hadithi kama Chombo cha Maudhui katika Fasihi: Uchanganuzi wa Riwaya za Mkangi, *Mafuta na Walenisi*. Tasnifu ya M.A(isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemuozea*. Nairobi: Spotlight Publishers (EA) Limited.
- Wambui, J. (2018). Usimulizi katika Riwaya ya *Dharau ya Ini*. Tasnifu ya M.A(isiyochapishwa) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2002). Place and Placelessness in Kiswahili Literature: The Role of Setting in Kiswahili Creative Writing katika *JUZUU65* uk 97-103. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K. W. (2003). Influence or Intertextuality? A Comparative Study of Kezilahabi's *Nagona* and *Mzingile* and Juan Rulfo's *Pedro Paramo* katika *JUZUU 66* uk 49-58. University of Dar es Salaam.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.
- Wichlacz, S. (2006). Issues of Narration. Voice-over in film. Retrieved From <http://msal-tresea.rchjournal.wordpress.com>. Accessed on July 2015.
- Yenjela, D. W. (2015). Invoking Memories of Legendary African Women. A Reading of Rocha Chimera's Trilogy *Siri Sirini* pp48-65. *Pathways to African Feminism and Development, Journal of African's Studies Centre*. Retrieved from journals.uonbi.ac.ke/index.php, Vol 1 No3. Accessed on August 2018.
- Yenjela, D. W. (2017). Narrated Histories in Selected Kenyan Novels, 1963-2013. Tasnifu ya Phd (isiyochapishwa) Stellenbosch University. Retrieved from <https://scholar.sun.ac.za>. Accessed on July 2018.
- Zhang, M. (2016). Youth Narrative in Feng Tang's *The Beijing Trilogy*. Retrieved from <https://scholarworks.umass.edu/masters-thesis-2/385>. Accessed on November 2018.

VIAMBATISHO

Kiambatisho 1: Kibali Cha utafiti Kutoka Chuo Kikuu cha Chuka


CHUKA UNIVERSITY
Knowledge is Wealth (Sapientia divitia est) Akili ni Mali

CHUKA UNIVERSITY INSTITUTIONAL ETHICS REVIEW COMMITTEE

Telephones: 020-2310512/18
Direct Line: 0772894438
Email: info@chuka.ac.ke

P. O. Box 109-60400, Chuka
Website: www.chuka.ac.ke
8TH JULY 2019

REF: CUIERC/ NACOSTI/025
TO: LUCYLINE NJERI MWONGELA

Dear Sir/madam

RE: USIMULIZI KATIKA RIWAYA TRILOJIA YA KISWAHILI: MFANO WA SIRI SIRINI.


This is to inform you that *Chuka University IERC* has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is *NACOSTI/NBC/AC-0812*. The approval period is *1st April, 2019 – 31st March, 2020*.

This approval is subject to compliance with the following requirements;


- i. Only approved documents including (informed consents, study instruments, MTA) will be used
- ii. All changes including (amendments, deviations, and violations) are submitted for review and approval by *Chuka University IERC*.
- iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours of notification
- iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affected safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours
- v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions.
- vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal.
- vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to *Chuka University IERC*.

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) <https://oris.nacosti.go.ke> and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely







PROF. ADIEL MAGANA
CHAIRMAN CHUKA UNIVERSITY IERC

Chuka University is ISO 9001:2015 Certified...



Inspiring Environmental Sustainability for Better Life

Kiambatisho 2: Kibali Cha Utafiti

 REPUBLIC OF KENYA	 NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION
Ref No: 496281	Date of Issue: 21/August/2019
RESEARCH LICENSE	
	
This is to Certify that Miss. LUCYLINE MWONGELA of Chuka University, has been licensed to conduct research in Tharaka-Nithi on the topic: USIMULIZI KATIKA RIWAYA TRILOGIA YA KISWAHILI: MFANO WA SIRI SIRINI for the period ending : 21/August/2020.	
License No: NACOSTIP/19/646	
496281 Applicant Identification Number	 Director General NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION
	Verification QR Code 
NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.	